

## **BUNGE LA TANZANIA**

---

### **MAJADILIANO YA BUNGE**

---

### **MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Tano - Tarehe 13 Februari, 2006**

*(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika(Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

### **NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:**

Taarifa ya mwaka na Hesabu za Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2005 (*The Annual Report and Accounts of the Presidential Parastatal Sector Reform Commission for the year ended 30<sup>th</sup> June, 2005*).

### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):**

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2004 (*The Report of Controller and Auditor General for the Financial Year ended 30<sup>th</sup> June, 2004*).

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 48

**Barabara ya Mima - Mkanana - Wotta - Kibakwe**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kuifanyia matengenezo makubwa barabara ya Mima - Mkanana - Wotta hadi Kibakwe; na kwa kuwa barabara hiyo ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa maeneo hayo:-

(a) Je, Serikali ina maelezo gani kwa wananchi wa Mima, Mkanana na Wotta kuhusu matengenezo ya barabara hiyo?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kutengenezwa kwa barabara hiyo ya Mima - Mkanana hadi Wotta kutarahisisha sana usafirishaji wa mazao na abiria katika maeneo hayo kuliko hali ilivyo sasa ambapo wananchi hutembea kwa miguu kutoka Mkanana hadi Mima/Berega na kutoka Mkanana hadi Wotta?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Barabara ya Mima - Mkanana - Wotta - Kibakwe yenyewe urefu wa kilometra 69 inapitika kwa urahisi katika kilometra 24 tu kati ya Kibakwe na Wotta, ambapo sehemu ya Mima na Mkanana kilometra 21 inapitika kwa shida hasa kipindi cha masika na kilometra 25 zilizobaki kati ya Wotta na Mkanana hazipitiki kabisa kutokana na makorongo makubwa yanayokatisha barabara hivyo kusababisha sehemu hiyo ya barabara kujifunga kabisa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hiyo na ndiyo sababu kwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, imekuwa ikifanya matengenezo ya mara kwa mara katika barabara hii kati ya Kibakwe na Wotta kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara (*Road Fund*), isipokuwa sehemu ya barabara kati ya Wotta, Mkanana hadi Mima yenyewe kilometra 45 ambayo inahitaji fedha za maendeleo kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Halmashauri imetengeneza barabara yenyewe urefu wa kilometra 24 kati ya Kibakwe na Wotta na mwaka 2005/2006 Serikali imeendelea na matengenezo ya kawaada na zile sehemu korofii kati ya Kibakwe na Wotta.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa itaiweka barabara hiyo kwenye mpango wa maendeleo kwa kutumia fedha za *Local Government Capital Development Grant* ili kufanya yafuatayo:-

- Kufanya matengenezo ya maeneo korofii (*Sport Improvement*) kati ya Mima na Mkanana;

- Kufanya matengenezo ya muda maalum (*Periodic Maintenance*) kati ya Mkanana na Wotta;

- Kufanya matengenezo ya kawaida (*Routine Maintenance*) kati ya Matonga na Wotta; na

- Kujenga kwa awamu madaraja na Makalvati yanayohitajika kati ya Wotta, Mkanana hadi Mima.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kutengenezwa kwa barabara hii ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Vijiji vya Mkanana na Mima, kwa kuwa kuwepo kwa barabara nzuri kutarahisisha usafirishaji wa mazao na abiria na kupunguza adha ya kutembea kwa miguu.

Aidha, barabara nzuri kati ya vijiji hivyo vya Mima-Mkanana-Wotta, itasaidia sana wananchi wa maeneo hayo kupata soko la uhakika kwa ajili ya mazao yao na hivyo kupunguza umaskini katika maeneo hayo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa kazi ya Wabunge ni kuishauri Serikali na ukisha shauri Serikali kwamba mfuko huu wa *Road Fund* asilimia 30 inayotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara vijijini haitoshi.

Sasa je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya kuongeza toka asilimia 30 angalau ifike asilimia 40 Mfuko wa *Road Fund* ili tuweze kutengeneza barabara vijijini. Kwa sababu barabara vijijini ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwa hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi kwamba barabara hiyo itatengenezwa katika awamu hii ya mwaka 2006/2007 kuongezeka kwa asilimia 30 kunategemeana na uwezo wa Serikali. Kwa hiyo, namhakikisha Mheshimiwa George Lubeleje kwamba kwa mwaka huu tutahakikisha kwamba hilo tatizo tunalipunguza. Ahsante. (*Makofii*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kinachoulizwa hapa na Mheshimiwa Mbunge ni ile *formula* ya kugawa zile fedha za *Road Toll Fund*. *Formula* iliyopo inasema asilimia 30 kwa asilimia 70. Sasa kinachoulizwa hapa kiongezeke kutoka asilimia 30 zifiki asilimia 40 ndiyo swali ambalo limeulizwa hapa. Je, Serikali ipo tayari kuongeza kiwango cha *Road Toll Fund* inayokwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya iwe asilimia 40 na *Road Fund* ibaki na asilimia 60?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, tunatoa ahadi Serikali kwamba tutaliangalia suala hili. (*Makofî*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata namba 49 sitaruhusu lijibiwe kwa sababu sasa hivi katika Mahakama Kuu chini ya jopo linaloongozwa na Jaji Kiongozi yaliyomo maudhui ya swali hili yanashughulikiwa na Mahakama chini ya maombi ya madai Na. 49 ya mwaka 2005 ambapo taasisi inayoitwa *Legal Human Rights Centre* kama mwombaji wanawashtaki Mwanasheria Mkuu, Thomas Ole Sabaya nadhani ndiyo DP anayetajwa, Alexander Lyimo, *Serengeti District Council* na *Bonchugu Village Council*.

Sasa kwa mujibu wa sheria za nchi yetu suala kama linasubiri hukumu na linashughulikiwa Mahakamani hatuwezi tukalijadili hapa Bungeni. (*Makofî*)

Na. 50

### **Baraza la Mawaziri**

#### **MHE. GRACE S. KIWELU aliuliza:-**

Kwa kuwa kulikuwepo na mpango uliopendekezwa na *Civil Service Reform Commission* ilioongozwa na Mheshimiwa Dr. Mary Nagu wa kupunguza ukubwa wa Serikali Kuu na kuongeza nguvu na madaraka Mikoani na Wilayani:-

Je, uteuzi wa Baraza kubwa la Mawaziri uliofanywa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, unakwenda sambamba kisera na mpango huo?

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA aliijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge Viti Maalum, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza programu ya kuboresha Utumishi wa Umma kwa awamu, awamu ya kwanza ilianza mwaka 1993 na ilikamilika 1999.

Mheshimiwa Spika, programu inayօendelea sasa ni mwendelezo wa mageuzi hayo na imepangwa kukamilika mwaka 2011. Katika awamu ya sasa, Serikali inajenga uwezo wa watumishi wake ili kuwa na watumishi wa umma watakaokuwa chachu ya maendeleo, kwa kusitiza utendaji unaozingatia matokeo (*Results Oriented Management*).

Katika mfumo huu wa Memejimenti, malengo na mikakati ya kufikia malengo hayo yameainishwa ikiwemo muundo wa Serikali, raslimali na nguvu kazi ya kufikia malengo ya kila Wizara na Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Grace Kiwelu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Serikali hayapimwi kwa ukubwa au udogo wake, bali kwa tija na ufanisi katika kutekeleza majukumu yanayoikabili.

Muundo wa Serikali ya Awamu ya Nne umezingatia *agenda* na matakwa ya wananchi ya wakati tulio nao hivi sasa. *Agenda* na matakwa ya kipindi hiki yameleta majukumu mapya na pia kuweka umuhimu wa juu katika baadhi ya majukumu yaliyopo ambayo muundo wa siku za nyuma usingeweza kuyatekeleza kwa ufanisi na tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, majukumu mawili ya msingi yamewekwa bayana kwa Serikali ya Awamu ya Nne, nayo ni na nanukuu:-

(a) Kuitoa Tanzania kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na tegemezi na kujiingiza katika mkondo wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea.

(b) Kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwezeshaji katika ujenzi wa uchumi na kutokomeza umaskini. Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Serikali pia inaendelea na utekelezaji wa mpango kabambe wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA). Kutokana na malengo haya Serikali inahitaji timu ya usimamiaji na watekelezaji ambao kila mmoja wao bila kugubikwa na majukumu mengi na mazito anatekeleza wajibu wake kwa uadilifu, kwa wakati, kwa makini na kwa ufanisi na tija.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza azma hiyo, Serikali imeunda Wizara mpya kutokana na idara na vitengo vya Wizara za zamani ili kuongeza mafanikio zaidi ya utendaji inayozingatia matokeo ili kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Hivyo kwa kuzingatia msukumo wa mahitaji ya Watanzania kwa sasa kama vile maji, umeme, ulinzi na usalama, chakula, uchumi imara na utawala bora, kulikuwa na umuhimu wa kuangalia upya muundo wa Serikali ili uwiane na majukumu yaliyopo. (*Makofi*)

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake marefu na mazuri. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza. (*Makofi*)

Kwa kuwa Serikali imekuwa kubwa kwa maana ya Mawaziri na Makatibu Wakuu, je, Serikali inaweza kuliambia Bunge hili Tukufu ni kiasi gani cha fedha kitaongezeka kwa maana ya magari, nyumba, mishahara na malazi?

La pili, Serikali haioni ukubwa huu wa Serikali umekuwa mkubwa utainyima Serikali kutoa zile huduma vizuri kama vile elimu, afya na maji? (*Makofi*)

**SPIKA:** Sehemu ya kwanza ya swali siwezi kuiruhusu kwa sababu inahitaji takwimu ambazo itabidi zitolewe. Hilo ni swali jipya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri, nafikiri tunahitaji majibu kwenye sehemu ya pili. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, sawa na jibu langu la msingi kama nilivyozungumza ukubwa wa Serikali haupimwi kwa gharama bali tunapima kwa ufanisi. (*Makofi*)

Hivyo namwomba Mheshimiwa Grace Kiwel, aangalie ufanisi wa Serikali ambao utatokana na ukubwa wa Baraza la Mawaziri bila ya kuangalia gharama. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kweli Mheshimiwa Waziri amesema ufanisi haupimwi kwa ukubwa lakini kwa kuwa ukubwa wenyewe wa Baraza la Mawaziri ni lazima uendane na ufanisi wa watu walio chini yake; na kwa kuwa *reform* iliyofanywa mwaka 1990 ilichukua dhana kwamba wale waliokuwa wameingia kwanza ndani ya Serikali ndio wanaondoka au wazungu wanasema *first in ndiyo last out*.

Mheshimiwa Spika, je, hili Baraza kubwa la Mawaziri lina watumishi wa aina gani ambao kweli wataweza kulihudumia Baraza hili kubwa ambapo wengi waliomo ndani ya Serikali ni wazee na vijana wote wako nje? (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyingine tena nadhani swali hili linaleta hoja mpya kabisa ya ufanisi na kadhalika. Tunaendelea. (*Makofi*)

Na. 51

### **Mkakati wa Kupeleka Umeme Vijijini**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme ni nyenzo muhimu katika maendeleo kwa ujumla hapa nchini; na kwa kuwa Serikali imeandaa mikakati maalum ya kupeleka umeme Vijijini ikiwa ni pamoa na kupitisha Bungeni Sheria ya Kuanzisha Taasisi kwa jina la Wakala wa Nishati Vijijini na Mfuko wa Nishati Vijijini:-

(a) Je, Taasisi hiyo inayoitwa Wakala wa Nishati Vijijni imeanza lini?

(b) Je, Mfuko wa Nishati Vijijni umetengewa kiasi gani cha fedha?

(c) Je, ule mradi wa kupeleka umeme huko Mgashi katika Jimbo la Bumbuli utaanza mwezi gani ikizingatiwa kuwa Serikali iliahidi kuwa utaanza mwaka 2006?

## **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Wakala wa Nishati Vijiji haijaanza rasmi. Baada ya Bunge kuitisha Sheria ya Kuanzisha Wakala na Mfuko wa Umeme Vijiji, Aprili, 2005. Wizara sasa inakamilisha mchakato wa kupata watendaji wake. Tunatarajia mchakato huu utakuwa umekamilika ifikapo mwezi Aprili, 2006, na Taasisi zitaanza kutoa huduma kuanzia mwaka ujao wa fedha, yaani 2006/2007.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa Bajeti ya mwaka wa fedha, 2005/2006, Wizara imetenga fedha jumla ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya matumizi ya shughuli ya mchakato wa kuanzisha Taasisi hizi na matumizi ya Ofisi ikiwa ni pamoja na mishahara ya watumishi wake watakaoajiriwa.

(c) Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme kijiji cha Mgashi katika Jimbo la Bumbuli unahuisha ujenzi wa laini ya umeme ya kilovoti 11 kutoka Belei hadi Mgashi umbali wa kilometri 20.8 Laini hii itapita katika vijiji vya Kwesina, Baga, Mgashi na Nkosi. Shirika la Umeme *TANESCO*, linatarajia pia kuweka vipoza umeme (*transforma*) 4 na kujenga laini ndogo za usambazaji umeme zenye umbali wa kilometri 9.5 na kuwaunganishia wateja. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa shilingi za Kitanzania milioni 600.0.

Kutokana na hali mbaya ya kifedha inayoikabili *TANESCO* kutokana na ukame, fedha za kugharamia ujenzi wa mradi huu zitaombwa Serikalini katika Bajeti ijayo ya mwaka 2006/2007.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Nilikuwa nadhani Spika wakati mwengine pengine ni *right handed* zaidi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mradi huu ulishakubaliwa mwaka 1998, je, Waziri haoni kwamba kuna haja ya kutumia mbinu mbalimbali ili kuondoa manung'uniko ya wananchi wale kwa sababu fedha zilizotengwa mwaka 1998 zilitumika Kitaifa wakati wa ukame mkali na sasa hivi wanasubiri kwa hiyo, majibu haya yanaonekana kwamba yanasegeza muda tu kwa sababu Serikali ilisema utaanza mwanzoni mwa mwaka huu sasa inakuwa bajeti ya 2006/2007.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu nililowasilisha hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri nafikiri tumeweka wazi kwamba mradi huu utashughulikiwa kutokana na kuomba fedha katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 na suala la matatizo ya *TANESCO* nafikiri yanafahamika nchi nzima na suala la ukame linafahamika. Naomba lieleweke hivyo.

**Kupanda kwa Bei ya Umeme**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania kama nchi nyingine za Mashariki na pembe ya Afrika imekumbwa na uhaba mkubwa wa mvua ambao umeathiri uzalishaji wa umeme nchini; na kwa kuwa kupanda kwa bei ya mafuta dunia pia kumeathirika upatikanaji wa umeme kwa bei nafuu nchini hali iliyosababisha *TANESCO* kupandisha bei ya umeme:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kupanda kwa bei ya umeme kumefanya umeme uonekane kuwa ni bidhaa ya anasa kwa Watanzania wengi wenye kipato kidogo badala ya kuwa nyenzo ya kusukuma gurudumu la maendeleo, na hivyo kuwa kikwazo kwa uchumi na uhifadhi wa mazingira kwa ujumla?

(b) Je, Serikali iko tayari kufuta ukiritimba wa utoaji wa umeme na kuruhusu Makampuni mengine kama *IPTL* na *Songas* yauze umeme moja kwa moja kwa wananchi jambo ambalo linaweza kupunguza gharama za umeme nchini?

(c) Je, gharama za kuwalipa *Net Group Solutions* zimechangia kwa kiasi gani kupanda kwa bei ya umeme nchini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ya niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba umeme ni muhimu kwa maendeleo yetu. Hata hivyo ili *TANESCO* iendelee kutoa huduma hivyo haina budi kufidia gharama zake za uendeshaji kunatokana na uuzaji wa umeme na pale inapobidi Serikali imekuwa ikitoa ruzuku kwa *TANESCO* ili bei isipande sana.

(b) Mheshimiwa Spika, mwaka 1992 Serikali ilitangaza sera mpya ya umeme na kuondoa ukiritimba wa *TANESCO* na kuruhusu sekta ya umeme iendeshwe kwa misingi ya kibashara ya ushindani. Sera hiyo inaruhusu Makampuni mbalimbali kuwekeza kwenye sekta hiyo. Tayari makampuni ya *IPTL*, *Songas*, *Kiwira* na *TanWat* yamezalisha umeme na kuiuzia *TANESCO*. Kuhusu kuruhusu makampuni hayo kuuza umeme moja kwa moja kwa wateja ni kwamba makampuni hayo yanayozalisha hayako tayari kuwauzia wateja wadogo wadogo kwani gharama za kuhakikisha umeme huo kuwafikia hao wateja zitakuwa kubwa na pia wanaogopa upotevu wa umeme wakati wa kusafirisha.

(c) Mheshimiwa Spika, gharama za kuwalipa *Net Group Solutions* hazichangii kupanda kwa bei ya umeme nchini, kwa sababu *TANESCO* inapata ufadhili wa moja kwa

moja kutoka Shirika la Maendeleo la Sweden yaani *Swedish International Development Agency* kwenye kulipa ada ya *Net Group Solutions* ya *USD 486,000* kwa kila robo ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana *Net Group Solutions* walilipwa na wafadhili jumla ya *USD 1.9* yaani *fixed retainer fee*.

Aidha, katika mkataba wa *Net Group Solutions*, yapo pia malipo ya *bonus* yanayofanywa na *TANESCO* pale wanapofanya vizuri.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo moja la nyongeza.

Je, Serikali iko tayari kuondoa ushuru wa *VAT* kwenye mafuta kama vile dizeli, petroli pamoja na *petroleum product* ili kupunguza unafuu wa umeme na wananchi waweze ku-afford kununua umeme na hatimaye tuweze kutunza mazingira yetu?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala la bei ya umeme ni moja ya kazi ambayo sasa hivi pale Wizarani tunaifanya kwa maana ya kuitathmini na ni mambo mengi. Si suala la *VAT* tu. Unapoingilia suala la kodi unaingilia mfumo mzima wa matumizi na mapato ya Serikali. Kwa hiyo, ni suala zito na inabidi litathminiwe kwa uhakika. Lakini nataka niseme kwamba tunayo kazi ya kutazama upya suala zima la bei za umeme naomba mtupe muda tufanye kazi hiyo. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa *Net Group Solutions* tayari walishalipwa *bonus*, je, kuna ufanisi gani uliopatikana wakati wananchi hawana umeme na menejimenti yao bado haijaonekana kuonyesha kupunguza matatizo kuliko ile menejimenti iliyokuweko ya Watanzania?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, wakati wa semina pale *Ubungo Plaza* na wakati Wizara yangu inawasilisha mada juu ya hali ya umeme nichini, nilitoa taarifa kwamba yapo matatizo ya uendeshaji ndani ya Shirika la Umeme na nilisema kwamba Serikali inalifanya kazi. (*Makofi*)

Nataka niseme kwamba walipoingia *Net Group Solutions* kipindi cha mwanzo palionyesha dalili kwamba wangeweza wakafanya vizuri na kwa kweli walifanya vizuri kwa maana ya eneo moja la ukusanyaji wa mapato. Lakini nilisema baadaye kwamba sisi Serikalini tunatambua kwamba yako matatizo na matatizo hayo tunayashughulikia. (*Makofi*)

**Kurudishwa kwa JKT**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeamua kurudisha tena Jeshi la Kujenga Taifa kwa manufaa kama yale yaliyoanzisha Jeshi hilo miaka ya nyuma:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa inatakiwa itoe ufanuzi wa kina juu ya kusudi la kurudisha jeshi hilo na kusema walengwa watakuwa ni watu gani?

(b) Je, kwa wale waliotakiwa kujiunga na jeshi hilo kwa mujibu wa sheria kabla ya kusitishwa kwa shughuli zake wamewekewa utaratibu gani baada ya kurudishwa tena kwa jeshi?

(c) Kwa kuwa vijana wetu wanaomiliza darasa la saba na kukosa nafasi za kuendelea na masomo wamefurahia sana uamuzi wa Serikali wa kurejesha jeshi hilo, je, watahusishwa namna gani katika utaratibu huo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa mwaka 1963 na baadaye kutungwa sheria mwaka 1964. Tokea mwaka wa 1964 hadi mwaka 1966 vijana walikuwa wanajiunga kwa utaratibu wa kujitolea (*volunteers*). Utaratibu huo ulioneckana kuwa na mapungufu kwani vijana waliokuwa wakijiunga kwa wingi ni wale waliomiliza elimu ya darasa la saba. Mnamo mwaka 1966, sheria ya JKT ilifanyiwa marekebisho kwa kujumuisha vijana waliomiliza elimu ya kidato cha nne na zaidi. Vijana hao walilazimika kutumikia mkataba ndani ya JKT kwa mujibu wa sheria (*Compulsory*). Kutohana na matatizo ya kiuchumi yaliyojitekeza, Serikali mnamo mwaka 1987 ililazimika kusitisha uingiaji vijana kwa utaratibu wa kujitolea. Hali hiyo iliendelea na hadi ilipofika mwaka 1994, Serikali ililazimika kusitisha kwa vijana wote kujiunga na JKT.

Mheshimiwa Spika, kufuatia wimbi la mabadiliko ya mfumo wa maisha duniani na athari za utandawazi, uchumi huria na kadhalika, tabia za vijana wengi wa Kitanzania zimebadilika. Wengi wa vijana wetu wametawaliwa na tamaduni za kigeni ambazo haziendani na maaadili na utamaduni wa Kitanzania. Ili kurejesha maadili kwa vijana wa Kitanzania, Serikali mnamo mwaka 2000, iliamua kurejesha utaratibu wa vijana wetu kujiunga na JKT kwa lengo la kuwapatia mafunzo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mgana Msindai, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kusudi la kurejesha utaratibu wa vijana wetu kujiunga na JKT ni kuwapa malezi bora kwa kuwafunza ukakamavu, nidhamu na Utaifa, mbinu za ulinzi na kujenga ari ya kupenda kazi za mikono mafunzo hayo yanalenga katika kuwaweka vijana wawe raia wema na kuwa tayari kushiriki katika ujenzi wa Taifa lao walengwa wa mafunzo hayo ya JKT ni vijana wote wa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa kwa kuwa ndio kwanza tumelifufua upya Jeshi la Kujenga Taifa, ni mapema mno kuwa na utaratibu wa kuwachukua tena vijana wote waliokusudiwa kwa mujibu wa sheria kutokana na idadi ya kuwa ni kubwa sana.

Suala hili linapaswa kuamuliwa kwa makini sana na pia kwa kutegemea kwa kuongezeka kwa mapato ya Serikali na kwa hiyo kukua kwa Bajeti ya JKT. Kwa hivi sasa vijana walio katika kundi hili nao wanaruhusiwa kwenda JKT kwa mpango wa kujitolea tu.

(c) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo juu utaratibu wa sasa wa kuwachukua vijana kwa lengo la kujiunga na JKT unawahuisha vijana wote kwa njia ya kujitolea wakiwemo wale waliomaliza elimu ya darasa la saba.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza.

Kwa kuwa sasa hivi JKT ndio mahali vijana wetu wanaponolewa na kuwa na sifa nzuri. Sasa Serikali haiioni kwamba inapohitaji vijana wetu kujiunga na Polisi, Jeshi, Magereza, Uhamiaji na kadhalika wote watoke JKT ambao wameshapimwa kuliko kuchukua vijana wa mtaani?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mgana Msindai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge lakini itategemeana na vijana hao na sifa zinazohitajika kujiunga na sehemu ambazo wanatarajia kujiunga asante.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swalii la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sasa hivi vijana wengi huja kwetu Wabunge na kuomba wajiunge na Jeshi la Kujenga Taifa. Je, Serikali inaweza kuanzisha vituo hivi kila Wilaya ili kila kijana anayetaka kujiunga ajiunge?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, sijalielewa vizuri swalii lake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, unaweza kurudia tafadhali.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, swali ninalouliza ni kwamba, vijana wengi kwa sasa hivi huja kwetu sisi Waheshimiwa Wabunge na kuomba kwamba wajiunge na JKT kwa sababu ya manufaa ambayo yanatokana na vijana waliojiunga. Je, Serikali ipo tayari sasa kuanzisha vituo vya JKT kila Wilaya ili vijana wetu wapate fursa ya kujiunga nalo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vituo vya JKT vilivyopo au vilivyokuwepo ambavyo vinatarajia kukarabatiwa gharama yake ni shilingi bilioni 7.6. Kuanzisha vituo vingine kwa sasa hivi ni gharama.

Na. 54

**Vikosi vya JWTZ Kujenga Barabara**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR ( k.n.y. MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Jeshi la Wananchi Tanzania limekuwa likitoa changamoto kubwa kwa Serikali katika ujenzi wa nyumba.

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kukipa nguvu kikosi cha *Field Engineer* ili nao waweze kutoa mchango wao katika ujenzi wa barabara zetu?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ulinzi wa Taifa Na.24 ya mwaka 1966 imeeleza kuwa jukumu kubwa la Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni Ulinzi wa Taifa yaani kulinda nchi na mipaka yake na kutoa mafunzo ya ulinzi kwa wananchi. Aidha, Jeshi pia limepewa jukumu la kutoa misaada ya dharura kwa kushirikiana na mamlaka zingine za kiraia zinazohusika wakati wa dharura na maafa yanapotokea. Kikosi cha Uhandisi Medani huhusika wakati wa kutoa misaada wakati wa dharura na maafa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, napenda kujiwu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Moja ya majukumu ya Kikosi cha Uhandisi Medani (*Field Engineer Regiment*) ni kufungua barabara wakati wa vita, ili kuwezesha kupitisha askari, zana, mitambo na huduma mbalimbali kuweza kufika katika sehemu nyingine. Vile vile, kikosi hiki hutumika wakati wa maafa yanapotokea kwa kutengeneza na kukarabati miundombinu kwa njia ya dharura ili kuwezesha huduma mbalimbali kuendelea na kuwafikia waathirika.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba upo umuhimu wa kikosi hiki kukipitia vifaa mbalimbali vya ujenzi wa barabara, lakini utumiaji wa vifaa hivyo uwe kwa malengo yale yale yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria ya Ulinzi. Hata hivyo, Wizara yangu itaendelea kukiimarisha kikosi hiki kivifaa kila hali ya fedha itakaporuhusu. (*Makofii*)

Na. 55

**Barabara ya Njia Panda - Qanded - Matala Kupewa  
Hadhi ya Kuwa Barabara ya Mkoa**

**MHE. GRACE S. KIWELU (k.n.y. MHE. DR. WILBROD P. SLAA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa Bodi ya Barabara Mkoa (*Road Board*) ilikwisha kuwasilisha maombi ili barabara ya Njia Panda- Qanded hadi Matala ipandishwe daraja na kuwa barabara ya Mkoa (*Regional Road*); na kwa kuwa Serikali katika majibu yake Bungeni mara kadhaa imesema itawasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ili kuruhusu kupandisha hadhi barabara kadhaa nchini ikiwemo na barabara iliyotajwa:-

(a) Je, ni lini sasa Serikali itawasilisha Muswada Bungeni ili lengo hilo la kupandisha hadhi barabara zilizoombewa ikiwemo na ile ya Njia Panda - Qanded hadi Matala na barabara ya Kibaoni (Manyara) hadi Slathano - *Upper Kitete* - Lositete – Selela Wilayani Karatu?

(b) Kwa kuwa barabara ya Njia Panda - Qanded - Matala kwa sasa iko kwenye hali mbaya sana, na huenda ikawa mbaya zaidi baada ya mvua; na kwa kuwa Serikali Kuu tayari imegharamia ujenzi wa daraja la Baray katika barabara hiyo. Je, isingekuwa wakati muafaka kwa Serikali Kuu kuptitia *TANROADS* kukarabati barabara ya Njia Panda - Matala ili fedha nyingi zilizotumika kukarabati daraja la Baray zitumike vizuri na kikamilifu kwa barabara hiyo kutumika wakati wote wa mwaka?

(c) Kama Serikali imekubali, je, kazi hiyo itaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwanza napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea na maandalizi ya Sheria Mpya ya Barabara yaani *Roads Act*. Hatua ya maandalizi iliyofikiwa kwa sasa ni kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, maandalizi ya rasimu ya sheria mpya ya barabara yamekamilika.

(ii) Kazi ya kutayarisha *schedules* za sheria hiyo inaendelea ambapo kundi la kwanza linahusisha barabara kuu na barabara za mikoa zenyetumile jumla ya urefu wa kilometra 35,000 ambazo zinasimamiwa na Wizara ya Miundombinu. Kazi iliyofanyika hivi sasa ni kuhakiki majina na urefu wa barabara hizi, kazi ambayo inatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Kundi la pili linahusu barabara zinazosimamiwa na TAMISEMI zenyetumile urefu wa karibu kilometra 50,000. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2006 .

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Njia Panda - Karatu - Mang'ola hadi Mataala ipo katika mtandao wa barabara zinazohudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu. Aidha, Wizara yangu iliichangia Halmashauri hiyo kwa kujenga daraja la Baray na hivyo Halmashauri ya Wilaya inashauriwa na inapaswa kutenga fedha za kutosha kwa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuanza kwa kazi za matengenezo ya barabara hiyo kutategemea mipango ya Halmashauri ya Wilaya husika hadi hapo Serikali itakapofikia uamuzi kama itakuwa ya Mkoa au la.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba sheria imekamilika.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini itakuja ndani ya Bunge ili iweze kuitishwa?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali imekarabati na kujenga daraja katika korongo la Baray ni kwa nini basi pesa hizo hizo zisitumike kukarabati barabara hiyo ili daraja hilo liweze kuitika wakati wote?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, la kwanza kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi nimesema kwamba rasimu imekamilika na sasa hivi tunatayarisha *schedules* za barabara, urefu na majina ya barabara hizo na nimesema kwa upande wa barabara

zinazohudumiwa na Wizara yaani barabara kuu na zile za Mikoa *schedules* hizo zinakamilika mwisho wa mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, lakini zile zinazohudumiwa na Halmashauri za Wilaya zitakamilika mwishoni mwa mwezi Juni. Kwa hiyo, kwa mantiki hiyo, sheria hiyo itakuja Bungeni baada ya mwezi Juni.

Lakini kuhusu suala la Wizara kutengeneza daraja la Baray ni kwamba huo ulikuwa ni msaada pale ambapo uwezo upo na kuna matatizo maalum Wizara husaidia mara chache barabara au madaraja yanayoshughulikiwa na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, lakini haina maana kwamba kwa kutoa msaada huo wa kujenga daraja, basi Wizara imeshachukua barabara ambayo inahusika na Wilaya.

Kwa hiyo, Wilaya zinashauriwa mpaka hapo tutakapokuwa tumeainisha upya na kutenganisha upya barabara zipi ziwe za Wizara na zipi ziwe za Halmashauri ziendelee kuhudumia barabara zake kama ilivyo kwa sasa.

Na. 56

Ujenzi wa Barabara ya Magu – Mwabuki

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara inayotoka Magu, Bukwimba, Ngudu, Jojiro hadi Mwabuki ina hali mbaya sana; na kwa kuwa barabara hiyo inaungana na barabara ya lami kwa upande wa Magu (Mwanza - Musoma) na pia inaungana na barabara ya lami upande wa Mwabuki (Mwanza - Shinyanga):-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kupunguza msongamano wa magari kupitia Mwanza hasa kwa magari yaendayo Shinyanga au Musoma?

(b) Je, Serikali inajua kuwa endapo barabara hiyo itatengenezwa kwa kiwango cha lami, uchumi wa Mji wa Ngudu utapanda?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Barabara ya Magu - Ngudu - Jojiro hadi Mwabuki yenyeye urefu wa kilometra 70 ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Mwanza. Hali ya barabara hiyo kwa sasa si ya kuridhisha sana kutohana na maeneo mengi kutokuwa na changarawe. Hata hivyo, barabara hiyo

inapitika vizuri wakati wa kiangazi, isipokuwa ina maeneo machache yanayopitika kwa taabu wakati wa myua.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na uwezo mdogo kifedha, Serikali haina mpango wa kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami hivi sasa. Hata hivyo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa barabara hiyo itafanyiwa matengenezo kwa kiwango cha changarawe chini ya Mradi uitwao *Performance Maintenance and Management of Roads*. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia pamoja na fedha za ndani ambapo Mkandarasi atakabidhiwa barabara na kuwajibika kuifanyia matengenezo kwa kipindi cha miaka mitano.

Aidha, ili kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Mwanza, Wizara yangu imepanga kujenga kwa kiwango cha lami barabara kuu ya Usagara - Kisesa yenyeye urefu wa kilometra 17 ili kuhakikisha magari yanayokwenda na kutoka Musoma na Shinyanga hayapiti katikati ya Jiji la Mwanza hivyo kupunguza msongamano katika Jiji hilo. Zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hiyo tayari zimekamilika na zitatangazwa mwezi huu wapili.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye sehemu (a), barabara hiyo itafanyiwa matengezezo kwa kiwango cha changarawe ambapo itapitika vizuri wakati wote na hivyo kuendeleza uchumi wa eneo hilo kwa uhakika angalau kwa miaka mitano ijayo.

**MHE. RISHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, amesema kwamba barabara hiyo itawekewa changarawe, ni lini barabara hiyo itawekewa chagarawe?

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa barabara iliyotajwa katika swali la msingi inafungua Wilaya ya Magu, Maswa na Kwindu, Serikali haioni sasa ikaweka hata fungu dogo la dharura ili tuhakikishe kwamba tumefungua njia ya kuhakikisha kwamba Wilaya hizi zinafaidika na fedha zake kuliko kusubilia Bajeti ya mwaka 2006/2007?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka huu tumeipitisha tayari na mipango ambayo ipo kwenye Bajeti wote Wabunge tulishiriki katika kuiangalia. Kwa kazi ambazo hazikuweza kutengewa Bajeti kwa mwaka huu, zitawekwa kwenye Bajeti inayofuata. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo nia na ndiyo maana imekuwa ikitenga Bajeti ili kuweza kuunganisha Wilaya hizi tatu ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja. Kwa hiyo, awe na subira na hizi kazi zitafanyika kwa mujibu wa ratiba iliyowekwa kwenye utekelezaji.

Na. 57

### **Vifaa Vya Ujenzi Wa Vyumba Vya Madarasa**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Kondoa Kusini kwa juhudi zao wamejenga vyumba vya madarasa themanini lakini wameshindwa kukamilisha ujenzi huo kutokana na uwezo mdogo wa kupata vifaa kama Mabati, Saruji na Mbao.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kusaidia upatikanaji wa vifaa hivyo ili majengo hayo yasiendelee kuharibika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Pascal Degera, kwa kuchaguliwa tena na wananchi wa Kondoa Kusini, aendelee kuwa Mbunge wa Jimbo la Kondoa Kusini na pia nampongeza kwa jubudi zake za kufuatilia masuala ya elimu katika Jimbo lake na Wilaya yake ya Kondoa. Aidha, nawapongeza wananchi wa Jimbo la Kondoa Kusini kwa juhudi ambazo wamefanya za kujenga vyumba vya madarasa themanini kwa ajili ya Sekondari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na mgawo wa Kitaifa wa fedha za *MMES* zilizopatikana. Mkoa wa Dodoma ulipata fedha za ruzuku ya maendeleo kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 64 kati ya 97 ambavyo Mkoa ulikuwa umepangiwa.

Vyumba 28 katika shule za zamani na vya madarasa 36 katika shuke mpya. Pia Mkoa ulipata ruzuku ya kukamilisha ujenzi wa nyumba 37 za walimu kati ya nyumba 38 walizopangiwa. Nyumba 28 katika shule za zamani na nyumba 9 kwa shule mpya. Kati ya vyumba vya madarasa 64 na nyumba za walimu 37 walizopewa Mkoa wa Dodoma, Kondoa ilipata vyumba vya madarasa 28. Madarasa 12 kwa shule za zamani na 16 kwa shule mpya. Nyumba nane za walimu, sita kwa shule za zamani na nyumba mbili kwa shule mpya.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii basi kushauri Halmashauri na wananchi kuendelea kukamilisha majengo yaliyojengwa wakati Serikali inafanya juhudzi za ziada kupata fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoka kwa wahisani ili kusaidia nguvu za wananchi katika Wilaya ya Kondoa na nchi nzima kwa ujumla. Wizara itazigawa fedha zitakazopatikana nchi nzima kwa uwiano sahihi kwa kila Wilaya kwa lengo la kuongeza idadi ya wahitimu wa Darasa la Saba kuingia shule za Sekondari. Ni matarajio yetu kuwa fedha zitakazopatikana Wilaya ya Kondoa itapata fedha za kununulia vifaa kwa ajili ya kuendelea kukamilisha majengo yake.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika mgao wa madarasa ama vyumba vya madarasa kuititia mradi wa *MMES*, Wilaya ya Kondoa ilipatiwa vyumba 54; na kwa kuwa Naibu Waziri katika majibu yake amekiri kwamba Wizara imetoe fedha kwa ajili ya vyumba 28 tu. Je, vyumba 26 vilivyobaki fedha zake zitatolewa lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, Wizara tukipata fedha, fedha hizo ziweze kugawiwa sawa kwa nchi nzima. Mpaka sasa hatujapata fedha za wahisani ili kuweza kukamilisha miradi hiyo. Hivyo tunamwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine kutoka Majimbo mengine waweze kuwa na subira hadi fedha za *MMES* zitakapopatikana ndipo tuweze kuzituma haraka katika Wilaya zote nchini.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alituambia kwamba tuwe na subira na kuna Wilaya mpya zilizogawanywa mwishoni mwa mwaka jana. Je, Wilaya hizo mpya zitakuwa katika utaratibu huo wa kugawiwa hizo fedha kuliko kuwekwa kwenye zile Wilaya za zamani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, Wilaya sita zilizotamkwa zianzishwe tunaelewa kabisa Wilaya hizi zimo katika Wilaya zile za awali ambapo shughuli zake bado zinaendelea kushughulikiwa kama kawaida. Lakini kwa sababu uwanzishwaji wa Wilaya hizi utatenga pia pesa kwa ajali wa ujenzi wa shule zao za sekondari.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge wala asiwe na wasi wasi fedha za *MMES* zitakapopatikana Wilaya hata hizi mpya zitapewa fedha kama kawaida. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi waliupokea mpango wa *MMES* kwa matumaini kwamba pale ambapo wanajenga shule za sekondari za Kata, mpango wa *MMES* au Serikali itawasaidia wananchi kumalizia hasa baada ya kufika kiwango cha *linter* lakini hadi sasa Kata nydingi ambazo zimefikia kiwango hicho hazijapata msaada wowote wa Serikali. Kuna tatizo gani mpango huo usitekelezwe wa kuwasaidia wananchi pale ambapo wameonyesha jitihada za kujenga mpaka kufikia hatua hiyo ya *linter*?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mpango wa *MMES* umeahidi kusaidia shule zitakazojengwa kila Kata lakini nataka nitoe taarifa pamoja na kwamba tunaegemea kupata bilioni 61.7 ambazo zitapatikana kuanzia mwezi Machi bado tunategemea kwa kiwango kikubwa nguvu za wananchi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba nilikuwa nafululiza maswali ya nyongeza kwenye Wizara hii lengo langu lilikuwa ni kwamba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı aweze kujibu kwa mara ya kwanza. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 58

### **Huduma ya Maji ya Bomba**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kata ya Ndungu ina mradi wa umwagiliaji ambao umeanzishwa mwaka 1990 kwa ajili ya kilimo cha mpunga, na kwa kuwa maji hayo yanapotumika kwenye mashamba ya mpunga mengine yanapita na kuingia kwenye bwawa la Kalemawe; na kwa kuwa bwawa hilo nalo ni chanzo cha mirefeji mikubwa miwili inayotumika kwa kilimo na matumizi ya nyumbani kama vile kupika na kunywa kwa wananchi wa Vijiji vya Kalemawe, Karamba na Mgandu; na kwa kuwa, maji hayo yanakuwa yamechanganyika na mbolea na dawa zinazotumika kwenye mashamba ya mpunga na hiyvo kutokuwa salama kwa matumizi ya binadamu.

Je, Serikali haioni kwamba ni vyema ikachukua hatua ya dharura kabisa ya kuwapelekea wananchi hao huduma ya visima virefu vya kudumu wakati ikijitayarisha

kuwapatia maji ya bomba ili kuwaepusha na madhara makubwa ya magonjwa mengi yanayotokana na mchanganyiko wa dawa na mbolea kwenye maji wanayotumia.

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Same Mashariki kama ifuatavyo:-

Bwawa la Kalemela lilijengwa mwaka 1959 kwa madhumuni makubwa ya kuzuia mafuriko, umwagiliaji wa mashamba wakati wa kiangazi na uzalishaji wa samaki. Kutokana na ongezeko la watu maji ya bwawa hilo kwa sasa yanatumika kwa matumizi ya nyumbani pia.

Mheshimiwa Spika, uchafuzi wa bwawa la Kalemawe ni mojawapo ya mifano ya uchafuzi wa vyanzo vingi vya maji hapa nchini, unaotokana na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za binadamu kama vile kilimo, ujenzi wa nyumba, viwanda vidogo na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu madhara ya muda mrefu yanayosababishwa na shughuli zao. Hivyo maji ya bwawa hilo si salama kwa matumizi ya nyumbani ukizingatia utunzaji na namna maji yanavyokusanywa kutoka maeneo mbalimbali yenye makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mikoa na Wilaya tutaanza kutekeleza programu ya majisafi na usafi wa mazingira kuanza Julai, 2006. Katika programu hiyo Wilaya ndiyo itakuwa na jukumu la kuchagua miradi yake, kupanga na kutekeleza miradi hiyo ya maji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kukubaliana na ushauri wake Mheshimiwa Mbunge wa kuchimba visima virefu vya kudumu, ili kuwapatia huduma ya maji safi na salama wananchi wa vijiji hivyo. Aidha, ili kutekeleza ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na pia kuwanusuru wananchi wa maeneo hayo kutotumia maji yasiyosalama, napenda kuchukua fursa hii kushauri haya yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Same ione umuhimu wa kutekeleza mradi wa dharura wa visima katika maeneo aliyyoyataja Mheshimiwa Mbunge ili kuwaondolea wananchi kero ya ukosefu wa maji safi na salama.

(ii) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya itoe kipaumbele kwa vijiji vya Kalemawe, Karamba na Mgandu kwa kuviingiza vijiji hivyo katika Programu ya Majisafi na Usafi wa Mazingira itakayoanza Julai, 2006 ambapo huko ndiko fedha za kuchimbia visima virefu vya kudumu zitapatikana. (*Makofi*)

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu swali vizuri na nina uhakika hata wananchi wamefurahi. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, maswali yetu hapa Bungeni sisi Waheshimiwa Wabunge yanajibiwa na wataalam. Kwa hivyo, mara kwa mara wataalam hawa ni kweli wanakuwa wamefika kwenye maeneo lakini wao hawaguswi sana na madhara ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne hategemei sana wataalam, anatoka ofisini anakwenda kuona kero za wananchi yeye mwenyewe. Waziri wa Maji na Naibu Waziri na ninyi hamuoni udharura wa kwenda kwenye Kata ya Ndungu mkaona hii hali ya wananchi ilivyo mbaya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa ni Waziri wa Maji kwa muda mrefu na anaelewa hili tatizo la maji katika nchi yetu kwamba sasa sio kero tena, inakuwa ni aibu kidogo kwa Taifa.

Je, Serikali ya Awamu ya Nne inakuja na mkakati gani mzito wa kuondoa hili tatizo la maji kwa Taifa zima, haswa ikijua kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo tulikpokuwa tunaomba kura za Rais na kura zetu wenyewe tuliahidi wananchi kwamba ifikapo mwaka 2010 kwa kutumia Ilani ya Uchaguzi ya CCM maji salama yatapatikana mijini kwa asilimia 90 na kwa vijijini ni kwa asilimia 65? Naomba kujibiwa swali hili (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nakubaliana naye kwamba Rais anatembelea maeneo yeye mwenyewe bila kukaa ofisini. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Mawaziri vile vile watafuata nyayo za Rais kwenda katika maeneo aliyoyataja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, nakubali tatizo la maji ni kubwa nchini. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ilielekeza kwamba kipaumbele kikubwa katika miaka hii mitano ni kuhakikisha kwamba watu wengi zaidi wanapatiwa maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutatekeleza kwa nguvu zetu zote kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, ninayo matangazo tu sasa. La kwanza, kumekuwa na mvutano wa chini chini hapa kuhusu hali ya joto na baridi ndani ya ukumbi huu. Waheshimiwa Wabunge wanawake wakidai ukumbi huu una baridi kali na Waheshimiwa Wabunge wanaume wakidai kwamba kuna joto. Sasa wataalam wamerekebisha na tunahisi hali ya leo ndiyo hali ambayo inawajibu makundi yote mawili. Kwa hiyo, wale waliokuwa wanadhani ni joto au baridi, wasidhani kwamba mitambo imeharibika, hii ndiyo hali itakavyokuwa ili wote tuweze kukaa vizuri kuamua mambo ya wananchi wetu. (*Makofi/Kicheko*)

Tangazo la mikutano, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wanaombwa wakutane mara baada ya kipindi hiki cha Maswali na Majibu, kuzingatia Muswada wa Taratibu za Mazishi ya Viongozi. Hakikutamkwa chumba hapa, lakini nadhani wataelekezwa hapo.

Pili, Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti ameomba akutane na Wajumbe saa tano asubuhi hii ni chumba namba 231. Tatu, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii wakutane saa tano katika chumba namba 219 asubuhi hii.

Nne, Kamati ya Huduma za Jamii wakutane saa tano chumba namba 133. Tano, Kamati ya Kilimo na Ushirika wakutane chumba namba 227 nao saa tano. Mwisho, Waheshimiwa Wabunge wanawake wote mnaombwa baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana, mbaki humu ndani. Kuna mkutano mfupi tu wa kuelezana mambo muhimu sana. Katibu Tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Hoja ya Kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Bungeni Tarehe 30 Desemba, 2005**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu, naomba kuchukua nafasi hii kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kupata ushindi wa kihistoria, lakini pia kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. Vile vile nachukua nafasi hii kuwapongeza Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu Mawaziri wote, hali kadhalika wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika. *(Makofi)*

Baada ya hapo ningependa pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu ambao ni wanawake wa Mkoa wa Pwani na wanawake wa CCM kwa ujumla kwa kunipa nafasi kwa kipindi kingine cha tatu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natanguliza kuunga mkono hoja ya hotuba ya Rais mia kwa mia. Katika hotuba hiyo Mheshimiwa Rais namshukuru zaidi wakati alipoongelea suala la wavuvi. Tunajua kwamba muda mwangi tulikuwa tukilalamikia suala zima la wavuvi. Katika kipindi hiki tumefurahi kuona kwamba katika ukurasa wa 31 wa hotuba yake amegusa kabisa kwa uwazi kwamba Serikali itawawezesha wavuvi wengi iwezekanavyo kupata zana bora. Hili kwa kweli limetufurahisha wengi ambao tumezungukwa na Bahari, Maziwa pamoja na Mito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ningeomba pamoja na kuwapa wavuvi zana bora ili waweze kuvua zaidi na kuweza kupata mazao ambayo wangeweza kuuza na kupata

tija nzuri, ningeomba ili tusirudie kufanya makosa ambayo sasa hivi tunayarekebisha kwa kuhakikisha kwamba mazao yetu hatuyauzi kama yalivyo ila tunayaboresha kwa kufungua viwanda vya kuweza kukoboa korosho, kutengeneza sigara, kutengeneza sukari. Basi ningeomba hili wazo la kuwapa wavuvi zana bora liendane sambamba na kuwashawishi wawekezaji kujenga viwanda vya samaki hususan samaki wa baharini.

Mheshimiwa Spika, tunajua sasa hivi kuna viwanda ambavyo vinasindika samaki, lakini vinapeleka minofu ikiwa mibichi. Sasa mimi nakumbuka katika uhai wangu niliwhi kuona samaki wa makopo wakitoka China na wakitoka nchi nyingine za nje ambao wameshatengenezwa tayari kwa kula. Sasa ningeomba, kipindi hiki basi na sisi tujielekeze kwenye kutengeneza samaki wakiwa tayari kwa kula. Najua Mafia tunao samaki wazuri sana wa *size* zote, wa makabila yote. Sasa tukiishia tu kwenye kuvua na kuanika, maana ndiyo njia kuu tunayoitumia, kwa kweli haitatufikisha mbali. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie pia na kuwashawishi wawekezaji wakubwa na wadogo ili waweze kuja kufungua viwanda maeneo ambayo wavuvi wetu watakuwa wanavua samaki kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ningeomba kuunganisha na hivyo hivyo viwanda. Sasa hivi vijana wengi na wanawake wanafanya miradi, lakini miradi mingi ni miradi midogo midogo na wanajielekeza zaidi kwenye miradi ya biashara, kukaanga samaki, kufanya biashara za kuuza nguo na kufanya biashara za kukoboa korosho.

Sasa mimi ningeomba hizi Wizara za Biashara na Viwanda liwape nafasi kubwa zaidi wenzetu wa *SIDO* kuweza kuwahamasisha na kuwaelimisha vijana na wanawake katika kuachana na biashara hizi ambazo haziwapi tija ya kutosha, waingie kwenye viwanda vya kati na viwanda vidogo vidogo. Najua malighafi tunazo kila upande. Kila upande wa Tanzania kuna malighafi ambazo tunaweza tukazitumia kuziboresha kupitia kwenye viwanda vya kati na viwanda vidogo, tukaweza kupata hali zetu za kiuchumi kuinuka zaidi na kwa haraka kuliko hivi sasa. Nitachukua mfano wa Mafia, Mafia tuna zao la Mnazi. Zao la Mnazi ninavyofahamu kuanzia kuti, ukiondoa mizizi sijasikia matumizi yake, yote ni malighafi ambayo inaweza ikatumika kwa kupitia viwanda kuweza kutoa bidhaa ambazo tunaweza tukasafirisha nje na kuuza ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukatengeneza kamba, tunaweza tukatengeneza mafagio, tunaweza tukatengeneza *ma-brush*, hali kadhalika tunaweza tukatengeneza *furniture* za mbao za mnazi. Kwangu mimi Mafia nikiangalia Minazi, ipo minazi ambayo iko tayari kutengenewa mbao lakini inaoza, yapo makuti ambayo yangeweza kutengenezwa mafagio lakini yanaoza, yapo makumbi ambayo tunaweza tukatengeneza vitu vingi sana, lakini tunayachoma moto. (*Makofi*)

Sasa mimi narudia tena kuomba sana Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Ninamshukuru Mheshimiwa Basil Mramba wakati akiwepo katika *SIDO* aliwhi kujaribu kutuletea Kiwanda cha Mazulia cha *Doormats* pamoja na kamba. Lakini baadae wenzetu wa *SIDO* hawakuweza kutekeleza kuimalisha zaidi viwanda hivi Mafia na kuwapeleka wengi zaidi katika kujifunza jinsi ya kutumia mazao ya mnazi. Hilo ni mfano ambao uko

hai mimi ninaufahamu. Lakini nina ukakika hata kwa Mikoa mingine na Wilaya nyingine tunayo mazao mengi tu ambayo tungeweza tukayaboresha kuitia viwanda vya kati na vidogo vidogo kwa kuwatumia akinamama na vijana na wao wakawenza kunufaika na vile vilivywazunguka na hatimaye Serikali yetu ikaongeza Pato la Taifa na sisi kufaidika na huduma zinatolewa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba niongelee suala la UKIMWI. Naishukuru Serikali kwa kuleta dawa. Lakini naomba sana wenzetu wanaoshughulika na UKIMWI waende mbali zaidi kuangalia wagonjwa wa UKIMWI. Baada ya dawa mahitaji mengine ni nini. Mimi nafahamu ni chakula. Baadhi ya wagonjwa hawa wanakuwa, wanapofuka kwa dawa ambazo wanapewa bila kupata lishe ya kutosha. Tunajua kwamba si rahisi kuwalisha wagonjwa wote, lakini wapo ambao wanajidhihirisha wazi kwenye *Clinic* zao wanazokwenda kwamba hawana uwezo wa kupata lishe bora. Sasa tufanye utaratibu wa kuwatumia wafadhili wetu, *NGOs* zetu kuweza kuwapitia na kuwafuatilia hawa wagonjwa kama kweli baada ya kula dawa wanapata na chakula husika cha kuweza kuongeza maisha yao! Au wengine ndiyo wanapofuka na kufa haraka kwa kutokuweza kupata chakula cha kuendana na dawa hizo!

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache na kwa kuwa kengele ya kwanza imeishalia, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nitoe shukrani kwa vile ni mikutano wa kwanza wa Bunge letu, kumtolea shukrani Mungu kwa kunifanya leo niwe Mbunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Lakini pili, napenda nitoe shukrani kwa wanajimbo wa Mbinga Magharibi ambao wao kwa upeo wao wanavyofikiri waliniruhusu mimi kuzunguka nchi nzima kukampeni kwa ajili ya Chama cha Mapinduzi, Wabunge na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru sana kwa vile walinipa siku 13 tu za kukampeni katika jimbo hilo, lakini siku nyingine zote waliniruhusu niende huko nchi nzima nisaidie Chama changu cha Mpinduzi kushinda. Lakini wanajimbo hawa walitoa sharti moja tu, ikiwa Mawaziri watapatikana kutoka CCM basi waende kule Mbinga Magharibi kwenda kusaidia kutatua matatizo sugu ambayo yanawakabili wao kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kupata kura nyingi na za kishindo na kuwazidi wenzake wote ambao hata *ten percent* ya ushindi wake hawakuufikia. Nimpongeze pia Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume na Chama cha Mapinduzi Zanzibar kwa kukata miguu ya *CUF* kule. Zamani ilikuwa baada ya uchaguzi *CUF* walikuwa wanafanya mikutano mingi, lakini baada ya uchaguzi huu sijawahi kuona *CUF* wanafanya mikutano tena maana nadhani sasa wamekwisha. Lakini nitakuwa mpungufu wa fadhila ikiwa sitampongeza hapa Mama Salma Kikwete. Ni mama ambaye ni *courageous* na wengi wetu hapa ametusaidia sana kuongeza ushindi katika Majimbo yetu pamoja na mimi. Lakini pia niwapongeze Mawaziri, Naibu Mawaziri, wewe

mwenyewe Mheshimiwa Spika, Naibu wako na Wabunge wote ambao wamepitia katika tanuri la kushinda kwa kishindo kupitia Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Hotuba yenyewe ya Rais inaonyesha matumaini ya hali ya juu sana kwa Watanzania na hata majirani zetu Waganda na Wakenya. Jana kuna rafiki yangu mmoja alinitembelea hapa Dodoma, alinieleza kuwa kama Rais Kikwete atafanya ziara kwenda Kenya ni jinsi gani wananchi wanavyomsubiri kwa hamu kubwa Kenya na Serikali ya Kenya inavyoijiandaa kumpokea Rais huyu kijana. Lakini yeye alikwenda mbali zaidi akasema sasa tumepeata Rais wa kwanza wa Afrika Mashariki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa katika hotuba hiyo, mimi mchango wangu mkubwa uko kwenye chakula. Nchi yetu imegubikwa na njaa, lakini nimuunge mkono Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela kwamba kwa kiasi fulani njaa hii tumejitakia wenyewe, kwa sababu Tanzania ni kubwa na yako maeneo na mikoa ambayo kila wakati mvua inanyesha. Mkoa kama wa Ruvuma, Mbeya, Iringa, Rukwa ni mikoa ambayo kila wakati kila mwaka kunakuwa na mvua nyingi za masika na za vuli. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba sehemu hizo hakuna njaa, hakuna ajabu mvua kuonyesha Mikoa hiyo. Pengine kuna ajabu mvua kuonyesha Dodoma, kuna ajabu kuonyesha mvua Singida na maeneo kama hayo. Lakini si ajabu kwa Ruvuma hasa kwa Wilaya ya Mbinga kunyesha mvua. Sasa baada ya kupata njaa hii Serikali imejitahidi sana kuagiza chakula kutoka nje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini nguvu hii hii ambayo Serikali imejitahidi kuagiza chakula kutoka nje, kama ingetumika kuandaa utaratibu na mipango ya kutafuta chakula kwenye mikoa hii, nafikiri hata fedha za nje zisingetumika nyingi zaidi kwa sababu tuna ardhi yetu wenyewe, tuna wataalam wetu wenyewe, tuna mvua zetu wenyewe. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri, sasa tumechelewa, lakini ni vizuri kuweka mipango kuanzia mwakani, Serikali kwenda kuangalia, wataalam kwenda kuangalia mikoa hiyo ni maeneo gani ya vijiji wanayatumia kwa ajili ya kilimo na maeneo gani ambayo yanafaa kwa kilimo lakini hayatumiki ili tuzalishe mazao kwa wingi na tuondokane na aibu ya kuagiza chakula kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni elimu ya Sekondari. Tumeambiwa hapa na Waziri Mkuu kwamba wanafunzi ni wengi ambao wameshindwa *ku-join* na elimu ya sekondari kutoka shule ya msingi. Serikali ya Tanzania imeruhusu hata Mashirika ya watu binafsi na watu binafsi wenyewe kuanzisha sekondari na shule za msingi na wale wanaotoka shule za msingi mara nyingi huenda shule za sekondari ikiwa umefaulu bila kujali alikuwa shule ya msingi ya binafsi ama ya Serikali.

Kwa kipindi hiki ambacho wanafunzi wa *primary school* kwenda *secondary school* hawajapata *secondary school* kwa sababu ya nafasi, nashauri Serikali iangalie utaratibu wa kuwaomba wenyе shule binafsi ambao wana nafasi kwenye shule zao waruhusu hawa wanafunzi ambao wanaelea nje wawafundishe kwenye shule zao mpaka hapo Serikali itakapojenga uwezo wa kuongeza shule. Ziko shule za sekondari za binafsi ambazo zina nafasi ya kutosha, kwa hiyo, tukifanya utaratibu tunaweza kupata shule

ambazo zitatusaidia ili wanafunzi wetu hawa waliofaulu waende shule za Sekondari bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, suala la tano ni suala la Utamaduni. Ninashukuru Rais ameunda Wizara ya Utamaduni, Habari na Michezo. Upande wa Michezo, tayari kuna Uwanja wa kisasa ambao nchi yetu imeujenga na sasa ni *challenge* kubwa kwa wanamichezo wetu kutumia Uwanja ule. Lakini kwa upande wa Utamaduni kwa maana ya sanaa za maonyesho, utaratibu huu ni vizuri Wizara ikafikiria pia kuunda majumba ya Starehe ambayo watu kutoka nje, Watanzania wenyewe wanaweza kwenda kwenye maeneo yale na wakaona starehe hizo. Lakini leo akija mgeni au vikundi vyetu, akitaka kuona sanaa za maonyesho anakwenda kwenye *ma-bar* kwenda kuona sanaa za maonyesho. Lakini ni vizuri Serikali ikaunda majumba ya burudani ya starehe ili watu wakaone sanaa badala ya kuona pombe.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaomba Wizara ya Utamaduni iwafuatilie wasanii hasa katika upande wa haki miliki na haki shiriki. Wasanii hawaelewi jambo hilo. Wanafikiri wakasharekodi, ndiyo mwisho. Akipeleka Redio Tanzania, akipeleka *Radio One*, akipeleka kwenye kituo chochote kile cha kurushia matangazo ya *Television*, anafikiri huo ndio utamaduni, hiyo ndiyo uchumi.

Kwa hiyo, nafikiri Serikali iwaelimishe wasanii haki zao za msingi ni zipi, haki za kufanya biashara ni zipi ili wasanii wafaidike na jasho lao. Kwa haya machache naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, jina langu ni William Jonathan Kusila, siyo Jonathan Kusila, kama linavyoonekana kwenye orodha yako, naomba lisahihishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hotuba hii ya Rais. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuliongoza Taifa letu.

Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo. Nikupongeze pia wewe Spika na Naibu wako kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuliongoza Bunge hili. Naomba vile vile niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kushika nyadhifa zao mbalimbali na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuchaguliwa katika Majimbo yao na kupitia Viti Maalum kuingia katika nyumba hii. Mwisho nimalizie shukrani hizi kwa kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Bahi kwa kunichagua kwa mara ya nne mfululizo kuwatumikia katika Jimbo hili. Ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama kuchangia hoja hii katika eneo moja tu, eneo la njaa. Tatizo la njaa ni kubwa sana katika Taifa letu hivi sasa, nadhani hili halihitaji msisitizo zaidi, linaleweka na ni tatizo la nchi nzima. Ninachotaka kusisitiza au kuongelea kuhusiana na tatizo hili ni kusisitiza umuhimu wa upatikanaji wa chakula katika soko na katika hali kama hii. Nataka kwanza niishukuru sana Serikali na hasa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kauli zake za kuwafariji

sana wananchi na kuwapa matumaini na hatua mbalimbali ambazo zinachukuliwa na Serikali yetu katika kupambana na tatizo hili. Mimi ninawapongeza na kuwashukuru sana, zinatia moyo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala la upatikanaji wa chakula katika soko katika hali kama hii ni suala nyeti na ni muhimu sana kwa sababu mbili, kwanza kabisa kudhibiti upandaji holela wa bei ya chakula katika hali kama hii. Kwa sababu waswahili wanasema, hakuna shari isiyo na heri. Mara wanasema, kufa kufaana. Kwa hiyo, katika hali hii lazima watajitokeza watu ambao wanataka kunufaika kutokana na janga hili ambalo Watanzania wanalo na haitakuwa rahisi kudhibiti bei kama chakula sokoni upatikanaji wake utakuwa tatizo. Lakini vile vile upatikanaji wa chakula katika soko utasaidia sana kupunguza hofu kwa Watanzania kuhusiana na janga hili. Sasa hali ilivyo hivi sasa kwa kweli upatikanaji wa chakula katika soko umekuwa ni wa wasi wasi. Juzi juzi hapa Mheshimiwa Rais amekwenda bila taarifa kwenye Soko Kuu la hapa katika Mkoa wa Dodoma la Kibaigwa na amejionea mwenyewe. Pale ni mahali ambapo mahindi yalikuwa yanapatikana kwa wingi sana wakati wote mwaka mzima, lakini hali alioikuta juzi ilikuwa ni tofauti sana. Sasa hilo tu peke yake linaleta hofu kwa watu kwamba pengine hata hiki chakula tunachokizungumzia hapa nchini hakipo. Kwa hiyo, kupatikana kwa chakula kutasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi ni bei. Sasa moja ya sababu kuu ya kuwa na hifadhi ya Taifa ya chakula ni kuhakikisha kwamba wakati kama huu chakula hicho kinaingizwa katika soko ili kudhibiti upandaji holela wa bei. Hiyo ndiyo moja ya sababu kuu za kuwa na hifadhi ya chakula pamoja na kuhakikisha kwamba chakula chenyewe kinapatikana. Sasa namna ya hakika na ya pekee kabisa ambayo tunaweza kudhibiti upandaji holela wa bei ya chakula katika soko sasa hivi ni kuhakikisha Serikali inatoa chakula hicho kutoka kwenye hifadhi yake kuhakikisha kinaingia katika soko kwa bei itakayokuwa ya soko kwa hivi sasa ili kuzuia wafanyabiashara ambao wana mahindi yao binafsi wasipandishe bei ya chakula kiholela. Hivi sasa hivi ukienda kwa mfano kwenye masoko mengi, tembelea hata hili Soko Kuu la hapa Mjini Dodoma, huwezi kujua leo utauziwa mahindi kwa bei gani na kesho utauziwa kwa bei gani. Bei inapanda kila siku kwa sababu hakuna udhibiti.

Mheshimiwa Spika, katika hali hii hata kama tungeliweka polisi kila mahali kuhakikisha kwamba chakula hakipandi bei kiholela, haitawezekana isipokuwa tu kwa njia ya kuhakikisha kwamba kuna chakula ambacho bei yake inajulikana ambacho kitasaidia sana kudhibiti wafanyabiashara kupandisha bei ya chakula holela. Mheshimiwa Rais alitoa mfano hata juzi alipokuwa anatuhutubia kwamba mtu akitoa chakula sehemu moja anakipeleka umbali usiozidi hata kilometra moja, lakini chakula hicho kinapanda bei kwa mara mbili kwa kufanya hivyo tu, ukijaribu kufanya mahesabu na nini. Kwa kweli utakuta kwamba hakuna kinachohalalisha bei hiyo kupanda kiasi hicho. Mimi nasema kama Serikali haiwezi kutoa chakula na kuingiza chakula sokoni kwa bei itakayokuwa imeeleweka ili idhibiti upandaji holela wa bei, tutapata tatizo sana na mimi ninavyosema itaongeza hofu na vile vile hata tatizo lenyewe litazidi kuongezeka.

Kwa hiyo, ninachotaka kushauri ni kwamba pamoja na hatua zote nzuri ambazo Serikali inazichukua katika kuhakikisha kwamba chakula kinasambnaa na kinawafikia wananchi na kuwasaidia wale ambao hawana uwezo kabisa wa kununua chakula lakini hatua madhubuti kabisa zichukuliwe na Serikali ili kuhakikisha kwamba sehemu ya akiba ya chakula cha hifadhi ya taifa tulichonacho kinaingia katika soko kwa bei inayoeleweka ili kiweze kudhibiti upandaji holela wa bei ya chakula sokoni. Kwa vyovyote vile bado tutawahitaji wafanya biashara binafsi kuchangia katika jitihada hizi za kukabiliana na upungufu wa chakula nchini na watauza kwa bei zao watakazo, lakini itasaidia sana kama kutakuwepo na chakula ambacho kita-*check* huo upandaji holela wa bei za chakula.

Mheshimiwa Spika, hilo ndilo nilitaka nisisitize sana katika suala hili la njaa na hasa katika kukabiliana na hali hii katika kipindi tulichonacho hivi sasa na ukubwa wa tatizo lenyewe.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nalo nilitaka nisisitizie ni hili suala la ujambazi, nalo vile vile limeleta hofu kubwa sana katika Taifa na kama kuna hofu na kama wananchi wanajisikia kwamba hawako salama, basi hata ushiriki wao katika shughuli mbali mbali za maendeleo, ushiriki wao katika uzalishaji mali vile vile utaathirika. Sasa hivi kila mahali vijijini ujambazi unatokea watu wenye maduka magogo madogo wanaporwa, Mijini wanaporwa kwa hiyo, kila mtu anajiona siyo salama nyumbani kwake, anapotembea na hii itaathiri sana hata uzalishaji mali na hata tu ushiriki wa wananchi katika shughuli mbali mbali.

Kwa hiyo, hili lazima lipigwe vita kwa nguvu zote na naishukuru Serikali katika hili kwamba kauli zake na vitendo vyake inaonyesha dhahiri kwamba kuna nia na uamuvi wa kweli kabisa wa kukabiliana na tatitizo hili. Mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama nataka niihakikishie Serikali kwamba nitaungana nao nitashirikiana nao katika kuhakikisha kwamba tunalipiga vita suala hili kwa nguvu zote. Ni tishio kubwa na kwa kweli limejengea hofu kubwa sana lakini minaamini majambazi hawawezi kuishinda Serikali yetu nguvu na kwa hiyo lazima tuendelee kukabiliana nalo, tupambane nalo mpaka hapo tutakapohakikisha kwamba limetokomezwa kabisa. Mitando ya uhalifu lazima ieleteke ili tuweze kukabiliana nayo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, yangu yalikuwa ni hayo, nashukuru sana. (*Makofit*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima James Mdee. Namwomba radhi Mheshimiwa Ruth Msafiri, msemaji wa kwanza Mheshimiwa Margareth Mkanga amerejea ukumbini, wengi walidhani kipindi cha Maswali na Majibu kitaendelea hadi saa 4.30 asubuhi. Kwa hiyo, nitamruhusu Mheshimiwa Mkanga mara baada ya Mheshimiwa Mdee, halafu ndiyo Mheshimiwa Ruth Msafiri atafuatia. Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote napenda nitoe shukrani za dhati kwa Chama changu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo, kwa kunipa fursa ya kukiwakilisha Bungeni na ninaahidi kwamba nitakiwakilisha ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitakuwa ni mtovu wa nidhamu nisipotoa shukrani kwa Naibu Waziri wa Maji kwa kutumia Taasisi ya *Hans Seidel Foundation*, alitoa semina ya wanawake ambao wanataka kuwa viongozi na ni kwa kutumia mafunzo yake kwa namna moja ama nyingine alini-*encourage* kugombea hii nafasi na hatimaye nimepata. Natoa shukrani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda nitoe pongezi kwako wewe binafsi, natoa pongezi kwa Naibu Spika, nitoe pongezi kwa Waziri Mkuu, nitoe pongezi pia kwa Mawaziri wote pamoja na Wabunge wote wa Viti Maalum na Wabunge wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais, napenda nimpe pongezi kwamba pamoja na kujumuisha Ilani ya Chama cha Mapinduzi ameingiza pia na Ilani ya CHADEMA katika mpango wake wa kazi. Kwa hiyo, nampongeza sana ameonyesha Utanzania na tunasema milango iko wazi akitaka ushauri katika kukamilisha... (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nitoe pole. Pole kwa Watanzania wote ambao wako kwenye njaa. Ujumbe ni kwamba, tuko pamoja na Wabunge wapo pamoja na nao katika kuhakikisha mnapata mahitaji yenu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze rasmi kuchangia hoja. Mimi nita-*focus* katika maeneo mawili. Eneo la kwanza ni watumishi wa Serikali na eneo la pili ni elimu. Muda ukiniruhusu nitazungumzia kidogo takrima.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na watumishi wa Serikali, ni ukweli ulio wazi kwamba watumishi wa Serikali ni watumishi ambao wanaishi katika mazingira magumu sana na kama tusipofanya mikakati kuhakikisha kwamba maisha yao yanaboreshwa hii hotuba ya Rais ambayo tunaijadili hapa haitakuwa na maana, kwa sababu wao ndiyo watendaji wakubwa wa kuhakikisha kwamba huu mkakati unakamilika.

Mheshimiwa Spika, kima cha chini cha mshahara ni shilingi 60,000. Kwa mahesabu ya haraka haraka, kwa Mtanzania ambaye anapanda mabasi mawili tu kwa siku anatumia karibia *half* ya mshahara wake katika nauli tu. Hiyo shilingi 60,000 ninayoizungumzia hapo haijakatwa kodi, ikikatwa kodi inabakia kama shilingi 50,000. Sasa unaona katika mwezi hawa watumishi wa umma ambao wana-*form percent* kubwa ya wafanyakazi wote wa Tanzania hii anakuwa na shilingi 20,000 tu. Hapo ndiyo alishe familia, hapo ndiyo aendeshe maisha yake ya kila siku na kadhalika. Kwa msingi huo, pesa haitoshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilibahatika kupitia hotuba ya aliyekuwa Waziri wa Utumishi akisema kwamba watumishi wa umma maisha yao yameboreka, hali inayopelekea watu kuvutiwa na kujiunga na Serikali. Mimi nimekuwa mtumishi wa umma kwa kipindi cha *almost* mwaka mmoja na nusu. Katika kipindi ambacho nilikuwa hiyo ofisi ambayo nilifanya kazi, nilishuhudia *interview* zikifanywa zaidi ya mara nne, kwa sababu watu

wanakuja, wanaona kwamba hali ni ngumu wanaondoka kwa kuwa wanajua kuna maeneo mengine ambayo wanaweza wakapata *green pastures*.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa umma ambao Mheshimiwa Waziri alikuwa *ana-refer*, labda ni wale ambao wanafanya *TRA* au *BOT* ambao *at least* maslahi yao ni mazuri au wa Wizara ya Fedha ambao japokuwa mishahara yao ni midogo, lakini wana *incentives* nyingine zinazowafanya *wa-survive* kwa mwezi mzima. Kwa hiyo, nashauri kwamba ili hii hotuba ya Mheshimiwa Rais iweze kutekeleza, tuangalie Wizara kutokana na majukumu yao. Tusiangularie Wizara kutokana na utamaduni kwa kuona kwamba Wizara fulani imezoleka kwamba inatakiwa ipate Bajeti kubwa, kwa hiyo, ni lazima ipewe Bajeti kubwa. Naomba tuliangalie hivyo na ninaamini pesa zipo kama mgawanyo ukifanyika *effectively*.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya pili ni kuhusiana na elimu. Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais alisema kwamba tuongeze japo Chuo Kikuu kimoja. Kwanza nimpongeze kwa hilo, kwa sababu ndiyo amekuwa *at least* Rais pekee katika awamu zilizopita kuwa na wazo la kuongeza Chuo Kikuu. Lakini binafsi naona kwamba Chuo Kikuu kimoja peke yake hakitoshi. Ni lazima Serikali yetu iangalie jinsi gani na yenye inaweza ika-*invest* kwenye elimu *in itself*. Tunajua kwamba *MMEM* na *MMES* ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, kwa hiyo, Serikali kwa hapo hata kama inatoa mchango itakuwa ni kwa kiasi kidogo.

Mheshimiwa Spika, vile vile tujue kwamba *EPA* inaanza mwaka 2008, tunataka kuingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mazingira yote hayo mawili kunakuwa kuna *free movement of labour*. Tanzania takwimu zinaonyesha kwamba tunatoa *graduates* 10,000 kwa mwaka wakati wenzetu Kenya na Uganda ni zaidi ya 40,000. Sasa tujiulize, tunasema kwamba tunataka kutengeneza ajira milioni moja kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tutatengeneza ajira za aina gani wakati tuko na watu ambao hawajaenda shule, ambao ni *majority*?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna vitu inabidi tuviangularie kimsingi, kama kweli tuko *serious* na tunasema tunataka tubadilishe uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, juzi kwenye semina, Katibu wa Wizara ya Fedha alisema kabisa China ilifanikiwa kwa sababu iliamua ku-*invest* kwenye elimu. Tusione aibu, tu-*invest* kwenye elimu, tunaweza tukapata shida katika hizi nyanja nyingine, lakini katika *future terms* tutapata *benefit* ya hali ya juu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naona muda umeniruhusu hivyo niongeze suala la tatu ambalo ni kuhusiana na takrima. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais alizungumzia kuhusiana na matumizi ya fedha katika chaguzi na kwamba viongozi inasemekana wanaingia kutokana na pesa zao na inawezekana ni ukweli au si kweli.

Mheshimiwa Spika, tukiwa kama Wabunge, tuna nafasi kubwa sana ya kuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais alisema kwamba uitishwe mjadala wa Kitaifa. Lakini wakati tunasubiri huo mjadala wa Kitaifa uitishwe, kuna *steps* ambazo

tunaweza tukachukua ambazo ziko ndani ya uwezo wetu. Takrima ipo katika sheria ya uchaguzi. Bunge kama chombo chenye uwezo wa kurekebisha sheria, tunaweza kumsaidia Rais wakati tukisubiri kuelekea katika huo mjadala mzima kufanya *amendment* ya hiki kipengele.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba ni kibaya na ninaamini kwamba kuna Wabunge wengi sana humu *whether* wa CCM au wa Vyama vyta Upinzani ambao wameathirika sana na hii takrima kwa sababu watu wanatoa rushwa, wanatumia takrima kama kivuli chake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nizungumzie kuhusiana na *time frame*. Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ametoa matumaini makubwa sana na ninaamini kama hayo matumaini yakitekelezeka kweli maisha ya Watanzania yatakuwa bora. Napendekeza kitu kimoja. Hii hotuba maana yake kila Wizara inakuwa na majukumu yake. Wizara ituletee *time frame* zake kwamba Rais amesema hivi, mimi Waziri nitatekeleza hiki katika kipindi cha miaka mitano, ili miaka mitano ikifika hapa waje watuambie wamefanikiwa kwa kiasi gani na Watanzania wana haki ya kuhoji kwamba yale matumaini waliyopewa yame-fail au yamefanikiwa ili baadaye waweze kufanya uamuzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na ninaunga hoja mkono. (*Makofî*)

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nianze kutoa pongezi kwa viongozi wakuu ambao ni Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais na Rais wa Zanzibar, kwa wote watatu kupewa ridhaa ya kuongoza nchi hii kwa imani kubwa na wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo nitoe pongezi kwa wanaofuatia ambao ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wote na Naibu Mawaziri kwa kuwa wasaidizi wa karibu wa Mheshimiwa Rais kwa sababu ndiyo wanaofuatia kiprotokali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia bila kuwasahau wewe mwenyewe Spika na Naibu wako, kwa sababu tunaamini na tumejizatiti kufanya kazi pamoja nanyi ili kuliletea Bunge na maendeleo ya wananchi kwa maamuzi tutakayoyatoto. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sitawenza kuwasahau Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochaguliwa na kuteuliwa katika sehemu mbalimbali. Sisi sote Mungu ametu jaalia kuingia hapa, atusaidie kwa ujumla wake tuweze kulitumikia Taifa hili kikamilifu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, siwezi kuwasahau wanawake wa Mkoa wa Morogoro ambao walianza mchakato wa kunichagua pale Morogoro, nikasonga mbele nikaenda kwenye Baraza Kuu la UWT na bila kuwasahau Wajumbe wa UWT Baraza kuweza kunirudisha tena humu Bungeni kuwakilisha watu wenye ulemavu Kitaifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hapa nina rai, Chama cha Mapinduzi ndiyo kimeonyesha ukomavu na demokrasia kamilifu kabisa kwamba kinajali makundi mbalimbali, kivitendo kabisa. Kwa hiyo, ningeomba vyama vingine vya siasa vijali navyo makundi yao kwa vitendo. Kwa mfano, kuna chama fulani kilizungumzia kabisa kwenye Ilani yake kuhusu walemavu. Nilidhani hapa nitakutana na wenzangu wakiwa wameingilia mlango mwengine, lakini siwaoni! Kwa hiyo, naomba vyama vingine vya siasa vizingatie suala hilo kwa sababu na sisi makundi mbalimbali tuna umuhimu, tuna hoja ambazo tunawenza tukasaidia Serikali yetu na nchi kuleta maendeleo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, niingie ndani ya hoja. Moja kwa moja niunge mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa sababu kwa kweli kwangu mimi ni maelekezo na muongozo amba unapaswa kutekelezwa kuanzia sasa na nashukuru mengine kwa kweli yameanza kutekelezwa kwa sababu ninaona Serikali inavyokwenda mbio kuweza kukamilisha yale ambayo yamedhamiriwa.

Mheshimiwa Spika, ninajikita ukurasa wa 15 sehemu ya 8 ambapo Serikali ya Awamu ya Nne imetamka kabisa itajali sana tena sana maslahi na mahitaji ya makundi maalum katika jamii. Hapa ninajikita kundi la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, ili lengo hili liweze kutimizwa, ningeomba nishauri au nikumbushe ni mambo gani ambayo yakifanyika yanaweza yakatusaidia kweli kutekeleza kikamilifu hii sehemu ya 8 ambayo Awamu ya Nne imejiwekea mikakati. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahitaji ya kielimu, niachilie mbali chakula, malazi na kadhalika, kwamba ni mahitaji ya jumla kwa binadamu kwamba anapumua, lakini basi kuna haya mengine. Binafsi nimeona hitaji la elimu kwa watu wenye ulemavu ni muhimu sana. Elimu ndiyo msingi na mwanga wa mengi, lakini kwa masikitiko niseme kwamba, Serikali imeweka sera ya undikishaji watoto wote lengwa kuingia madarasani, lakini kwa watoto wenye ulemavu hili limekuwa gumu kidogo kama si sana.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wazazi wanawaficha watoto hawa wasiende shule. Hapo naomba Serikali itumie sheria zile za kuwadhibiti wazazi, walezi kama hawa kwa sababu wanawakosesha haki ya msingi watoto hawa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba katika kutoweza kuingia na kuhudhuria shulenii, bado kuna mazingira ambayo si muafaka kwa watoto hawa ambavyo ni majengo, vifaa vya kusomea na kujifunzia kwa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Tusio na uwezo wa kujisukuma tunahitaji nyenzo za kutupeleka huko shulenii, la sivyo ni ile ya kubebwa na wazazi kwenda na kurudi. Unakuwa mzigo wa mzazi peke yake. Kwa wasioona, atawenza kwenda darasani, lakini bila *brail machine*, bila *tape*, ili kujikumbusha baadaye baada ya kusikiliza inakuwa tatizo. Wasiosikia nao bila vifaa inakuwa tatizo. Kwa hiyo, kwa kweli kuna matatizo kwamba hata mtoto akiandikishwa mengine mengi bado hayajakaa sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, ili kweli *section* hii ya 8 iweze kutimizika, basi labda paongezwe na ruzuku ya kuangalia haya yanayohitaji fedha na ruzuku yenyewe katika shule za binafsi ambazo nyingi zinaendeshwa na Taasisi za Kidini. Elimu ya watu wenye ulemavu ambayo inaitwa maalum iko sana mikononi mwa Taasisi za Kidini. Serikali itoe ruzuku siyo tu kwa walimu wale, ila tu ruzuku ya uendeshaji kwa sababu nilitembelea katika baadhi ya mikoa kipindi cha kwanza nilipokuwa Mbunge, malalamiko ni hayo. Mapadri wanaomba msaada zaidi kwa sababu kwa kweli elimu maalum ina gharama sana kuliko elimu hizi nyingine kwa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kuzungumzia juu ya elimu mjumuisho kwa sababu Wizara au Serikali ina sera hiyo. Si rahisi kiziki ukamchanganya na mtoto mwingine, kiziki huyo akaweza kumudu masomo hata kidogo! Anakuwa pale mbele anaangalia, lakini kinacholewaka hakuna. Jumla tunasema elimu kwa wote. Si wote, kwa sababu wengine wana matatizo haya ambayo yanapaswa kuangaliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie elimu katika suala la UKIMWI. UKIMWI tunajua matatizo yake. Watu wenye ulemavu elimu ya masuala ya UKIMWI inawapitia mbali kabisa kwa sababu semina zinaishia mijini. Hawa wengi wako vijijini na umaskini wao uliokithiri hata wanaowalea wanachoka. Kwa hiyo, elimu hii nayo waipate kwa sababu na hawa ni waathirika namba moja kutokana na matatizo yao mengi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukosefu wa elimu kuna matatizo ya ajira kwa watu wenye ulemavu. Wachache waliosoma hata siku hizi wapo waliofika mpaka Vyuo Vikuu, lakini ajira ni ngumu. Unapeleka barua ya usaili, ukishaonekana kwamba na wewe mtu mwenyewe unajisogeza sogeza tu wala hiyo kazi huipati tena! Kwa hiyo, bado kuna haja ya kuelimisha jamii kwamba hawa watu wanaweza kuajiriwa hasa wale waliokidhi mahitaji na vitu vinavyohitajika katika ajira kusudi waweze kujitegemea na wasiendelee kuwa mzigo kwa jamii na familia zao.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matatizo hapo hapo kwamba watu wenye ulemavu wangeweza kujiajiri wenyewe. Lakini kama elimu yenyewe ina matatizo, vyuo vyao vya ufundi ni vichache, mimi najua kipo kimoja tu ambacho kimebaki sasa hivi pale Dar es Salaam, hakina hata vifaa, hawana hata taaluma, hata ya ujasiriamali. Kwa hiyo, hata kujiajiri wenyewe inakuwa tatizo.

Mheshimiwa Spika, pili, hawana mitaji. Kuna mikopo ya Serikali, ya Mfuko wa Wanawake na Vijana ambayo inasimamiwa na Halmashauri zetu, kwa kweli kwa muda mrefu kutokana na *research* yangu ndogo hawakopeshwi, wanaonekana kwamba hawafai au hawawezi kulipa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la afya. Afya kuna sera ya uchangiaji na imetoa nafasi kabisa kwamba kunakuwa na msamaha kwa wale wasiojiweza kuweza kuchangia masuala ya afya. Lakini kwa muda mrefu utaratibu wa kupata huo msamaha umekuwa na usumbufu, umekuwa mgumu. Huu siyo kwa watu wenye ulemavu tu ambao hawana uwezo, ni hata kwa wazee. Kwa hiyo, nashauri kwamba utaratibu huu uangaliwe upya au basi iwe tu *free* kwamba watu wenye ulemavu wasioweza kulipia,

kwa sababu wapo wanaoweza kujilipia na wazee, basi wapate tu msamaha wa moja kwa moja kuliko kuweza kufuatilia huko kwenye Kamati za Kata na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kuzungumzia suala la chakula na njaa ambayo ipo sasa hivi, lakini Serikali inajitahidi kufanya mengi. Nakumbusha hapa kundi hili la watu wenye ulemavu huko tulipo nashauri wanaohusika wasisahau. Si wao mmoja mmoja, lakini kuna makambi ya watu wenye ulemavu na wasiojiweza nayo haya yasisahauliwe katika *location* ya chakula kwa sababu na wao ndiyo kama hivyo wanahitaji chakula.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mengi ya kuweza kuzungumzia, lakini kutokana na muda na kwamba tutapata tu nafasi ya kuweza kueleza mengine, naona nikumbushe haya machache ili yaweze kutekelezeka. Ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Namwita sasa Mheshimiwa Ruth Msafiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba, wakati huo Mheshimiwa Dorah Mushi ambaye simuoni humu ndani ya ukumbi ajiandae.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi ya kwanza kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa katika kufungua Bunge hili hapo tarehe 30 Desemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa wa kishindo ambao tumeupata. Kwanza ye ye mwenyewe, Wabunge na Madiwani wa Chama cha Mapinduzi hata kuwezesha kuunda Baraza la Mawaziri la Chama cha Mapinduzi na vile vile kupata Serikali nyingi za Mitaa ambazo zinaongozwa na Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa ushindi mkubwa alioupata ambao kwa kutangulia kwao kupiga kura kabla ya uchaguzi wa Tanzania Bara kulileta changamoto kuonekana kwamba upinzani umeendelea kulegea na kukosa nguvu ya kukubalika na hata ikawezesha ushindi wa Tanzania Bara na wa Jamhuri nzima kuongezeka baada ya kuwa tumeona matokeo yaliyotangulia. Nampongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nitapenda kuzungumzia mambo machache kama ifuatavyo, kwanza, napenda kuwashukuru wapinzani kwa kuunga mkono hotuba hii inayothibitisha kwamba wapinzani, viongozi wao, Ilani yao na wao wenyewe mwanzo wao ni Chama cha Mapinduzi.

Kwa hiyo, kwa vyovyyote vile hawawezi kuwa na lolote ambalo ni jipya ambalo ndani ya hotuba iliyotolewa wanaweza wakapata la kuongeza. Ile hotuba ndiyo chanzo ambacho wao wanapata mahali pa kusimamia na hata wanapozungumza wanafanya tu nyongeza, lakini hawana jipya la kuandika. Nawapongeza na ninawaomba muendelee

kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais na kuunga mkono utekelezaji wa Serikali yetu ambao utaendelea katika kutekeleza ilani ya maendeleo ya CCM. (*Makofî*)

Vile vile, nizungumze habari ya maji na nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kuunda Wizara ya Maji ikiwa ni Wizara pekee inayojitegemea. Tunapata maji kutokana na mvua, visima, mito, maziwa, bahari, chemchem na katika maeneo mbalimbali, lakini hali yetu ya ukame katika Taifa letu, mvua kidogo kidogo za miaka miwili iliyotangulia na kukosekana kwa mvua kwa mwaka huu kumesababisha mpaka tumeweza kuwa na janga la njaa ambalo hakika linatishia uhai na maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali yetu kwa kutusudia kuhakikisha kwamba Watanzania wataendelea kupata huduma ya chakula mpaka neema ya mvua itakapokuwa imekuja tena. Lakini ninaomba kusema kwamba Wizara hii ya maji iwe makini sana na ifanye kazi kwa bidii sana kwa sababu maji ni uhai. Ni uhai wa viumbe hai, wanadamu, mifugo, samaki pamoja na mazao mengi yanategemea maji. Kwa hiyo, tunapozungumzia maji tunatarajia kwamba ni lazima Wizara hii ishirikiane kwa karibu sana na Wizara nyingine kuhakikisha kwamba maji ndiyo chanzo cha uhai wa kila kitu.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza kukuza uchumi wa Mtanzania, tunaposema kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa, hatuwezi kulima kama hatuna maji. Tunapohitaji kilimo cha umwagiliaji hatuwezi kumwagilia pasipo kuwa na maji. Kwa hiyo, tunapozungumzia uhai wa Taifa, kiukweli hatuwezi kuzungumzia uhai wa Taifa bila kuzungumzia kuwepo na maji tena ya kutosha. Napenda kuiomba Wizara husika ijitalidi sana kuhakikisha kwamba suala hili la maji inalitazama kwa upana wake.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji wataalam wa ugani wawe karibu sana na wananchi wa Tanzania kwa sababu asilimia kubwa sana ya Watanzania ni wakulima, wengine ni wavuvi, wengine ni wafugaji na wachungaji. Hawawezi kufanikisha yote hayo pasipokuwa na maji. Kwa hiyo, suala zima la maji linarudi pale pale kwamba ndiyo stahiki na ndiyo maisha ya Watanzania , ni lazima liangaliwe kwa makini.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie pia kwa ufupi suala la elimu. Ninamuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba amepania kuendeleza kwa nguvu zake zote ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya mafanikio yote yaliyokuwa yameanzishwa na awamu zote zilizotangulia kusudi kuwezesha Tanzania yenye neema iwezekane na amesema kwamba hakuna Taifa lolote duniani ambalo limeweza kufanikiwa pasipokuwa na elimu, nami naunga mkono.

Mheshimiwa Spika, elimu yetu kuanzia ngazi ya chekechea kufika mpaka elimu ya juu ni msingi ambao utatuwezesha Taifa letu kusonga mbele. Kwa sasa hivi Tanzania tumepega hatua sana katika hatua za chekechea, elimu ya msingi na sekondari, tunaendelea vizuri. Lakini hapo ndipo mkwamo unapoanza. Unaanza kukwamisha watoto wa kike, unakwamisha familia zisizo na uwezo, unakwamisha watoto kwenda kujiunga na elimu ya juu, nafasi ni chache. Kama inawezekana na katika taratibu zinazoendelea ili Tanzania iweze kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anawenza kujitegemea kwa elimu aliyoipata walau ya kidato cha nne, basi kuwepo na uwezekano

wa kuongeza mwaka mmoja ili kila anayeweza kumaliza darasa la 12 atoke kule akiwa na elimu nyingine ya ziada ya kujitegemea. Elimu ile ifundishe ufundi, ifundishe biashara, kilimo, ufugaji au uvuvi kwa sababu si rahisi kwamba Watanzania wote wanaweba kumaliza darala la 12 wakapata nafasi za kuingia katika vyuo kuweza kujiendezea zaidi. Lakini kama kutakuwa na kozi ya ziada walau ya mwaka mmoja inaweza ikasaidia kila anayetoka shule akawa ameweza kuchagua fani yake na anaporudi akajianzishia ajira yake binafsi kwa ile fani aliyokuwa amechukua akiwa shulen.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nitoe shukrani zangu za dhati, tena za moyoni, za chini ya sakafu ya moyo wangu niwashukuru wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini kwa jinsi ambavyo walinipa ushindi wa radi. Nauita ushindi wangu ni ushindi wa radi kwa sababu magazeti yaliandika sana, sana sana likiwemo la gazeti la Rai kwamba mimi siwezi kuchagulika. Wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini heri wachague jiwe kuliko kumchagua Ruth Msafiri! Lakini baada ya kushinda hawakurudi kusema jiwe limeingia Bungeni. (*Makofî*)

Kwa hiyo, napenda niwathibitishie wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini kwamba walitambua mchango wangu wa miaka mitano wa jinsi ambavyo tulitoka katika kuwa na shule moja ya sekondari katika Kata 12 tukawa na shule saba. Wakatambua tulipokuwa na barabara tatu tukawa na barabara 15. Wakatambua jinsi ambavyo huduma ya afya ilikuwa duni tukawa na vituo vya afya. Wakatambua hali ya amani na utulivu na wakatambua jinsi ambavyo nilikuwa ninawatembelea na ninawajali wakanirudisha Bungeni.

Kwa hiyo, mimi si jiwe! Mimi ni Mbunge halali ambaye nilikubalika na wananchi wa Jimbo langu na ambaye nimekuja hapa kuendelea kuwakilisha. Nami nawaahidi kwa moyo wa dhati kwamba, nitaendelea kuwatumikia, kushirikiana nao kwa nguvu mpya, ari mpya na kuwezesha Jimbo la Muleba Kaskazini kuhakikisha kwamba linapiga hatua ya maendeleo kubwa sana ambayo hakika waliponichagua waliitegemea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na ninaunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba kushukuru kupewa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza, naomba nami pia niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Mjini walionichagua kwa kura nyingi, maana haikuwa kazi rahisi. Lakini wakanichagua, nikaweza kumshinda Mbunge wa Afrika na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili. Ni imani yangu Bunge sasa limepata Spika mahiri. Vile vile, nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na tena mwanamke wa kwanza kuwa Naibu Spika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, uniruhusu sasa nimpongeze Rais wetu kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana. Nina hakika kura zake zimefanya Wabunge wengi waingie Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Rais Amani Abeid Karume wa Zanzibar, kwa kuchaguliwa kuongoza kwa mara ya pili Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru mama Salma Kikwete, kwa kazi kubwa aliyofanya kuhakikisha Wabunge wengi tunaingia Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwashukuru na niwapongeze Wabunge wote walioingia katika Bunge hili katika kipindi hiki maana haikuwa kazi rahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia, nimpongeze Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwanza kwa kuchaguliwa na wananchi wake wa Monduli na kwa kuwa Waziri Mkuu wa nchi yetu. Ni imani yangu Mheshimiwa Edward Lowassa ataingia kwenye historia ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 30 Desemba, 2005 katika Bunge hili. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa namna alivyotoa hotuba yake. Ilikuwa hotuba nzuri, lakini pia iliyotolewa kwa umahiri mkubwa na ufundi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Rais aliitoa ile hotuba, lakini pia alikuwa anafanya mazungumzo humu ndani na kila Mbunge, kwa namna alivyoitoa hotuba yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mambo yote Mheshimiwa Rais aliyosema kwenye hotuba yake, kwanza sijui kama alikuwa anafanya makusudi, lakini aliyaelezea matatizo ya Jimbo langu kwa kina kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea mambo machache. Nchi hii tunalo tatizo kubwa la maji na katika Ilani yetu tumesema kwa miaka mitano ijayo asilimia 90 ya maeneo ya mijini itakuwa imepata maji safi na salama na asilimia 65 vijijini watakuwa wamepata maji safi na salama. Nadhani kuna mambo lazima sasa tufanyie maamuzi.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufanikiwa hilo, ningeomba kama inawezekana kwa sasa tuanzishe *National Water Fund* ili tuweze kupata fedha za kutekeleza miradi ya maji. Tulianzisha *Road Fund Board*, matokeo yake mnayaona. Nadhani umefika wakati sasa na maji tuanzishe *fund* kwa ajili ya kupata fedha ya kuleta maji nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania Mungu ameisaidia na ameibariki sana. Tunayo Maziwa makubwa matatu. Tunalo Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na tunalo Zwa kubwa la Nyasa.

Mheshimiwa Spika, maji yote katika maziwa haya ni maji safi na yananyweka. Tumeanza Ziwa Victoria tunapeleka maji sasa Mwanza na Shinyanga. Nadhani sasa tutengeneze *network* ya maji. Tutumie maji ya maziwa haya yamekaaa bila kutumika kwa kiasi cha kutosha. Tuchukue bomba lingine lienzie Ziwa Tanganyika, lilete maji katika Mkoa wa Kigoma wote, lije Urambo na Kaliwa, lije Tabora, lije likutane sasa na lile bomba kubwa linalotoka Ziwa Victoria lilete maji Singida, lipeleka maji Dodoma na hatimaye mpaka Dar e Salaam na Mikoa mingine. (*Makofi*)

Lakini pia, tuchukue maji ya Ziwa Nyasa nayo yaje yaki-*save* Mikoa ya Kusini yakutane pamoja. Ninaamini tukiweka *political will*, jambo hili litawezekana na tatizo la maji nchi hii itakuwa ni historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili basi baada ya maji yale ya mito sasa tuyielekeze kuyatumia vizuri katika kilimo cha umwagiliaji, tuyatumie vizuri katika kutengeneza umeme. Kwa sababu hayo hayo maji yakitumika kwa ajili ya kunywa, yatumike kwa *irrigation*, yatumike pia kwa kutengeneza umeme ndio maana leo tumeona mabwawa yetu sasa maji yanapungua kila kukicha. Umefika wakati sasa tuyatumie maji ya Ziwa Victoria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine uko kwenye barabara. Mimi ningombwa Serikali, iamue sasa tuwe na *custodian* mmoja wa barabara. Tutafute mtu mmoja anayetunza barabara za nchi hii. Tuondoke kwenye kusema barabara hii ni ya Halmashauri, barabara hii ni ya Serikali Kuu, tuondoke huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unapeleka fedha kidogo Halmashauri, zile fedha matokeo yake hazifanya kazi na barabara hazijengwi. Matokeo ya barabara zote za Halmashauri ni mbaya. Naomba sasa tutengeneze mkakati, barabara zote za nchi hii akabidhiwe *TANROADS* ili fedha zote tutakazopata za barabara nchi hii tuziweke kwenye kapu moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba niongelee uvuvi. Ziwa Tanganyika, halijatumika ipasavyo kwa uvuvi. Kuna aina 281 ya samaki katika Ziwa Tanganyika. Umefika wakati sasa Serikali ijielekeze kuhakikisha tunavuna hao samaki na sisi nao watu wa Kigoma tuweze kusafirisha dagaa wazuri waliopo pale na samaki wote kwenda nje ya nchi ili tuinue kipato cha wananchi wa Mkoa wa Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine Kigoma ina matatizo makubwa ya umeme. Umefika wakati na Mheshimiwa Rais, alirudia hapa kwenye hotuba yake basi tujitahidi jambo hili lifanyike kwa wakati ili wananchi wa Mkoa wa Kigoma nao wapate umeme wa kudumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muda umekwisha lakini nataka niongee kidogo kuhusu umoja wa nchi yetu. Mheshimiwa Rais, aliongelea suala la kuwa na shule angalau kila Mkoa shule moja itakayokuwa inachukua wanafunzi wote kutoka nchi nzima. Kwamba jambo hilo lingerudisha umoja wa vijana wetu. Hili ni jambo la muhimu sana.

Naomba sana Bajeti ijayo tujitahidi kila Mkoa sasa uwe na shule moja ya Mkoa ambayo itakuwa inachukua wanafunzi wengi kutoka Mikoa mingine ili tuwachanganya wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja hotuba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba ya Rais. Nakushukuru sana wewe, kwa jinsi ulivyoniona. Nimshukuru Mungu kwa jinsi ambavyo amenitetea sana katika ajali niliyopata mwezi wa kumi na mbili nikitokea kwenye kampeni katika Wilaya ya Kiteto. Namshukuru Mungu sana kwa sababu ndiyo amenisaidia hata nikaweza kuwepo mimi hapa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana wewe kwa kuchaguliwa na Wabunge wa Bunge hili ili kuweza katuongoza kwa kipindi hiki cha miaka hii mitano. Nampongeza tena Rais wetu kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi zaidi ya asilimia 80 hususan hata Wapinzani walimchagua, nampongeza sana. (*Makofi*)

Nimpongeze pia Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa na hatimaye pia kuchaguliwa na Wabunge wote isipokuwa watatu, nampongeza sana. Nawapongeza pia Mawaziri waliochaguliwa kwa kipindi hiki hususan wa akinamama waliochaguliwa kuwa Naibu Mawaziri na Mawaziri. Niwapongeza pia Wabunge wetu waliofanya kazi ngumu katika majimbo yao hadi kufanikiwa kuwepo hapa leo. Nawapongeza sana Wabunge, hata wale wa Viti Maalum. Nawapongeza pia Wakuu wa Mikoa walioteuliwa na Rais wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Hotuba hii inajitosheleza ni nzuri, imegusa maeneo yote. Kwanza, kabisa nikigusia suala la elimu napongeza sana Serikali yetu kwa kuanzisha Mpango wa *MMEM* umesaidia sana pia umefanikiwa. Tuliwahi kutembelea shule tofauti mbalimbali tulikuta watoto 200 mpaka 300 kwenye darasa moja. Kwa kweli mpango huu umefanikiwa sana, sasa hivi watoto wanasoma vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naendelea tena kuipongeza Serikali kwa Mpango wa *MMES*. Mpango wa *MMES* japokuwa Serikali inasema kwamba zitajengwa shule katika kila Kata, lakini ukiangalia sasa watoto tayari wamekwishafaulu na wengine waliofaulu miaka iliyopita hawajapata nafasi mpaka sasa hivi. Sasa tunaposema kwamba shule zitajengwa katika kila Kata ni kwamba wale ambao tayari wamekwishafaulu hawatawahi. Hii inachangia wimbi kubwa la watoto wa mitaani pia. Maana wale watoto waliomaliza darasa la saba, kama hawataendelea na shule za sekondari au kupata nafasi nyingine yoyote labda shule ya ufundi ni kwamba watarudi mitaani, tutapata watoto wengi waliopo katika mazingira magumu ikiwa ni wa kiume ndiyo wale tunawakuta wako kwenye machimbo ya madini. Ikiwa ni wa kike nao tena utakuta mtoto aliyemaliza darasa la saba hawezi akakaa nyumba kwao anaanza kumangamanga na kutafuta ajira.

Hii inapelekea sasa watoto wengi kuharibika. Kwa hiyo, itafutwe namna ya hawa watoto kusaidia kabla hawajaingia mitaani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nashauri watoto kama hawa hawajapatiwa mahali pa kwenda wapelekwe JKT kama ule Mpango wa Jeshi la Kujenga Taifa umeanzishwa basi hao wote waende kule JKT kwa sababu kule pia watajifunza studi za kazi na hatimaye watakuwa wamepata ujuzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kuishukuru Serikali kwa Mpango ule wa Elimu ya Msingi kwa Waliokosa (MEMKWA) hawa ni watoto wenye umri wa miaka kuanzia 10 mpaka miaka 17. Watoto hawa wengi wao kuanzia miaka 14, 15, 16 hadi 17 hawajui kusoma wala kuandika, hawajui hata kuandika jina lao, halafu ni mkubwa sasa kama ni wa kike ni mkubwa miaka 15 hajui kuandika jina lake, limekuwa ni tatizo. Elimu ya msingi inatolewa shule za msingi na yule kama amekwishakuwa mkubwa anaona aibu tena kwenda kuchanganyikana na wale wenzako wadogo wadogo. (*Makofî*)

Mimi ningeshauri na kwa kuwa pia madarasa yale hayatoshi, ningeshauri Serikali ishauri jamii ianzishe pia vituo mbalimbali kwenye Vijiji na Kata vya kuwasaidia wale watoto ambao hawajui kusoma wala kuandika ili kupunguza hilo wimbi la watoto wasiojua kusoma na kuandika. Hii ingesaidia sana kwa sababu kipindi cha mwaka 2003/2004/2005 niliona watoto wengi kuna watu walanzisha hivyo vituo na vikawa vimefanikiwa sana na hatimaye yule mtoto akimaliza pale aidha ni miaka miwili anajua study za ufundi, akitoka pale anaweza kujitegemea. Hii ingesaidia sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala la lingine, naunga mkono pia uboreshaji wa miundombinu ambao umefanyika nchi nzima hususan katika huduma za jamii ikiwemo barabara, elimu, afya na maji. Kwa kuititia hotuba ya Rais, naunga mkono kabisa pale ambapo uzalishaji unapopatikana kwa mfano kama eneo la Mererani, Wilaya ya Simanjiro katika machimbo ya *Tanzanite* kuanzia barabara ya *KIA* kwenda Mererani barabara ni mbovu sana. Barabara ni mbovu na kwa kuwa Rais wa Awamu ya Tatu na Rais wa Awamu ya Nne, pia alishatamka kwamba barabara hiyo, itatengenezwa. Barabara hiyo siyo ndefu sana ni mahali pa kilometra 40 tu kutoka *Kilimanjaro Airport* kwenda Mererani ni kilometra 40. Lakini kutokea hapa kwenda tena Ole-Kesmeti kuna umbali tena. Lakini machimbo ya madini ni sehemu ya uzalishaji, Serikali inapata faida na sioni ni kwa nini barabara ile iwe mbaya kiasi hicho na Serikali ishindwe kufikiria habari za hiyo barabara. Kwanza kabisa kilio changu kwa upande wa barabara ni vifo vya wa akina mama na watoto. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili nami nijaribu kutoa yale niliyonayo kwa kuititia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 30 Desemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea nami kama ilivyo ada nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kura nyingi alizopata ambazo zimempa ridhaa ya kuongoza nchi hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, pamoja na Naibu Spika kwa ushindi mliopata. Kadhalika nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, kwa uteuzi walioupata wa kuwapa nyadhifa walizonazo.

Vile vile nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kupita kwenye Majimbo yao na wale waliokuja Bungeni kwa njia tofauti zilizowafanya wafike hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea nachukua fursa hii kutoa pongezi kwa wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini, ambao mwaka 2000 walinipa likizo, nilikuwa Mbunge hapa lakini wakisema sitoshi wakanipa likizo kwa hiyo, nikapumzika. Lakini mwaka 2005 hawa wananchi wa Kigoma Kusini, wakafuta likizo hiyo na wakaniruhusu kuja kujumuika na wenzangu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais, ina mambo mengi na ukitaka kuchangia kama muda unatosha unaweza kuchangia kwenye kila ukurasa. Lakini mimi nitazungumzia maeneo machache na nianze na suala la elimu na hasa nitakwenda kwenye elimu ya msingi. Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Tatu na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, naye ameonyesha ataendeleza yale yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu kwenye hoja ya elimu. Tumepata madarasa mengi na usajili wa wanafunzi shuleni umeongezeka kutokana na mazingira ya kusomea kuwa mazuri.

Mheshimiwa Rais, anakumbuka alipokuwa anapita kuomba kura kama alivyozungumzia tatizo la maji ni kwamba amelipa umuhimu wa kwanza. Lakini vile vile suala la uhaba wa walimu kwenye shule zetu za msingi ni kubwa sana. Zimejengwa shule nzuri, lakini walimu hawatoshi. Nashauri Wizara inayohusika iweke mkakati wa pekee wa kutusaidia kufundisha walimu hata kama kutakuwa kuna *crash programme* ili wapatikane walimu watakaoweza kukidhi mahitaji yaliyopo sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo langu la Kigoma Kusini shule yenyе walimu wengi kuliko zote ina walimu wanne. Sasa hata kama utawapa madarasa mazuri wanafunzi hawa, lakini hakuna walimu, shule zingine kuna walimu wawili na shule hiyo ina mikondo miwili sina hakika kama tutakuwa tunatoa elimu bora wakati walimu hawatoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ninalotaka kuzungumzia mimi ni suala la kilimo na hili ninalainisha na hali ya njaa iliyopo nchini sasa. Sisi tunaotoka Kigoma, tuna bahati na fahari moja, tangu kabla ya Uhuru mpaka tumepata Uhuru mpaka leo tunavyolalamika kuhusu hali ya njaa nchini, sisi hatujawahi kupata chakula cha msaada na tunajivunia hilo, kwa sababu mazingira ni mazuri yaliyoko kule kwetu kwa kuwa tunayatunza. Lakini lingine kubwa zaidi ni kwamba majirani zetu walioko ng'ambo ya pili ya Ziwa

Tanganyika, nadhani ama ni kwa bahati mbaya au ni kwa kufahamu na wenyewe wanatunza mazingira yao. Kwa hiyo, kutokana na misitu waliyonayo inasaidia sisi kupata mvua.

Lakini hali nzuri ya kilimo na ardhi iliyopo Kigoma, ingeweza ikasaidia kupunguza makali ya njaa katika nchi hii kama utaratibu wa makusudi ungewekwa kuusaidia Mkoa wa Kigoma, ili uchangie kutatua tatizo la chakula kwa kuwawezesha kuwapa nyenzo. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, amezungumzia suala la kilimo cha kumwagilia. Watu wengi tunapozungumzia kilimo cha kumwagilia tunadhani tutamwagilia kutoka kwenye mito tu. Hivi hatuwezi kutumia maji ya Ziwa Tanganyika katika kilimo cha kumwagilia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilidhani watu walioko kwenye sekta ya kilimo, sasa waelekeze nguvu zao huko, kama hawajaweza kupata jibu wafanye utafiti waone kama inawezekana na mimi naamini inawezekana kutumia Ziwa Tanganyika kuweza kumwagilia na tutatatua tatizo la njaa iliyoko nchini. Nimesema tunapa mvua nzuri, lakini mvua hazinyeshi tangu tarehe 1 Januari mpaka 31 Desemba. Kuna wakati wa kiangazi na wakati wa masika na wakati huo tunaweza tukatumia maji ya Ziwa Tanganyika tukamwagilia.

La tatu, ni suala la miundombinu na hili nalielekeza Wizara ya Miundombinu, nalo ni suala la barabara. Naomba kushukuru kwamba hivi sasa zipo juhud zinafanywa, barabara inatengenezwa vizuri kutoka Tabora kuititia Urambo kwako Mheshimiwa Spika kwenda Kigoma. (*Makofi*)

Nashukuru hata kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi limepewa kipaumbele. Lakini ningeomba Wizara ihakikishe kwamba pale Mto Maragalasi eneo la Nguruka, daraja la kudumu linawekewa mkakati wa haraka. Mheshimiwa Rais, alipokuwa mgombea alifika Uvinza wakati anaomba kura tarehe 16 Septemba, 2005, alitamka kwamba Serikali ya Korea Kusini, tayari imekwishatenga fedha. Sasa mara nyingi inatokea matamko haya huwa yanaishi hewani tu. Ningeshauri ufanywe ufuutiliaji wa makusudi wa fedha hizo tupate daraja la kudumu. (*Makofi*)

Tunalo daraja la muda, wenzetu wa Mkoa wa Tabora, wanapata matunda na vyakula vingine kutoka Manyovu Wilaya ya Kasulu kuititia daraja la muda lililoko Nguruka kuja Tabora. Likipatikana daraja la kudumu watafaidika watu wa maeneo mengi ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la mikataba, hili naomba nisome kama Mheshimiwa Rais alivyosema, ninanukuu anasema: "Katika harakati za kupambana na rushwa yapo mambo mawili mengine ambayo tutayangalia kwa karibu la kwanza ni mikataba, tutaangalia upya taratibu za mikataba mbalimbali ilioingiwa na Serikali, Mashirika ya Umma na Idara, zinazojitegemea kwa nia ya kuongeza uwazi na uwajibikaji. Mikataba ni mwanya mkubwa wa rushwa zile kubwa kubwa. Nadhani wakati umefika wa kuwa na taratibu thabiti za kubana na kuziba mwanya huu."

Mheshimiwa Spika, Wabunge wamezungumzia suala la mikataba kuletwa Bungeni. Wabunge hawa ndio wawakilishi wa wananchi, Wabunge hawa ndiyo wanapitia yale mambo ambayo yakishapitiwa kwenye mikataba hiyo yanakwenda kufanya kazi kwa wananchi hao.

Mimi ningependekeza kama walivyopendekeza wengine mikataba iletwe hapa, Wabunge waipitie wajiridhishe na wakishajiridhisha ni dhahiri mikataba hii itafanya kazi ya uhakika na kutakuwa hakuna mashaka na mtu yeoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Kabla sijaanza ningeomba sana nitoe shukurani kubwa kwa wapiga kura wa Jimbo la Rufiji. Wapiga kura wa Jimbo la Rufiji, wamepigana kiume kwa sababu Kitaifa *CUF* walisema watakosa viti vyote lakini kitie cha Jimbo la Rufiji watachukua. Lakini nashukuru wapiga kura wa Rufiji wakaseme hapana. (*Makofi*)

Katika vita hivyo Jimbo la Rufiji limekuwa Jimbo la CCM lakini kwa kweli vita hiyo iliishia kwa mtu mmoja kupoteza maisha yake, katika fujo walizoleta wafuasi wa Chama cha Upinzani cha *CUF*. Nataka nitoe rambirambi kwa familia ya yule mpiganaji wa CCM aliyepotea kwa vita vya kuzuia Jimbo la Rufiji lisichukuliwe na *CUF* na tumefanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba kama ilivyo ada kuwapongeza sana viongozi wa Kitaifa hususan Mheshimiwa Rais, Jakaya Bin Khalfani Mrisho Kikwete, kwa ushindi wa *Tsunami*. Vile vile nampongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kura nydingi alizopata hapa Bungeni. Vile vile napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa kura nydingi mlizopata na hii habari mpya uliyoleta ya *Standard and Speed* tunakuunga mkono wote. (*Makofi*)

Vile vile niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri, kwa kuteuliwa kwao na vile vile kuwapongeza Wakuu wa Mikoa walioteuliwa hivyo karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukubali tu kwamba Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ana sifa za pekee. Ana uwezo mkubwa, nguvu na mvuto wa ajabu, ana upeo mpana, anapenda watu, anapenda maendeleo na anapenda haki. Sifa hizi zinanipa imani kwamba Mheshimiwa Jakaya Kikwete atatuvusha katika matatizo tuliyonayo ya njaa na ujambazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niseme machache kuhusiana na kilimo. Kilimo kimeelezwa katika Ilani ya Uchaguzi kwamba, ni uti wa mgongo wa urchumi na kwamba kitapanuliwa kwa asilimia 20 ili kiweze kusukuma urchumi wa nchi kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, iko sehemu ya nchi hii inaitwa Rufiji, sehemu hiyo ina ardhi kubwa, ina mabwawa mengi ya asili, ina rutuba na bwawa moja, nilizungumza hapa, ukienda samaki wanaruka wenyewe. Wakati huu wa njaa ndiyo nikamwambia Waziri wa Maliasilia turuhusu basi tuvune hata kwa mwezi mmoja ili tuponee njaa. Mabwawa hayo yako Rufiji.

Mheshimiwa Spika, miaka ya 1950 mpaka 1970 Rufiji, ilitoa chakula mpaka wakaitwa *National Service* na *TANU Youth League* kwenda kuvuna na kuambiwa wakishavuna basi ondoka nacho ni chako, hiyo ndiyo neema tuliyokuwa nayo kule Rufiji. Tuliletewa matrekta mengi na yakafanya kazi vizuri. Katika Ilani yetu ya Uchaguzi inazungumzia ulimaji kwa kutumia *plau* la kukokotwa na ng'ombe. Kule Rufiji ng'ombe kwanza ni kitoweo, mara nyingi ukizungumza ng'ombe alime wale jamaa hawakuelewi kabisa hilo la kwanza. (*Makofi*)

La pili, ni kwamba nchi ile ina mboji na ina magugu mengi, *plau* la ng'ombe haliwezi kulima na tangu miaka 1950 wale wenzetu waliotawala wakati huo wakajua hilo, ndio maana wakaleta matrekta na sisi miaka ya 1960 na 1970 tukapelekewa matrekta mengi na tukapata mavuno.

Kwa hiyo, ninaomba suala la kulima Rufiji lizingatiwe kwa maana ya kupelekewa matrekta. Haya yawe ya kukopeshwa kwa masharti nafuu au kama kunawezekana basi yaletwe kwa muda halafu yapelekwe kwingine, lakini tunajua kabisa ulimaji wa trekta ndiyo utatunasua katika matatizo ya njaa hapa nchini kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho katika hili la kilimo, tunaomba Serikali izidishe nguvu zake kuleta ukombozi Rufiji, kwa kurudisha kilimo cha pamba. Warufiji wote katika kampeni hii tumezungumzia pamba itarudi na nadhani Serikali haina njia nyingine ila ikazane kutuletea mbegu za pamba, ituletee wataalam amba wanakwenda shambani siyo wanaokaa ofisini na kama kawaida tupanue kilimo chenyewe kwa kutumia *tractors*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamba ya Rufiji ni pamba ya aina ya *long step* yaani uzi mrefu. Pamba ya aina hii ilikuwa inalimwa kule Misri tu na Rufiji. Wenzetu wakulima hawa wakutoka Shinyanga na wasukuma wote, wanalima pamba lakini utashangaa wenyewe warefu lakini pamba wanayolima ni nyuzi fupi. Sasa naomba kabisa ili kuongeza bidhaa hii ya pamba nyuzi ndefu, kilimo cha pamba Rufiji kirudishwe kwa msukumo mkubwa.

Pili, nataka nizungumzie juu ya habari ya barabara. Barabara kubwa zinazopita *I mean Kilwa Road* mpaka Lindi inapitia Rufiji. Barabara hii kwanza ilitengenezwa na Bibi Titi mwaka 1963 na kufunguliwa mwaka 1965, haikupata tena matengenezo. Wakati barabara nyingine tunajua wameli-surface mara nne mara tano, lakini hii ndio kwanza safari hii sasa imefikia Jaribu- Mpakani kutoka Mkuranga inakaribia Bungu. Serikali naishukuru kwa hilo lakini tumechelewa sana *justice delayed is justice denied*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inakuja barabara aina ya pili, ni barabara za Mkoa. Kuna barabara inatoka Kibiti kupitia Mkongo, kufika Utete kwa kuvuka Mto Rufiji. Barabara hii ni muhimu sana lakini haipitiki kwa sababu pantoni imekufa na *approach* ya kwenda kwenye hii pantoni nayo haipitiki kabisa. Kwa mfano Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyejita, Bwana Frederick Sumaye alifika Utete na akasema anataka kwenda Mkongo, basi ilimbidi apitie Ikwiriri kilometra 84 na kufika Mkongo *where as* kutoka Utete ukivuka pale *Utete ferry* ni kilometra 8 tu, kwa hiyo, nadhani barabara hii wakati umefika ifanyiwe matengenezo na pantoni ipatikane. Lakini hili ninaomba hili Waziri wa Miundombinu aandike kwamba Mheshimiwa Rais alifika Utete, akasema hii barabara lazima ijengwe na pantoni lazima ipatikane wananchi wakamguna pale, akarudia mara mbili, itajengwa na pantoni itapatikana.

Naomba kuunga mkono hoja, lakini Waziri wa Miundombinu tafadhali, tafadhali, Kibiti kwenda Utete ipitike na pantoni ya kivuko cha Utete kipatikane. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini nami kama wenzangu walivyotangulia nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kinondoni kwa kunichagua kwa kura nyingi mmo na leo hii kuingia kwenye Bunge hili. Nichukue nafasi hii na kwa sababu muda ni mchache basi nitoe pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa, walioteuliwa kwa nyadhifa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia kwangu katika hotuba ya Mheshimiwa Rais kwanza nimpongeze kwa kuchaguliwa kwake na kupata ushindi mkubwa, lakini nimpongeze kwa hotuba yake nzuri, hotuba ambayo imeleta matumaini mapya kwa Watanzania. Katika hotuba yake alizungumzia mambo mbalimbali na mimi naomba niyaguseguse, lakini kwa sababu muda ni mchache basi nitakwenda kwa *speed and standards*.

Mheshimiwa Spika, Rais alizungumzia uchumi unaoshirikisha raia, katika Jimbo la Kinondoni, tunao vijana, akinamama ambao wanajishughulisha biashara ndogondogo na biashara za kat. Tunaiomba Serikali iboreshe, ama iweke mazingira mazuri ili biashara hizo ziweze kufanyika vizuri kwa kutoa misaada, kutoa upendeleo maalum kwa makundi hayo ya vijana na akinamama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Dar es Salaam hususan katika Jimbo la Kinondoni tunalo tatizo kubwa sana la maji na Mheshimiwa Rais katika hotuba alilizungumzia na alilipa kipaombele cha kwanza kabisa. Jiji la Dar es Salaam inategemea chanzo kimoja tu cha maji Mto Ruvu, lakini pia hata miundombinu ya usambazaji wa maji hayo una matatizo ama kwa sababu ya uchakavu wa mabomba na zana za kusafirisha hayo maji. Lakini tatizo kubwa ambalo linajitokeza pia wapo baadhi ya watu wanaohodhi, wanahodhi maji hayo na kuyafanya biashara, kitu ambacho kinawanyima watu wengi kupata maji, naomba Serikali nayo iliangular hilo. Lakini nafikiri pia ni wakati muafaka kwa Serikali kuangalia uwezekano mwingine wa kuliletea Jiji la Dar es Salaam maji, tukiachana na kile chanzo chetu cha mto Ruvu, lakini inawezekana pia kama alivyosema Mheshimiwa Rais tunaweza tukachukua maji kutoka

Mto Ruffji. Naomba Serikali iliangalie hilo kwa makini ikiwezekana na iweze kulitekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Rais aligusia pia makundi maalum nami katika Jimbo la Kinondoni makundi hayo yapo, watoto yatima, walemvu, na wazee wasiojiweza. Naiomba Serikali iyaangalie makundi hayo kwa kuwasaidia, kuwapatia elimu na hata kuwapatika huduma bora za afya kwa uraisi zaidi. Dar es Salaam tunalo tatizo kubwa na ninafiki ni tatizo la nchi nzima, suala la ujambazi, pamoja na kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri walioifanya na wanaoendelea kuifanya. Lakini bado inaonekana ujambazi umekithiri, naiomba Serikali iwawezeshe iwapatie nyezo, ili waweze kukabiliana na majambazi hawa ambao na wenyewe pia wana ari mpya. Tunaomba nyezo hizo kwa sababu Jimbo la Kinondoni linasumbuliwa sana na ujambazi na ukiangalia vituo vyetu tulivyokuwa navyo, Kituo cha Magomeni, Kituo vya Kijitonyama Mabatini, hawana nyezo sawasawa za kufanya kazi. Lakini hata vile vituo vidogo ambavyo vipo katika Kata zetu na vyenyewe pia ama vinaukosefu wa askari lakini pia wanaukosefu wa nyezo za kupambana na majambazi hao.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuyatumia Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama kusaidiana na Jeshi la Polisi kukabiliana na wimbi hili kubwa la ujambazi, ambalo limeenea nchi nzima hususani katika jimbo la Kinondoni.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais alizungumzia sana michezo na Rais alionyesha kukerwa kwake na kudumaa kwa michezo katika Tanzania ama kuwa nyuma kwa michezo katika Tanzania, lakini pia alizungumzia suala la migogoro ambayo ndio inasababisha soka la Tanzania ama michezo ya Tanzania kuwa nyuma.

Tunaiomba Serikali pamoja na jitihada ambazo imezionyesha kutujengea uwanja wa kisasa, uwanja ambao nafikiri utaiwezesha Serikali kupata mapato makubwa sana utakapaokamilika na nina matumaini kabisa kwamba uwanja ule utakamilika kama ambavyo imepangwa. Tunaiomba Serikali ipitie upya sera ya michezo, sera hii michezo imepitwa na wakati. Lakini hata ile Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa na yenyewe pia imepitwa na wakati, na ninyi wenzangu ni mashahidi mmeona hata baadhi ya vyama vya michezo vimeshajiondoa kwenye BMT mfano ni Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania. Tayari baada ya Katiba yao kuitishwa na msajili wa vyama vya michezo tayari Shirikisho hilo halina tena mahusiano na Serikali, halina tena mahusiano na Baraza la michezo la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho hapo nyuma tulikuwa tunaona hata chaguzi zinasimamiwa lakini hivi sasa Baraza la Michezo haliwezi kabisa kuiingilia kabisa Shirikisho la Soka la Tanzania. Hii inaonyesha kwamba Sheria hii ya Baraza la Michezo imepitwa na wakati ndio maana vyama vya michezo vinaanza kuikimbia. Tunaiomba Serikali iangalie uwezekano wakuanzisha Sheria mpya ya maendeleo ya michezo ambayo ninahakika ikianzishwa Sheria itaendana na wakati na tunaweza kupata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, migogoro hii ya michezo chanzo kikubwa ni hawa wasajili wa vyama vya michezo vya Wilaya na Mikoa. Wasajili hawa ni maafisa utamaduni,

ambao hawana taaluma na tunafahamu kwamba ukiwa msajili lazima angalau uwe na taaluma ya sheria. Lakini hawa hawana taaluma, wapo tu pale na wao wamekuwa ndio chanzo kikubwa cha migogoro katika vilabu na katika vyama vya michezo. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali pia iangalie upya suala hili la kuwa na msajili msaidizi wa Wilaya na Mikoa ambao hawana taaluma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Rais anakerwa sana na kuzorota kwa michezo Tanzania na kipimo kikubwa ni timu zetu za Taifa, zinapofanya vibaya, lakini tuiombe Serikali sasa kwa sababu timu inayowakilisha Taifa ni kama Balozi wetu anawakilisha Watanzania wote. Tuiombe Serikali itengeneze mazingira mazuri ili wachezaji wetu wawe na hamu ya kuchezea timu ya Taifa. Mchezaji anaweza akaitwa kwenye timu ya Taifa lakini akakataa kwenda anaona ni bora abaki kwenye klubu yake kuliko timu ya Taifa kutokana na huduma mbovu anazozipata katika timu za Taifa.

Kwa hiyo, tunaomba Serikali isiachie vyama vya michezo kuendesha timu za Taifa, Serikali nayo iingilie na isaidie kuhakikisha hasa timu ya Taifa wachezaji wanakuwa na mishahara ambayo itawavutia kuichezea timu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba ninukuu maneno ya Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake alisema kwamba Tanzania yenye neema tele inawezekana, maisha bora kwa kila mtanzania yanawezekana, ni wajibu kila mmoja wetu kutimiza wajibu wake, na hakika wote tukitimiza wajibu wetu basi tutaikoa michezo na Tanzania itapiga hatua katika michezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuunga mkono hoja iliyotolewa. (*Makofii*)

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, kwanza nakupongeza wewe mwenyewe kwa ushindi ulioshinda katika Jimbo lako na ushindi ulioshinda ukakaa kwenye kiti hicho nakupongeza sana. Nampongeza sana Rais Jakaya Kikwete, nampongeza Rais wa Zanzibar Amani Karume na nampongeza ndugu yangu Edward Lowassa, kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu na nawapongeza Wabunge wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais imechangiwa sana na ni hotuba moja nzuri sana ambayo ime-cover kila mahali, ni hotuba ambayo imejitosheleza yenyewe hata bila kuchangiwa. Imesema mengi ukiangalia kwamba useme nini ambayo haikusemwa utakosa. Lakini nipende kusema tu kwamba kuna jambo ambalo Rais alilisema kwamba atajaribu kuangalia malumbano au mgogoro kati ya CUF na CCM, kama atayapatia muafaka amani ije. Lakini hapa tunapochangia sidhani tunamsaidia Mheshimiwa Rais kwa hilo, malumbano yaliyopo hapa Bungeni ni malumbano ya uchochezi. Sidhani tunamsaidia Rais kwa ajili ya hili, wananchi wanatusikiliza tunapolumbana hapa Bungeni, na tunapolumbana ndio uchochezi unazidi, tunazidi kuchochaea. Kwa hiyo, mimi nisingependa kabisa hayo malumbano, tumsubiri Mheshimiwa Rais kwamba ana utaratibu gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba nianze na hilo kwamba kwa kweli kwa maoni yangu malumbano yaliyoko hapa Bungeni sio sahihi, tungemsubiri Rais anampango gani na kusuluuhisha hili tatizo. (*Makofi*)

Jambo lingine ningeomba kumshukuru sana Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, siku hiyo alipofunga Bunge hapa alitupa sisi wananchi wa Longido Wilaya. Wananchi wa Longido pamoja na wananchi wa Wilaya zote saba aliyotangaza hapa wanampongeza, nadhani ni sisi ndio ametuaga vizuri. Tunampongeza sana, lakini naomba Serikali hii ya Awamu ya Nne itekeleza ahadi ya Rais Mstaafu, kuanzia sasa kila kitu kitakachogawanya hapa mpaka Bajeti igawanyiwe katika Wilaya hizo saba. Mimi sipendi kila siku nikifuata tena vitu Monduli, kwa nini mahindi ya msaada yaletwe Monduli. Kwangu ni afadhali kufuatilia mahitaji Kajado kuliko Monduli, Kajado iko karibu kuliko Monduli. Sasa kama tumekuwa Wilaya ya nini kupeleka tena vitu Monduli, nadhani Serikali imesikia hilo. (*Makofi*)

Jambo lingine ningeomba kulizungumzia ni umaskini. Umaskini ni jambo kubwa sana, limeeingia vijijini, umaskini mkubwa sana, lakini huu MKUKUTA tunaozungumzia mimi sioni kwamba unawasaidia watu wa vijijini na nianze kwa suala la mikopo. Tumethaminisha ardhi iwe na *value*, lakini ardhi inakuwa na *value* baada ya kupata hati, kama huna hati hiyo ardhi yako haina *value* yoyote. Mpaka leo vijiji havina hati, vijiji navyo vinastahili kutoa hati kwa wananchi na hawawezi kutoa hati kwa wananchi mpaka wao wawe wamepimiwa vijijini, wawe kwanza na hati ya kijiji, sasa wananchi wanaweza kutoa hati kwa mtu mmoja kwa wananchi kama wao hawana hati ya kijiji. Kuna vijiji 6000 ambavyo havina hati, unafikiri ni wananchi wangapi wapo katika hivyo vijiji 6000, unafikiri hao wananchi watapataje mkopo, tunapitisha Miswada hapa tuwasaidie wananchi lakini bado wananchi hawafaidiki, huu MKUKUTA tunaozungumzia hapa, ni baadhi ya watu ndio wanafaidika watu wa vijiji ambao hawana ardhi. Ardhi ambayo inaweza kuvamiwa na mtu yejote, ningeomba kusema kwamba vijiji vyote vipimwe, wananchi wote waweze wakapewa hati katika maeneo waliyopo na waweze nao kupata mikopo, mikopo haipo vijijini ipo mjini tu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niende haraka haraka nizungumzie suala la elimu. Mimi ninavyokumbuka kuanzia Rais wa Awamu ya Kwanza mpaka huyu aliyeo sasa wote wameona kwamba wafugaji wameachwa nyuma na kila mmoja anatoa ahadi, mpaka huyu aliyeingia Awamu ya Nne ametoa ahadi na ameona kwamba wafugaji bado wako nyuma kielimu, mpaka sasa hakuna mkakati uliowekwa kuwasaidia wafugaji wapate elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabweni, tulisema kwamba wafugaji wanastahili wajengewe shule za bweni, hali ni mbaya ndugu zangu, nawaambia kama tukienda kwa mtindo huu bila kuangalia makabila yaliyoko nyuma, tutatofautiana kama utajiri sasa ulivyo nchini walionacho na wasionacho. Tutakuwa na matabaka ya watu ambao wako nyuma kama ilivyo nchi zilizoendelea na nchi zilizoko dunia ya tatu. Kwa hiyo, ningeomba kusema kwa hilo hebu muangalie suala hili la elimu kwa sababu ni baya zaidi. (*Makofi*)

La mwisho nzungumzie suala njaa, suala la njaa ni tatizo, nilisimama siku moja nikasema kwenye semina kwamba Jimbo langu ndio Jimbo haya zaidi kuliko majimbo mengine yoyote na nadhani mmesikia kwenye redio. Bado nasema kwamba hali ni mbaya, mifugo imehama wameachwa watu wako vijijini lakini hakuna mifugo kabisa wanasubiri sasa ng'ombe wanaokufa wachune ngozi, wauze ndio watu wapate chakula, hakuna ng'ombe anayezika. (*Makofî*)

Kwa hiyo, mimi ili suala la kusema kwamba hakuna mtu atakayekufa kwa njaa, hebu tuangalie kwa sababu siwezi kusema kwamba sio sahihi lakini kama ni sahihi basi vyakula vifikishwe kwa wananchi.

Mwisho ningependa kusema kwamba uandikishwaji wa wanafunzi mwaka huu katika jimbo langu uko chini sana na kwa ajili ya njaa hakuna watoto wanaoweza wakatembea kilometra tano au sita kwenda shuleni, hata mahudhurio shuleni ni mabaya sana kwa ajili ya njaa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kueleza Serikali iangalie jimbo la Longido zaidi kwa sababu hali ni mbaya na ndio maana mmesikia Kenya hali ni mbaya pamoja na Longido, nashukuru sana. (*Makofî*)

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi na mimi nianze awali ya yote kuwashukuru wananchi wa Ludewa kwa kunipa kura zao nzuri zilizoniwezesha kufika hapa kwenye Bunge lako Tukufu, nawashukuru sana. (*Makofî*)

Pili na mimi nitoe pongezi kwa ndugu zetu wote waliopata wadhifa kwa kuteuliwa au kuchaguliwa nafasi mbalimbali kuanzia Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri, Manaibu, Spika na Naibu Spika na ndugu zangu wote Waheshimiwa Wabunge kwa kuweza kufika na kuwa *members* wa Bunge hili Tukufu, nawapongeza sana. (*Makofî*)

Kwa kuwa muda hautoshi nilikuwa na mambo mengi ya kuzungumza lakini nitajikita kwenye mambo manne na nitazungumzia zaidi suala la nishati ambalo pengine ni nyeti na linahusu sana Wilaya ya Ludewa, kisha nitazungumzia suala Teknolojia na Elimu ya Juu, halafu nitazungumzia suala la mazingira na mwisho nikipata nafasi nitazungumzia kuhusu kilimo

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati, mimi namwona Rais wetu ni kama mwana mazingira *number one*, ameweza kugundua kwamba sera yetu tuliyokuwa tunaenda nayo ya umeme ya kutegemea maji haiwezekani tena, na kwa kweli itabidi ndugu zetu wa Wizara inayohusika na *TANESCO* watuthibitishie kwamba itakuwaje kwamba tuweze kurudia hali ya awali ya kutegemea maji. Kwa sababu sote tunajua kwamba *catchments* za Mto wetu Ruaha zimeharibika, kule Ihefu kumeaharibiwa, uwezo wa kuli-*habilitate* ni *very difficulty* itachukua miaka mingi, Mto Pangani ambao tunategemea sana kwa umeme *catchments* zake zimeharibika sana na kwa sababu ya ukame matumizi ya maji kwa *irrigation* na matumizi mengine *catchments* ni makubwa sana. Kwa hiyo,

*competition for water* kwa ajili ya umeme na matumizi mengine ni makubwa sana, kwa hiyo, watuthibitishie tutarudia vipi kwenye hali ya zamani ya kutegemea umeme wa maji, kwangu mimi naona ni ndoto, kama itawezekana watupe mikakati ya jinsi watakavyo li-*habilitate* hizo *catchments* na kuhakikisha kwamba hali ya upatikana wa umeme wa maji utarudia. Kwa sababu hiyo kutegemea ku-*develop Stieglers Gorge* au vyanzo vya Rufiji ni ndoto vile vile kwa sababu vyanzo vya hiyo mito vile vile vimeharibiwa na vinaendelea kuharibiwa, kwa hiyo, hata tuki-*invest* kwenye *other hydro project* bado matatizo yako pale pale kwa hiyo tunabakiwa na gesi na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, nimepata fununu sijazithibitisha lakini inaelekea kuna wenzetu wa *TANESCO* pengine na Wizara wanafikiria kwanza wa-*develop* gesi kwa ajili ya umeme. Lakini hawata-*develop* Mchuchuma au makaa mpaka gesi iishe, maana yake ni kwamba watu wa Ludewa na Watanzania ambao wanafikiria makaa ni *source* ambayo ni *sustainable* wangojee pengine kwa karne moja. Sasa kila watu walipo kwa ajili ya maendeleo wanategemea *resource* walizonazo, wananchi wa Ludewa, wananchi wa Mkoa wa Iringa wanategemea makaa yale iwe kama ni *source* ya maendeleo ya maeneo yale, kuwaacha wamekaa tuna *resource* inakaa kwa muda wa karne nyingine ni kuwaonea wananchi wale. *Unless TANESCO* na Wizara hii ituambie itawapa *altenative* zipi za kuweza kujiletea maendeleo na kubadilika kwa kadri ya Ilani yetu ya CCM.

Mheshimiwa Spika, napata fununu kwamba wenzetu wa Malawi kwa mfano wanasema basi turuhusuni sisi tu-*invest* kwenye Mchuchuma lakini umeme ule wote uende Malawi. Sisi tunasema hapa sisi tutaweka ni akiba yetu mpaka hapo baadaye. Lakini sisi tunataka umeme hata kama hatutautumia tuna-*export* ili tupate fedha za kigeni, kwa hiyo, si lazima tu-*develop* Mchuchuma kwa ajili tu ya kujitosheleza hapa nchini, lakini vile kwa ajili ya kuuza nchi za nje. Kwa hiyo, mimi ushauri wangu ni kwamba tu-*develop* gesi na makaa ya Mchuchuma *from currently* nakubali kwamba gesi itatusaidia *in the very immediately term*. Lakini *in the medium and long term* tunahitaji *both projects* ili *tu-diverse file sources*, tumezoea, tumejjifunza kutokana na makosa tuliyofanya ku-*invest in one source* ambayo ni *hydro* na tukaweka mayai kwenye *basket* moja, matokeo yake tunayaona sasa. Tusirudie kufanya makosa tena, kwenda na *source* moja ya *energy* ambayo ni gesi tutumie *sources* zote zinazowezekana na *both* mkaa na gesi zinakubalika. (*Makofî*)

Kuhusu Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Rais ameona umuhimu wa kuhamasisha watu wawekeze kwenye matumizi ya sayansi na teknolojia, lakini huwezi ukawekeza uka-*develop* kwenye sayansi na teknolojia kama huna takwimu au utafiti. Kwa nchi hii yote kwa kweli katika kila sekta utafiti unapewa kipaumbele kidogo sana. Mimi nimefanya miaka mingi pale Chuo Kikuu kama Mkurugenzi wa Taasisi ya kutathmini rasilimali ya Chuo Kikuu na kila mara inapotokea kukata Bajeti, basi Bajeti ya Taasisi za Utafiti ndio ya kwanza kwenda na mtakubaliana na mimi Wizara nyingi sekta ile upande wa *research* unapewa hela kidogo sana. Kwa hiyo, tunadharau sana mambo ya *research*, hakuna nchi iliyoendelea hapa duniani ambayo haitumii, haifanyii *research* na kutumia *data* na *statistics*. Ushauri wangu ni kwamba Serikali ijitahidi sana kuwekeza katika utafiti tuwe na takwimu ambazo zitatuwezesha kwenye *planning*.

Baada ya hiyo naomba nizungumzie kwenye upande sasa wa mazingira. Mazingira yanachukuliwa kama maana yake ni kupanda miti, tunaona ndugu zangu wengi wanazungumzia kuhusu upandaji miti, lakini mazingira ni pamoja na mioto ambayo inasaambaa mbele ya uso wetu, kila mwaka tuna mioto kila mahali, kilimo ambacho hakifai cha sesa, kwenye miteremeko hata ukipita kwa ndugu yangu Job Ndugai, pale Gairo unaona udongo mwekundu tu ardhi ni nyekundu kwenye miteremko wanalima sesa, udongo unakwenda, tunaona kuharibika kwa vyanzo vya maji, tunaona rutuba ya mashamba inaharibika, yote haya ni masuala ya uharibifu wa mazingira. Ushauri wangu ni kwamba wahalifu wadhibitiwe na waadhibiwe. Ufugaji uzingatie maeneo yanayofaa kwa ajili ya ufugaji na maeneo ya kilimo na shughuli nyingine yaachwe yasipelekewe mifugo.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji vijiji tuhakikishe kwamba inafanyiwa *Environmental Impact Assessment (EIA)*, tumejifunza sasa hata hapa tumezungumza kuhusu mabwawa ya maji ambayo hayako *sustainable* mara nyingi ni kwa sababu hakuyafanya *EIA* na sasa hivi sheria inatutaka tufanye miradi yote tukizingatia matokeo ya *Environmental Impact Assessment*. Kwa hiyo, mimi ningeshauri Wizara inayohusika ihakikishe masuala haya ya mazingira yanatiliwa mkazo zaidi. (*Makofi*)

Kwa upande wa kilimo kwa sababu muda haunitoshi niseme tu kwamba ningeshauri tuzingatie *agro-ecological zones*, maeneno yanayofaa kwa kilimo cha mvua yapewe kipaumbele, yanayofaa kwa *irrigation* yapewe kipaumbele lakini bado *Environmental Impact Assessment* na *Strategic Environmental Assessment* lazima zifanywe ili tuondokane na matatizo ya uharibifu wa mazingira ambayo yanawenza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais inajitosheleza, wajibu wetu sisi ni kuhakikisha kwamba yale yaliyooanishwa mle ndani tunayatekeleza. Nianze kwa kuwapongeza wafuataao, kwanza kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupata kura nyingi za kishindo, nikifuata na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na Rais kushika nafasi hiyo ya Uwaziri Mkuu na kupata kura nyingi za ajabu hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ninakupongeza wewe mwenyewe pamoja na Naibu Spika, nikifuatia Mawaziri na Manaibu Mawaziri na Wabunge wote hapa Bungeni, nawapongezeni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nashukuru Chama cha Mapinduzi kwa kunituwa mimi Aloyce Kimaro, nigombee Jimbo la Vunjo na ninawashukuru wananchi wa Jimbo la

Vunjo kwa kunipa kura nyingi za heshima na nikaweza kuuondoa upinzani ambao ulidumu kwa miaka 10 katika Jimbo la Vunjo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninawaahidi wananchi wa Jimbo la Vunjo kwamba kama walivyonituma, nitawatumikia, naomba tupate ushirikiano, yale malumbano ya chama hiki, chama hiki yamekwisha, kilichobakia sasa ni ushirikiano wa kuchapa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niingie kwenye uchangiaji wa hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwanza tuanze na suala la njaa, suala la njaa ni suala ambalo limeikumba nchi yetu na ni suala ambalo tunatakiwa tulishughulikie kwa dhalura, kwanza kwa kusambaza chakula, hili naona linaendelea vizuri. La pili kusambaza mbegu na utaalamu katika yale maeneo ambayo tayari mvua zinanyesha, tuwe na mipango ya dhalura ya kuhakikisha kwamba wakulima wanapata pembejeo na mbegu zile ambazo zinakomaa kwa muda mfupi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya miezi miwili hiki chakula tulichogawa kitakuwa kimekwisha na kama wakulima hawajazalisha itakuwa bado tatizo ni kubwa, tuandae mipango ya dharura ya ku-*deal* na hili suala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili nichangie kwenye kilimo cha umwagiliaji, miaka yote tumekuwa tunazungumza kilimo cha umwagiliaji na kilimo cha utaalamu, kilimo cha umwagiliaji kinapaswa kupangiwa mipango kama mipango ya barabara. Unapozungumzia kumwagilia lazima kuwa na miundombinu, maji yawepo na yajengewe, ramani ziwepo na maeneo yaoanishwe ni maeneo gani ambapo mwaka huu wa fedha Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, itengeneza miundombinu ya umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile tuoanishe yale maeneo ambayo yanatakiwa yawe na kilimo cha kisasa, kilimo ambacho kinatumia matrekta. Tumekuwa tunasema kilimo, kilimo, lakini kilimo ni kile ambacho kinatumia majembe, tunataka tutambue sasa kila mkoa wakulima wakubwa wako wangapi na ni kina nani na wanalima ekari ngapi, wanazalisha kiasi gani kwa mwaka? Kama tulivytambua wakulima wanaouza chakula tumewatambua Bakhresa, tumewatambua *Mohamed Enterprise*, tumewambua Zakaria, tumetambua *Export Trading* na wengine. Sasa tunataka tutambua vile vile wakulima wakubwa na tuwape support. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile tunazalisha wataalam kutoka Chuo cha Kilimo cha Sokoine, wale wataalam tuwashauri waunde makampuni halafu Serikali iwasaidie waanzishe na wao kilimo cha kisasa, mashamba makubwa. Tunaposikia Zimbabwe wana kilimo, wana mashamba makubwa na sisi Tanzania tunafanya nini? Kila mkoa tuwe na kilimo hicho na vile vile hawa wanaonunua vyakula, wakubwa hao tunawashauri na wao kwenye maeneo yale ambao wanakwenda kununuwa chakula wanunue na wao matrekta, ambao watasmamia wawe wanakodisha kwa wakulima ili wakulima wayatumie wazalishe zaidi na vile vyakula wawauzie wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namshauri *Mohamed Enterprise* kule Singida aanze, awe mfano, anunue matrekta, wakulima wakodishe na vile vyakula watawauzia wale walionunua yale matrekta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine nataka niingie kwenye suala la utalii, nataka nichangie kwenye utalii hasa wa Mlima Kilimanjaro kwa sababu ndio nilikotoka. Mlima Kilimanjaro ni moja ya vivutio vikubwa sana hapa duniani. Mlima Kilimanjaro mwaka jana waliingiza dola milioni 14 ni sawa sawa na pesa ya Kitanzania shilingi bilioni 14 tunatumia mahesabu ya dolamoja sawa na shilingi 1,000.

Mheshimiwa Spika, lakini vijana wetu wanaosaidia watalii Mlima Kilimanjaro hawafaidi kutokana na mapato ya utalii. Tunaomba Wizara inayohusika kuanzia sasa ihakikishe kwamba wale vijana ambaa ndio wanakwenda na watalii mlimani kila mtalii anakwenda na *average* ya vijana watatu, vijana watatu wanakaa siku tano kule mlimani wanabeba nguo zao, chakula, maji, mahema na kila kitu, lakini wale vijana kipato chao ni shilingi 20,000 kwa siku tano. Wale watalii wanawaonea huruma wanataka wawalipe lakini yale makampuni ya utalii wakilipwa ile pesa haifiki kwa wale vijana.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ihakikishe sasa kuna mpango mahsus wa kuhakikisha wale vijana wanalipwa tena kwa kiasi cha dola 20 kwa siku kwa hiyo, kwa siku tano dola 100. Watalii wako tayari kulipa lakini mpangilio wa kulipa haujaoanishwa na Wizara, Wizara wakishachukua ile ya kwao basi ile nydingine wanasema watalipana huko, wao wana makampuni yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nishirikiane na Wizara kuhakikisha kwamba hao vijana wanalipwa kihalali na Mkoa wa Kilimanjaro unafaidi na mapato yanayotokana na utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna watalii walioingia mwaka jana walikuwa 33,255 kwa *average* ya vijana waliokwenda mlimani kwa mtalii mmoja wasaidizi watatu ni vijana 100,000 kama vijana 100,000 wangekuwa wanapata hicho kipato cha dola 100 tungefaidi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais moja kwa moja. (*Makofi*)

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, awali ya yote nashukuru kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana. (*Makofi*)

Kabla sijaanza kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ningetaka kutoa pongezi kubwa sana kwa wananchi wa Mbeya Vijijini kwa nafasi ambayo walikuwa wamenipa kwa kunichagua kwa kura nyingi ili nami niweze kushiriki katika kufanya kazi hizi ambazo sasa ninawawakilisha. Ninawashukuru sana na ninawaahidi kwamba nitashirikiana nao katika kuleta maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ingawa nimetoa shukrani zangu hapa nina uhakika kwamba mara baada ya Bunge hili litakapokwisha mwezi wa tatu nitakwenda kuwatembelea Kata hadi Kata ili niweze kuwashukuru kwa kazi ambayo walikuwa wamenipa, ninawashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, huu natumaini ndio mkutano wa mwisho ambapo tunapeana pongezi, maana yake zimekuwa nyingi kweli lakini nina uhakika kwamba hizi pongezi zitatupa changamoto kutupa nguvu mpya, ari mpya pamoja na kutuwezesha sisi Wabunge kufanya kazi kwa siku zijazo, tunakushukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu hiyo ni mara ya mwisho katika pongezi, ningetaka tu kutoa pongezi kwa wote waliochaguliwa kushika nafasi mbalimbali nikianzia na Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kishindo alichokipata. Lakini vile vile kwa Mheshimiwa Abeid Amani Karume, kwa upande wa Zanzibar na vile vile kwako wewe Spika kwa ushindi uliopata jimboni na kwa kuchaguliwa hapa pamoja na Naibu Spika, Mawaziri na Mawaziri wadogo na vile vile Wabunge wote ambaao kwa sasa tunashiriki katika Bunge hili, hongereni sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ningetaka vile vile kuchukua nafasi kutoa pongezi kubwa sana kwa Rais wetu kwa ajili ya hotuba aliyoitao ilikuwa ni nzuri sana, ilikuwa ni makini na ilitufariji sana. Hotuba hiyo ilizingatia sana Ilani ya Chama cha Mapinduzi na vile vile ilizingatia matatizo ya wananchi yale ambayo alikuwa akiyaelewa, yale ambayo aliyaona alipokuwa akitembelea wakati wa uchaguzi lakini vile vile yale ambayo aliyasikia wakati wa uchaguzi, yote hayo yamejaribu kujumuishwa katika kujenga hotuba yake.

Lakini vile vile inazingatia haja ya kuboresha maisha ya Watanzania wote na mwisho kabisa tumezingatia umuhimu wa kujenga mazingira ya uhuru, haki, upendo, amani na utulivu katika nchi ambayo ndio msingi wa kuweza kutuletea maendeleo. Kazi kubwa iliyoko mbele yetu ni kuweza kuitafsiri ajira hii ili tuweze kuitekeleza kwa ngazi ya Kata, kwa ngazi ya Majimbo yetu na vile vile kwa ngazi ya Kitaifa kwa kushirikiana na Wizara zote. Ninachokielewa ni kwamba tukifanya kazi kwa pamoja na tukishirikiana kwa hakika maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka kushiriki katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa kuanzia na suala la kilimo. Suala la kilimo ni uti wa maendeleo lakini ni uti wa maendeleo tu pale ambapo barabara zetu za vijijini zitakuwa imara, ni uti wa maendeleo pale tu ambapo mazao ambayo yanazalishwa na wakulima yanaweza kufika sokoni. Lakini vile vile ni uti pale tu ambapo mazao ambayo ni ya ziada yanaweza kwenda viwandani ili yaweze kuhifadhiwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia kilimo tujue kwamba mtaji mkubwa kwa mwananchi ni ardhi, Tanzania ina ardhi kubwa ya kutosha, kuna hekta 88.6 za ardhi kati ya hizo 44 milioni zinafaa kwa ajili ya kazi ya kilimo, kati ya hizo ni milioni 6 tu mpaka milioni 10 ndizo ambazo zinatumika kwa kazi ya kilimo ukiangalia utaona ni kwamba bado tuna ardhi kubwa ambayo haijatumika sawasawa kwa ajili ya kazi za kilimo. Lakini natumaini matatizo makubwa ambayo tunayo ni ugawaji na matumizi ya ardhi ambayo

natumaini ndio tatizo kubwa katika nchi yetu na hii inathibitika vile vile kutokana na matatizo ambayo tunayapata ya migogoro mbalimbali katika nchi yetu. Pia nikianza kuchukua mfano wa eneo la jimbo kuna eneo ambalo liko Mbalizi ambalo lilikuwa limechukuliwa na Serikali kwa ajili ya matumizi ya *Tanganyika Packers* ardhi hiyo haikutumika na *Tanganyika Packers* lakini *Packers* ikaja ikabinafsishwa hiyo sehemu ambayo ni ardhi katika eneo la Mbalizi nayo walitaka kuibinafsisha lakini wananchi wengi amba ni zaidi ya 50,000 wanaokaa maeneo hayo hawana eneo la kulima na kwa sababu hawana eneo la kulima ina maana kwamba maisha yao yako hatarini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachoomba kwa upande wa Serikali ni kuhakikisha kwamba wanawarudishia wananchi hao ardhi hiyo ili nao waweze kushiriki katika kuleta maendeleo na kuweza kujajiri wao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, njaa imezungumziwa sana, imewahi kuwa ni matatizo huko nyuma sasa hivi ipo na kwa hakika tusipokuwa waangalifu na kuchukua maamuzi ya makusudi itakuja tena siku zijazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, njaa ni balaa, gharama ya njaa ni kubwa sana, inawezekana kwamba tunazungumzia, lakini hatujalichukulia hili suala kwa undani wake. Fedha za maendeleo nyingi sana ambazo sasa hivi zingeweza kuwa zinatumika kwa ajili ya kuleta maendeleo zinatumika kwa ajili ya kununua chakula, fedha hizo kama tungkuwa tumezitumia kwa ajili ya kuimarisha kilimo tusingeingia kwenye tatizo la njaa. Nguvu kazi inayotumika sasa hivi katika kutatua tatizo letu kuanzia ngazi ya Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya nguvu kazi hiyo ni kubwa sana nayo ni gharama kwa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wananchi kushindwa kufanya kazi zao sasa hivi za maendeleo kwa sababu hiyo kubwa, inawezekana kwamba hata vifo vinawenza kutokea endapo labda hatua za muhimu hazichukuliwi, tunachoomba ni kwamba hatua za makusudi zichukuliwe ili kuhakikisha kwamba njaa haitokei katika maeneo yetu. Ili kuhakikisha kwamba njaa haitokei tunahitaji kuongeza mavuno yawe makubwa katika hekta moja, kuna uharibifu mkubwa sana wa mazao sasa hivi karibu asilimia 40 ambayo yanazalishwa yanaharibika. Kwa hiyo, tunahitaji kuwa na maghala, tunahitaji kuwa na viwanda vyta kusindika, tunahitaji kuwa na bei nzuri ili kuwapa hamasa wakulima wengi kwa ajili ya kuweza kuzalisha zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mbeya ambapo tuna uhakika wa kuwa na mvua nzuri, hatujawahi kupata matatizo ya mvua, tunahitaji kuwa na kiwanda cha mbolea tungependekeza kama kuna matatizo hayo kwa muda wa miaka mitano Serikali ijitolee kutoa ruzuku kwa mwekekezaji wa kiwanda cha mbolea ili sehemu zote za kusini ziweze kupata mbolea ya kutosha na kwa kufanya hivyo tutakuwa na uhakika wa kuweza kupata chakula bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kwamba sisi tunasema kilimo ndio uti wa mgongo, lakini katika nchi hii hatuna kiwanda cha zana za kilimo, hatuna kiwanda cha mbolea, natumaini tunahitajika kufanya maamuzi mazuri katika hilo. Kama tukitumia

mpango huu wa kumwagilia maji vizuri nina uhakika kwamba sehemu za Kusini vile vile zitashughulikiwa vizuri, kwa kufanya hivyo tutakuwa na uhakika kwamba angalau mazao ya mahindi yanaweza kupatikana mara mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mbeya wakulima wa Pareto wamenyanyaswa sana, mazao yao ya mwaka 2001 hawajalipwa mpaka leo, Serikali mwaka 2004 ilitoa pesa lakini pesa hizo walipewa mawakala nyingine zililipwa na wakulima waliokuwa wengi hawakuweza kulipwa. Wakulima sasa hivi wamekataa kulima Pareto.

Kiwanda cha Pareto cha Iringa kimefungwa kwa sababu hakipati Pareto ya kutosha kutoka kwa wakulima. Wale mawakala mpaka sasa hawajachukuliwa hatua yoyote, tungeomba hatua zichukuliwe ili kuweza kuwanusuru hao wakulima na wao wako tayari kuanza tena kilimo cha Pareto endapo walikuwa wamelipwa hela hizo na kwa hakika wameahidi kufanya kazi kwa ari mpya, nguvu mpya ili kuweza kuinua maisha yao.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ni kitu cha maana kwa upande wa Mbeya, tunajenga uwanja mkubwa wa Songwe ambao ndio mkubwa kuliko yote, tumetumia bilioni 27 ili kuweza kufanya kazi hiyo, lakini tusipojitarisha uwanja huo hautatumika vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya hotuba ya Rais. Kwanza kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza katika mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze mchango wangu kwa kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wake wa kimbunga katika chaguzi zilizopita mwezi wa 10 na wa 11 mwaka jana. Napenda pia nitoe ponezi zangu nyingi kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wake Dr. Ali Mohamed Shein na Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Abeid Amani Karume, kwa ushindi wao wa *Tsunami* katika chaguzi hizo zilizopita.

Pongezi na shukrani zangu nyingi pia ziwafikie wapiga kura wangu wa Kisarawe kwa kukipa Chama cha Mapinduzi ushindi mkubwa wa kimbunga wa kutoa kura nyingi sana kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwangu mimi mwenyewe na kurudisha wagombea wote wa Chama cha Mapinduzi wa Kata zote za Wilaya ya Kisarawe, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia wananchi wa Kisarawe kwamba sisi wote waliotuchagua tutafanya kazi usiku na mchana tuhakikishe kwamba tunashirikiana nao ili kuweza kuondoa kero zao na kuweza kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana wewe mwenyewe, Naibu wako na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ushindi wenu. Napenda vile vile niseme kwamba chini ya uongozi wenu na michango ya Bunge hili Watanzania wategemee mafanikio makubwa kutokana na mchango wa Bunge hili. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana wenzetu wote walioteuliwa katika majukumu mbalimbali Serikalini na Wenyeviti wetu tuliowachagua katika Bunge hili ili kuongoza Kamati zetu na mwisho nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushindi wao ambao umetuleta katika Bunge hili, nafahamu haikuwa kazi rahisi, lakini tumeweza kupita na nina amini kabisa kwamba wapiga kura wetu wamefanya kazi nzuri kuchagua Wabunge ambao watawahudumia, ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuchangia hotuba ya Rais, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo inagusa kero zote za wananchi na kwa kweli hotuba hii imekuwa ni mwongozo kwetu sisi wote katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kupelekea mchango wangu kwenye maeneo mawili tu ambayo ni maji na mazingira. Maeneo haya licha ya kupewa uzito mkubwa katika hotuba ya Rais na hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ndio kero kubwa ya Wilaya ya Kisarawe. Nianze na maji, kwenye hotuba yake Rais amesema kuwa maji ndicho kilio kikubwa cha Watanzania mijini na vijijini, ni kweli hiki ndio kilio kikubwa cha wanakisarawe. Mheshimiwa Waziri Mkuu atakumbuka kuwa alipokuwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, alilazimika kufika Kisarawe kuona tatizo hili la maji pale mjini na vijijini, nashukuru kwamba kwa juhudi zake na Serikali tumeweza kupatiwa visima vingi, tumeweza kukarabati Bwawa la Kilaminaki, tumeweza pia kujenga malambo machache, lakini kwa sababu ya ukame ambao umedumu kwa muda wa miaka mitatu mfululizo haya yote sasa hivi hayafanyi chochote na wananchi bado wanapata shida.

Mheshimiwa Spika, akinamama kule Kisarawe hivi sasa wanashinda na kukesha visimani na wengi wao wanarudi bila ya maji, maji hayapatikani hata kwa usombaji wa mikokoteni ambao umekuwa ndio umerahisisha mambo. Sasa hivi ni vijana wachache wenyе kuweza kumiliki baiskeli ndio ambao wanaweza kupata maji na wakawauzia wananchi kwa bei za juu si chini ya shilingi 200/= kwa dumu.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili haliwezi kutatuliwa na malambo peke yake wala haliwezi kutatuliwa kwa visima vifupi, naishauri Serikali na tena kwa dhalura wahakikishe kwamba sasa tunakwenda katika utaratibu wa visima virefu (*boreholes*) hii naamini kwa wakati huu ndio ambayo inaweza ikatuo koa na masuala la malambo na nini yataendelea wakati mvua zitakapokuwa zimenyesha. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niingie kwenye mazingira, ukame unachangiwa sana na ukataji miti hovyo na kilimo katika maeneo ya vyanzo vyya maji, sisi wa Wilaya ya Kisarawe tumeathirika sana na hili, miti imekatwa sana kwa kuchoma mkaa na kuni na

mijengo. Kwa bahati mbaya kuwa karibu na Jiji kuna faida zake na hasara zake, faida kubwa ni kwamba kuna soko la kuweza kuuza mazao lakini hasara ni kwamba mazingira ya Wilaya ya Kisarawe sasa hivi yameharibika kwa sababu ya watu wanamaliza misitu ili kuweza kupeleka mkaa kule Dar es Salaam. Sasa kwa bahati mbaya, pamoja na kwamba Serikali juzi juzi tu imepigwa marufuku uchomaji wa mkaa, lakini mimi nafikiri hii peke yake haisaidii, kwa sababu mkaa ni nishati lakini mkaa vile vile ni ajira kwa watu wa Dar es Salaam, ukisimamisha mkaa maana yake ni kwamba kwa kuwa hawawezi kumudu umeme na umeme wenyewe vile vile haupatikani wakati wote unawaambia kwamba sasa waishi maisha ya zamani kabisa na kwa kule vijijini umeshaondoa ajira, niseme kwamba watoto wetu wa Kisukuma naona wengine hapa hawapo, wale walioshindwa ufugaji wameshamia Kisarawe wanamaliza misitu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa kama hakuna ajira maana yake ni kwamba misitu itaendelea kumalizwa. Kwa hiyo, mimi ningependa nikubaliane na Rais kwamba katika hotuba yake ameododhesha mambo kumi muhimu katika hilo suala la mazingira lipo.

Katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameododhesha mambo manne makubwa ya kuzingatia, katika hilo mazingira lipo. Sasa sisi wa Kisarawe ambao tunaathirika sana kwa uharibifu wa mazingira nasema kwamba hapana budi hatua thabiti zichukuliwe ili suala hili liweze kuleta unafuu kidogo kwa wananchi wa Kisarawe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa tu nishauri yafuatayo, kuhusu maji nimeshasema *boreholes*, kuhusu mazingira mimi nafikiri kabla ya kupiga marufuku uchomaji wa mkaa ni vizuri tuhakikishe kwamba kuna nishati mbadala na hii ni pamoja na kuweza kupanua Mradi wa Kiwira ili utoe mkaa ya mawe, nishati ya jua, upopo na kadhalika ili pawe na nishati mbadala wakati tunapiga marufuku mkaa. Pili tuhakikishe kwamba kuna ajira mbadala, hawa wanaokata mikaa kama hawakupata kazi nyingine ya kujiajiri maana yake ni kwamba wataendelea kukata mikaa au watahamia

Mheshimiwa Spika, wakati wa kampeni tumewaaahidi watu kwa kufuata Ilani ya Uchaguzi kwamba watapewa mitaji, watapewa mikopo, taasisi za fedha zitakuwa zimeelekezwa, nashauri Serikali ihmize jambo hili ili kusudi watu waweze kupata ajira ya kujiajiri wenyewe na waachane na kuharibu mazingira. Pili, tuhamasishe utengenezaji wa majiko ambayo yanaweza kutumia hizo nishati nyingine badala ya mkaa, hiyo vile vile itatoa ajira na itapunguza uharibifu wa misitu.

Mheshimiwa Spika, tatu, nashauri kabla ya kutoa amri hiyo ya kusitisha uchomaji wa mkaa basi upandaji miti uwe ni suala la kufa na kupona, sio miti ya kuweza kutoa kuni na ya kujengea, lakini miti ambayo itasaidia kuleta mvua na kusitiri rutuba ya udongo ambayo sasa hivi inaondoka kwa sababu ya kuwa wazi. Tukifanya haya, ninaamini kabisa tutakuwa tumewaokoa. Naamini haya ninayosema sio Kisarawe tu, lakini yanagusa Wilaya nyingi.

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo yangu kwamba Serikali itayachukua maoni haya kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya ili matatizo haya ya maji na mazingira yaweeze kudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sina haja ya kupigiwa kengele ya pili. Naunga mkono hoja na nakushukuru sana, ahsante. (*Makofî*)

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi katika uchaguzi uliomalizika mwaka jana. Nampongeza sana na tunamtakia kila la kheri Mungu amwongoze ili aweze kufanya kazi zake vizuri na zenyé mafanikio. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza Makamu wa Rais, ndugu yetu Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na Bunge hili kumpitisha kwa kura karibu zote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi ili kuliongoza Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nina uhakika kazi yako unaijua na utaifanya kwa uhakika na naamini tutapata mafanikio chini ya uongozi wako. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Naibu Spika, Mheshimiwa mama Anna Makinda. Kwa kweli sisi wanawake tumefarijika sana na nina uhakika ametujengea heshima ndani na nje ya nchi. Naamini Mama Makinda ni mtu mwenye uwezo na atafanya kazi yake vizuri na sisi tunawatakia kila la kheri ili muweze kufanya kazi yenu kwa uzuri zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile niwapongeze Mawaziri, Naibu Mawaziri na wenyewe kuteuliwa kushika nafasi hii ya uongozi ili waweze kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutenda kazi zake. Nina uhakika Baraza hili wote walioteuliwa wana uwezo mkubwa na nina hakika watamsaidia Mheshimiwa Rais kukamilisha au kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote na vile vile na mimi mwenyewe nichukue nafasi hii kuwashukuru wanawake wa UWT Mkao wa Dodoma hususan Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkao ambao walinchagua kwa kura nyingi na kuniwezesha tena kurudi katika Bunge hili, nawashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda, naomba nichangie machache ili nami niweze kutoa mawazo yangu nini ninachofikiri juu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ni kwamba imejitosheleza na wala haina kipingamizi kwa sababu imelenga kutatua matatizo ya wananchi na imelenga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na imeonyesha dira ni vipi itatekeleza Ilani hiyo. Kwa hiyo, nadhani sisi kazi yetu ni kuiunga mkono na kumsaidia Mheshimiwa Rais ili aweze kutekeleza kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, eneo langu ambalo nitachangia siku ya leo, moja, ni kuhusu makundi maalum. Nianze na kundi la vijana. Kundi la vijana kwa wale ambao wanaomba kuajiriwa, mimi huwa nakerwa na kipingamizi kimoja. Ukitosha katika matangazo ya nafasi za kazi unakuta inaeleza sifa zinazotakiwa unakuta kuna kasehemu ambacho kinaleza kwamba awe na uwezo wa miaka mitatu mpaka mitano. Hivi kweli humu ndani wote tungeajiriwa kwa sifa hizo tungekuwepo humu? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nadhani imeffika wakati Serikali iondoe kipengele hicho kwa sababu vijana hawa si kana kwamba wanaajiriwa waende wakawé Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wa Wilaya au nani wakati mwininge wanaajiriwa katika nafasi za kawaida tu. Unapoajiriwa ndipo unapojifunza kazi na ndipo unapopata uzoefu. Naiomba Serikali iangalie upya kipengele hiki ikiwezekana kiondolewe ili tuajiri vijana wengi wasomi katika nafasi mbalimbali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nizungumzie juu ya vijana ambao wanajajiri wenyewe na hasa wale wanaokwenda mafunzioni kwa mfano wakienda *VETA* na maeneo mbalimbali. Wanapokwenda kule wanajifunza ufundi wa aina mbalimbali bahati mbaya wanapomaliza mafunzo hawana tena mahali pa kwenda kupata uwezekano wa kupata vifaa vya kufanya kazi. Naishauri Serikali ikiwezekana basi wanafunzi hao wakishajifunza katika maeneo mbalimbali basi katika ule mfuko amba ni wa kukopesha vijana waangalie uwezekano wa kukopeshwa vifaa ambavyo anaweza kuondokana navyo pale ili akifika nyumbani aweze kuvitumia na aweze kujajiri mwenyewe kuliko akiondoka mikono mitupu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka nizungumzie eneo la wanawake hasa katika mfuko ule wa kuwakopesha wanawake. Mfuko huu sasa hivi hautoshelezi tena. Kumkopesha mwanamke shilingi 200,000 au shilingi 300,000 au shilingi 50,000 bado hatafanya kazi yoyote na hiyo hela. Naiomba Serikali iongeze hela ili hao akina mama wanapokopa basi angalau ianzie shilingi 500,000 akipata hizo hela anaweza akafanya mradi mzuri na ukaleta mafanikio katika familia yake na akaweza kujiondolea umaskini alionao.

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine ni kuhusu wazee. Nadhani wazee wastaifu kuwafanya watembee kwenda Dar es Salaam kufuutilia mafao yao ni kuwaonea. Kwa sababu uko utaratibu ndani ya Serikali kwamba anayetarajia kustaifu miezi sita anaandalisha mafao yake. Sasa kinachofanya mpaka mzee huyu aende Wizarani kutafuta mafao ni nini?

Naiomba Serikali basi itenye fungu la fedha kwa wale ambao wamestaifu baada ya miezi sita hawajapata *cheque* zao za kustaifu watakopkwenda Wizarani wawalipe

posho na nauli au vinginevyo atafutwe aliyechelewesha aweze kulipa hizo hela. Ni vizuri tuwaenzi wazee hawa kwa sababu wametumikia nchi hii kwa uaminifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na wazee wale ambao wako majumbani. Wazee hawa wakati mwengine unakuta wanahangaika barabarani, mzee huyu hathaminiwi akienda hospitali, mzee huyu hathaminiwi akienda popote pale. Nadhani kuna haja ya kuangalia ile sera ya wazee kama ipo karibu basi ishughulikiwe ili iweze kuletwa Bungeni mapema na iweze kufanyiwa kazi kwa sababu wazee hawa wanapata shida sana na hasa kwa kipindi hiki cha mwaka huu wa njaa, naomba ikiwezekana Serikali itoe kauli kwamba wazee hawa wawe wa kwanza kuhudumiwa wakati wowote wanapoonekana mahali popote wanapohitaji huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la walemavu nadhani linaeleweka na ningeomba wapatiwe vifaa ambavyo wanaweza wakavitumia wakati wanapovihitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie barabara ya Arusha - Dodoma - Iringa. Barabara hii naomba kipindi hiki pamoja na ahadi za Mheshimiwa Rais alizoahidi pengine itashughulikiwa katika kiwango cha lami. Naomba Serikali ilione hilo na kwamba katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ama kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais basi na hili liwe mojawapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la uchafu unaozagaa katika miji yetu mbalimbali. Jambo la kushangaza hili ni tatizo kubwa linaweza kushughulikiwa lakini halishughulikiwi ni aibu kwa wageni mbalimbali wanaoingia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iweke utaratibu mzuri katika miji yote ili uchafu ulioko uondolewe ili kuiweka miji katika hali ya usafi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho ni suala la kilimo. Mimi nasema kwa ufupi kwamba kilimo tulichonacho nchini ni kilimo ambacho kinategemea jembe la mkono. Naomba Serikali kama ilivyounda hii Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji basi wasomi hawa waingie katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kukipongeza Chama changu cha Mapinduzi ambacho kiliniteua ili niwe mgombea wa Jimbo letu la Tandahimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wana Tandahimba wote ambao kwa namna moja au nyingine walinipa kura za kishindo na kuweza kuingia hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Halfan Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, ambaye ni Rais wa Zanzibar, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote pamoja na wewe Spika na Naibu wako kwa kuteuliwa kwa kura nyingi kuiongoza Jamhuri hii ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeguswa sana na hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Imeamsha hisia kwamba huenda ana nia ya dhati kabisa ya kutaka kuboresha maisha ya Watanzania na alivyokuwa akihutubia pale, nina imani mbele kuna mafanikio. Lakini pamoja na hayo nataka kuchangia katika maeneo yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, eneo langu la kwanza ni kuhusu mpasuko wa kisiasa na uzalendo. Nitakuwa na maeneo mawili (a) na (b) katika kuliongelea hili lakini nitazama zaidi katika uzalendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme ni vizuri uzalendo unaotajwa ukaanza hapa Bungeni. Nilisikitishwa sana tarehe 30 Desemba, 2005 wakati Mheshimiwa Rais anaingia kuna baadhi ya viongozi hawakusimama kuonyesha *respect* kwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Sasa kama tuna-*advocacy* uzalendo sisi viongozi tunaomkaribia inakuwaje hatuwezi kuonyesha uzalendo huu hapa? Ikumbukwe kwamba Rais yule ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo, lazima tuanze sisi tulio karibu nawe kumheshimu na kuonyesha kila aina ya mapenzi kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili katika hilo la uzalendo ni kuhusu suala la JKT. Ninachofahamu wakati ule nikiwa Jeshini miaka ile ya 1980 JKT ilijenga uzalendo mzuri sana, ilijenga urafiki na umoja mionganoni mwa Watanzania. Pale tulikuwa tunaongea suala la Kitanzania. Kwa kuwa Serikali ilisimamisha na baadaye kurudisha tena, naomba sana Serikali ijitahidi sana marudio haya yanayofanywa yaende kwa kasi ya juu kabisa. Kwa sababu naamini pale ndiko tunakoweza kujenga mahusiano mazuri na ikiwezekana sasa Watanzania Bara waweze kwenda Zanzibar suala la JKT liende Zanzibar na wale wa Zanzibar waje huku.

Suala la ulinzi na usalama katika nchi yetu ni suala la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini sehemu ya JKT haifanywi kuwa suala la Muungano. Naomba tulifanye kuwa suala la Muungano kwa sababu naamini linaweza kwa namna moja au nyingine likapunguza matatizo yanayojitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili katika mchango wangu ni suala la elimu. Kwa sasa kuna mfumuko au ufahamu mkubwa wa Watanzania kuelewa na kutaka kuwa na haja ya kuwa na sekondari nchini. Sasa hivi kila Wilaya, Kata unasikia kunaanzishwa shule ya sekondari, lakini mfumuko huu wa kuanzisha shule za sekondari hauendana na jitihada za Serikali kuwa na Walimu wa kutosha na majengo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, nina mawazo kwamba kwa sababu suala la wanafunzi wanaoingia sekondari sasa hivi wamekuwa wengi na imekuwa bahati mbaya kwamba

wanafunzi wengine wanakosa nafasi, tufanye hivi, sheria zetu zile za elimu zisiwe *strict* sana tuwe *room for exception* kwamba mahali ambako kuna shule za msingi tatu kijijini basi tuchukue shule moja tuifanye kuwa ya sekondari pale. Kwa mfano katika maeneo ya Tandahimba ninayotoka kuna kijiji cha Mchichira kina shule za msingi tatu na hizi shule mbili zina watoto karibu 500 kila shule lakini kuna shule moja ina watoto 150 tu. Tungeweza tu kuibadilisha ile tukaifanya shule ya sekondari wale watoto watakosa nafasi sasa hivi wakawenza kuwa-*covered* kwenye shule ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tujitahidi kuongeza suala la walimu kwa sababu hata hizo shule za sekondari zilizopo hizo zina matatizo. Nafahamu jitihada zinazofanywa na Serikali kukifanya Chuo cha Chang'ombe, Mkwawa na Mtwara kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki na Viambata, lakini mimi nadhani jitihada hizi zinatakiwa kuongezwa maradufu. Sasa tujitahidi kuwe na angalau kila Mkoa Vyuo vya Ualimu vitatu ili vipunguze tatizo la walimu kwenye shule za msingi na shule zetu za sekondari.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hali ya vijijini kule. Mimi Mkoa wa Mtwara naweza kusema una idadi kubwa ya vijana wanaoitwa wamachinga wanaopatikana Dar es Salaam. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, si kwamba wanakwenda Dar es Salaam kwa sababu wanataka kwenda kutalii tu au kufanya biashara tu pale ni kwamba hatujawatengenezea mazingira mazuri, mazingira bora, *infrastructure* nzuri za kuwezesha wao kukaa kule. Hakuna miundombinu kule, hakuna ajira za haraka haraka kule! Naomba Serikali sasa ijitahidi kwa bidii na jitihada zake zote kuboresha hali za vijijini kule kupatikane maji ya kutosha, barabara ziwe nzuri, umeme, zahanati za kutosha, hali hii haitawafanya wale waende mjini kwa sababu kule mazingira yatakuwa yanawaruhusu.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kuokoa muda kwa sababu kengele ya kwanza imeshalia, nataka kuongelea pia kuhusu usalama wa raia kidogo. Hapa tuna tatizo. Tunawalaumu sana polisi, *of course* wanajitahidi sana kwa kazi lakini Serikali ijitahidi kuongeza ajira ya polisi. Unaenda kwenye kituo unakuta watu watano, wanne, wawili hivi wanajipangaje pangaje kufanya kazi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Tandahimba *of course* liko chini ya *OCD* wa Newala lakini pale kuna kituo Tandahimba ambako ndio makao makuu ya Wilaya mpya iliyoanzishwa hivi karibuni, lakini kuna Maafisa Polisi pale 11. Hivi wanafanyaje kazi, wanataka wawe na zamu na mambo mengi ya kufuatilia pale? Mimi nadhani wakati umefika tujitahidi kwa udi na uvumba Serikali iongeze ajira ya Maaskari wetu wa Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni barabara ya Mtwara - Dar es Salaam kumekuwa na *story* tu nyingi. Naishukuru kampuni ya *CISSO* inayojenga kuanzia Nangurukuru - Mbwenkulu angalau inatia matumaini, lakini kampuni ya *KARAFI* inayoanzia Mbwenkulu - Lindi inatakiwa Serikali iwatupie macho. Kuna haja ya kuwa na *close supervision* na wale kwa sababu ni wababaishaji. Hakuna wanachofanya *they are going very slowly*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatutakuwa na cha kuwaambiwa Watanzania miaka mitano ikiisha hapa. Tumewaahidi ahadi nyingi na kwa kweli zile ahadi mimi nategemea zikamiliike lakini kwa hali ile hatutakuwa na cha kuwaambia. Kura za CCM Mtwara na Lindi kule zimejaa tu, lakini kama kwa kweli tutashindwa pale eeh, sijui yatakayojitokeza mimi naweka tahadhari mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu afya. Mikoa ya Kusini haina Hospitali ya Rufaa. Imekuwa tatizo sasa ukiugua ugonjwa mdogo tu unaohitaji hospitali kubwa kidogo inahitaji gharama kufika Dar es Salaam, wagonjwa wengine wanafia njiani. Naomba Serikali ilione hilo sasa kipaumbele kiwekwe sio tu Kusini na hata Kanda nyingine ambazo hazina Hospitali ya Rufaa tunahiji kuboresha afya za Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni taasisi ya fedha. Mimi ninachojua taasisi za fedha zimekuwa zikitoa mchango mkubwa sana katika uchumi wa mahali popote na sasa uchumi wa Tanzania...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema naunga mkono hoja, lakini tuangalie Wilaya zile ambazo hazina mabenki ili ziweze kuboresha uchumi wa Tanzania, nashukuru. (*Makofi*)

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu nami nichangie hoja hii iliyo mbele yetu. Awali ya yote, napenda kuwapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Kyerwa katika Wilaya ya Karagwe kwa kunichagua kwa kura nyingi ili nirudi tena katika Bunge hili nikiwa mwakilishi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri ambayo imetoa mwelekeo mzuri wa kuonyesha njia ili tuwaletee Watanzania maisha bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitachangia machache, kwanza elimu. Tuna msukumo mkubwa wa kutaka kufanya shughuli ili vijana wetu wanaomaliza shule za msingi waweze kwenda shule za sekondari. Limeshaelezwu juu ya suala la *MMES* leo asubuhi, lakini ni wajibu wangu niiase Serikali ijithidi inavyoweza ili hizi pesa za *MMES* zipatikane haraka iwezekanavyo. Katika Jimbo langu la uchaguzi tayari tuna vyumba 18 ambavyo viko tayari wananchi wanasubiria pesa za *MMES* ili waweze kumalizia na wanafunzi waweze kuanza kusoma. Lakini pia si suala la wanafunzi kuanza kusoma tu, mvua nzito zitakuja hivi karibuni na kama baadhi ya vyumba hivi havikuezekwa, huenda tukawa na matatizo ya vyumba hivi kuharibiwa na mvua na ikabidi kuanza kujenga upya. Hapo hapo kwenye elimu, katika jitihada za Serikali za kuongeza shule na kusajili wanafunzi wengi hasa katika *primary* na *secondary*, kuna wabia wa aina fulani ambao wametusaidia katika kujenga shule. Hawa ni wale ambao wamewekeza katika shule

binafsi kama tunavyoziita. Hawa ni wajibu Serikali iwapatie misaada inavyowezekana. Kwa mfano, sio sahihi sana kumtoza kodi mtu anayewekeza katika elimu kama vile unavyomtoza mwekezaji katika shughuli za baa, *hall za music, casino*.

Mheshimiwa Spika, napendekeza wanaowekeza katika elimu wapewe vivutio maalum ili waweze kupanua shule zao ambapo kiuhakika ni zetu wote, lakini ili tuweze kuvutia wawekezaji wengine katika shughuli hii maalum katika Taifa letu. Tuwape vivutio kama tunavyowapa au kuzidi wanaowekeza katika madini, *Export Processing Zone* ili waendelee kusaidia Serikali yetu katika kupanua elimu.

Mheshimiwa Spika, nishati. Wilaya ya Karagwe hususan Jimbo la Kyerwa tuko pembezoni mwa Tanzania. Magharibi tunapakana na nchi ya Rwanda lakini Kaskazini tunapakana na nchi ya Uganda. Pale mpakani ambapo tunapakana na nchi ya Uganda maeneo yote ya Tanzania na ya Uganda wananchi hawana umeme. Lakini kuna tetesi kwamba wenzetu wa Uganda wana mpango kabambe wa kusambaza umeme kwa watu wanaoishi pale mpakani. Napendekeza na naomba Wizara yetu ya Nishati na Madini iwasiliane na wenzao wa Uganda ili pindi umeme huo utakapoletwa na wenzetu wa Uganda maeneo yetu ya Tanzania yaliyo karibu na Uganda yaweze pia kupatiwa umeme, kwa sababu itakuwa ni aibu, kama vijiji vinavyopakana hiki cha Uganda kinakuwa na umeme na hiki cha Tanzania kinakuwa gizani. Maeneo ninayoongelea ni maeneo ya Murongo, Bugomora, Mabira, Kibingo, Kaisho na Isingiro.

Mheshimiwa Spika, maombi ya Wilaya kamili. Nilivyoeleza ni kwamba Jimbo la Kyerwa liko mpakani na Uganda katika sehemu ya Kaskazini. Wananchi wa Jimbo la Kyerwa wanaiomba Serikali ili kuharakisha maendeleo, ili kuleta usalama zaidi iwatenge Jimbo hili la Kyerwa kuwa Wilaya kamili ya Kyerwa. Naomba hivyo kwa sababu Jimbo la Kyerwa ni kubwa, liko pembezoni mwa Tanzania na suala hili la kuwa mpakani mwa Rwanda na Uganda tunakuwa na matatizo makubwa ya usalama wa raia. Tunaamini kama vyombo vya Serikali vikiwa karibu na wananchi usalama wa raia utaimarika na sio usalama wa raia peke yake wale wa Jimbo la Kyerwa, lakini Mkoa mzima wa Kagera hata na sehemu nyingine za Tanzania kwa sababu haitakuwa rahisi kupitisha vifaa vya kuja kufanya hujuma kama vile bunduki za kuja kufanya ujambazi kama vyombo vya Serikali viko karibu karibu na mpaka wa Rwanda na Uganda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia Jimbo la Kyerwa lina uchumi wa kutosha kujisimamia, lakini pia kwa wananchi wengine wa Jimbo la Kyerwa ni mwendo mrefu kuondoka maeneo yao kufuata huduma makao makuu ya Wilaya ya sasa hivi. Niondoe wasiiasi wa garama, ni kwamba katika Jimbo la Kyerwa tayari baadhi ya miundombinu inayotakikana na Wilaya iko tayari. Kwa mfano tuna Kituo cha Polisi, *Health Center* nzuri ambayo inaweza kupanuliwa na ikawa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, suala la mawasiliano. Tukiwa pembezoni mwa Tanzania, mawasiliano ni muhimu sana. Shirika la TTCL miaka 7 au 8 iliyopita ililetu simu za kawaida, lakini ilizisambaza katika Kata moja ya Kaisho, tangu miaka hiyo hawajajitahidi kusambaza katika Kata nyingine 10 za Jimbo hilo. Napenda niwahimize waje wasambaze huduma yao katika kata nyingine za Jimbo la Kyerwa. Kwa njia ya

pekee niwashukuru watu wa *Vodacom* na *Mobitel*, baada ya kusikia kilio chetu wameshakuja na wameonyesha nia kubwa kabisa ya kuja kusambaza huduma zao, sio katika Jimbo la Kyerwa peke yake, lakini na katika maeneo mengine ya Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, Jimbo la Kyerwa limebarikiwa kuwa na rutuba na maeneo mazuri ya kilimo na mazao yake ya maharagwe na mahindi yanasaidia sehemu nyingi za Mkoa wa Kagera, lakini pia yanasafirishwa mpaka Kahama na Shinyanga. Vijana wa Jimbo la Kyerwa wanaiomba Serikali iwasaidie kwa kuwapatia mradi wa kuweza kupata matrekta ya kukodisha ili waweze kulima na kuuza zaidi na kujipatia maisha bora, na wasaidie Taifa katika kupambana na kilio cha njaa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia wa dakika mbili hauruhusu tuendelee na mjadala huu. Kwa hiyo, itanibidi nisitishe shughuli za Bunge kabla ya wakati wake.

Nitangaze tu kwamba saa 11.00 jioni atatangulia Mheshimiwa Saning'o Kaika Telele, atafuatiwa na Mheshimiwa Nimrod Mkono wajiandae na kuwahi kwa kuwa tutakuwa tunaanza hiyo saa 11.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kutokana na namna tunavyokwenda vizuri katika kujadiliana, tunao wasemaji 12 na majadiliano yetu ya dakika 10, wote watafikiwa na hao ndio watakuwa wachangiaji kwa hoja ile yote ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa maana hiyo, baada ya kumaliza hao 12, mnakumbuka tulitengua kanuni ya 49(A) (a) kwamba tupunguze muda. Kwa hiyo, baada ya kumaliza orodha hii, ile kanuni imeshakwisha kazi yake tunarudi kwenye kanuni yetu ya kawaida ya dakika 15 kwa kila mchangaji.

Kwa hiyo, sasa nitamuita Mheshimiwa Saningo Kaika Telele atafuatiwa na Mheshimiwa Nimrod Mkono na Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki ajiandae. Mheshimiwa Telele!

**MHE. KAIKA SANING'O TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais mchana huu na kuwa mtu wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, naomba na mimi niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na Watanzania lakini vilevile kwa ndugu yangu Waziri Mkuu kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Monduli kuwa Mbunge wa Monduli lakini baadaye kupendekezwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge hili kuwa Waziri Mkuu kwa kura nyingi.

Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, Mawaziri na Manaibu wao, Wakuu wa Mikoa walioteuliwa mionganii mwetu kuwa Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wabunge wote nawapongezeni sana kwa kuchaguliwa na wananchi kutoka Mikoa yenu. (*Makofî*)

Bila pia kuwasahau wananchi wangu wa Jimbo la Uchaguzi la Ngorongoro, nawashukuru sana kwa sababu walianza kuonyesha imani yao tangu kwenye kura ya maoni na wala hawakutaka niingie kwenye mikiki mikiki ya kampeni, nimeshinda kwenye kura ya maoni na hivyo kupita bila kupingwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwanza niipongeze kwa kweli ni hotuba nzuri sana, inaeleweka vizuri na mimi nafikiri kwamba kama Serikali huwa inakuwa na ilani yake basi hii ni ilani ya Serikali kama ambavyo Chama cha Mapinduzi kinakuwa na ilani yake. Kwa kweli tumepewa maelekezo na maagizo ya kutekeleza na kama tungeweza kutekeleza vizuri inavyotakiwa hapa au ilivyozungumzwa hasa katika hotuba hii, kwa kweli tungekuwa tumepiga hatua nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la njaa ni jambo ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi kwa uchungu sana lakini mimi naona kwamba Serikali kwa kweli imefanya kazi kubwa sana tangu ilipoona dalili za njaa nchini, imefanya kazi kubwa ya kutafuta chakula. Tatizo tu linaweza kuwa kule katika ngazi ya Tarafa, Kata na Kijiji kwani watendaji pengine wanaweza wakazembea katika suala hili lakini kwa kweli tutaomba Serikali itoe maelekezo yanayoelewka kwa watendaji wa ngazi za chini ili chakula hiki kwa kweli kiweze kuwafikia Watanzania waliokumbwa na njaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niko kwenye sekta ya utalii, ukurasa wa 47, Mheshimiwa Rais ametaja utalii kwa ni moja ya sekta ambazo ni muhimili mkubwa wa uchumi wa nchi yetu, hii ni kweli. Tanzania yetu hii tunazo Hifadhi za Taifa kama 13 au 14. Watalii wanatembelea Hifadhi za Taifa na kutokana na watalii wanaoingia nchini tunapata pato kubwa la fedha za kigeni. Lakini hizi *National Parks* kwa mfano Ngorongoro siyo Hifadhi ya Taifa, Ngorongoro kama ilivyo yenyewe pale ina matumizi mseto, ni *Multiple Land Use* kwa sababu wako Wamasai pale wako na mifugo yao, wako wanyama pori, ni *Multiple Land Use*.

Lakini naogopeshwa na maneno ambayo yanazungumzwa kuhusu Ngorongoro ndani ya nchi na nje ya nchi. Ngorongoro inazungumziwa kama ni *World Heritage Site* yaani ni Urithi wa Ulimwengu. Ile Ngorongoro inazungumziwa kwamba *it is an international biosphere reserve*, inazungumziwa kwamba ni *eight wonders of the world*,

inazungumzwa kwamba *it is a tourist destination*. Sasa mimi napata matatizo kwamba haya maneno ni makubwa kwa eneo lile kiasi kwamba juzi hapa Mzee Ngombale ametupa semina ya kusema kwamba Mbunge anapaswa kuangalia mambo matatu, lazima aangalie maslahi ya Jimbo lake la Uchaguzi na lazima aangalie maslahi ya Chama chake na lazima aangalie na kukereketwa sana na maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Ngorongoro haizungumzwi kwamba *it is also a nation heritage site*, wala haizungumzwi kwamba *it is also a local heritage site*, inazungumziwa kwamba ni eneo la Kimataifa tu. Sasa mwisho tunafika mahali tunajenga mawazo ambayo tunalihamishia eneo hili Ulaya huko kwenye *ma-international wanakozungumzia*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi kidogo hili linanipa tabu lakini tutaendelea na nitaomba Bunge hili tuendelee kusema kwamba Ngorongoro ni sehemu ya Tanzania na kwa hiyo Watanzania wana haki na eneo hili kama ambavyo linapigiwa upatu kwamba ni eneo la urithi wa dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine kule Olduvai Gorge kuna masalia ya mifupa ya binadamu wa kale miaka mingi sana iliyopita kama *million 3 or 4 years ago*. Lakini wakati Mheshimiwa Rais akiwa kwenye kampeni alikuja mpaka Olduvai akapata maelezo mazuri sana kuhusiana na eneo lile lakini akavutiwa sana baadaye akataka kwenda mahali panaitwa Laitore, Laitore kule kuna unyayo wa binadamu wa kale miaka mingi sana iliyopita. Lakini ukifika pale hakuna kinachoonekana sasa. Rais, Mgombea wakati huo wa Chama cha Mapinduzi akanauliza kwa sababu nilikwenda kumpokea unyayo wenyewe huu unaozungumzwa uko wapi kwa sababu ni mawe tu yamefunikwafunika pale hakuna kinachoonekana. Mimi nikababaika kidogo kwa sababu sasa kwa nini haionekani ndiyo baadaye Wataalam wakasema tumeshauriwa tufunike kwa sababu unajua mambo ya maji yatakuja maji yatachukua. Lakini akauliza tena hivi mna uhakika bado iko au Wazungu wametuibia? Sasa watu wakababaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nafikiria kwamba Wizara inayohusika kwa kweli itengeneze *museum* palepale Laitore kama ambavyo kuna *museum* kule kwenye Olduvai Gorge ambapo mifupa ya aina zote inapatikana pale kwa sababu Mzungu kutoka kule anataka huo unyao wa kale lakini asione huwezi kum-*convince* kwamba ipo kama ambavyo na Mgombea wa Urais alikuwa hajawa *convinced* kwamba ipo.

Lakini lingine ni kwamba tuna maboma ya Kitalii, tunaita *Cultural Bomas*. Haya maboma tunayaanzisha kwa sababu ya kuwasaidia Wamasai wale wakati wa kiangazi kama ilivyo sasa wanapatapata pesa kule wakiingia watalii kila gari ni shilingi 50,000/= lakini wanachopata wao ni shilingi 20,000/= pekee na shilingi 30,000/= inakwenda kwa *Tourist Drivers* wale ndiyo wanachukua hiyo. Kwa hiyo unakuta maboma yale *literal* wanawafanya kazi hawa watu wa utalii. Huu ni unyonyaji na tunafikiria kwamba tungewasaidia hawa watu kupunguza umaskini unaotokana sasa na ukame na mifugo inapokosa malisho. Nitaiomba Wizara inayohusika kwa kweli isaidie kusimamia hili kwa sababu inaonekana Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro yenyewe imeshindwa kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni Sheria ya Ngorongoro. Sheria ya Ngorongoro ni ngumu sana lakini nina matumaini kwamba kwa sababu Taifa limeanza kuangalia ile Sheria ya Wanyamapori Namba 12 ya Mwaka 1974 nadhani hiyo imefikia hatua za juu na wakati wowote inaweza ikafikishwa kwenye Bunge hili kufanyiwa marekebisho. Nina imani hata Sheria hii ya Ngorongoro kwa mtiririko huo tunaanza na Sheria kubwa tunateremka tunaweza tukafikia mahali tukarekebisha kwa sababu Sheria hii kwa kweli imewabana watu sana kiasi kwamba kwa kweli eneo lile la Ngorongoro linaweza likabinafsishwa kwa mwekezaji pamoja na Ndugu zangu wale Wamasai wakabinafsishwa mlemle. Hili linawezekana kwa sababu kwa kweli sheria zinawabana mno hawana *say* yoyote katika hili, sasa nafikiri hili tutaendelea kuiomba Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE: BALOZI HAMIS S. KAGASHEKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Naona muda unatubana kwa hiyo nitajitahidi kuyasema hayo ambayo nitayasema na nitayaacha yale ambayo wenzangu wameshayasema.

Lakini kabla sijaingia katika mada hii ya kuizungumzia hotuba ya Mheshimiwa Rais, naomba kwanza nimponeze ye ye mwenyewe Mheshimiwa Rais kwa ushindi wa kimbunga, nimponeze Waziri Mkuu, Mawaziri, Spika, Naibu Spika na Wabunge wenzangu katika jitihada tulizozifanya mpaka hivi leo tukawa katika Bunge hili Tukufu.

Baada ya kusema hayo, napenda sana nipeleke salama zangu za pongezi kwa Mheshimiwa Aman Abeid Karume na Chama cha Mapinduzi Zanzibar. Nina sababu za Msingi kusema hivyo kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Rais katika hotuba yake kwamba zumari inapopigwa kule Zanzibar basi huku Bara huchezwa lakini nafikiri *situation* ilikuwa *more relevant* kule Bukoba kwa sababu zumari ilipopigwa kule Zanzibar kwa kweli Bukoba tulicheza sana. Kwa hiyo tunawashukuru sana wenzetu wa Zanzibar. Tunawashukuru sana kwa ushindi huo kwa sababu mlitupa sana moyo na ninadhani mnaelewa ninasema nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, hotuba ya Mheshimiwa Rais nikiitazama nasema kwamba *it is an omnibus statement; it is a policy statement* ambayo kabisa Rais hakuacha kitu amekwenda katika maeneo yote ambayo yatahitaji kuwa *covered* katika kipindi chake cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika mtazamo wangu nadhani ili mambo mengi yaliyo katika hotuba hii yatekelezwe, kuna kitu kimoja ambacho ni muhimu na chenyewe ni *mechanism* ya kutekeleza mambo ambayo Mheshimiwa Rais ameyataja katika hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeweza nikashauri labda *mechanism* hiyo ingeweza kuwa *Cabinet Secretariat*, lakini *Cabinet Secretariat* mimi ninavyojua ama ninavyofahamu ni chombo ambacho kimekuwepo kwa muda mrefu sana na ni chombo

ambacho sidhani kama kimepewa nguvu za kutosha kuweza kufuatilia jambo kama hili lakini nadhani iko haja ya kuwa na chombo ambacho kitatazama haya maamuzi na baadhi ya mapendekezo ambayo Rais ameyaweka na kutazama vipi yanatekelezwa kwa sababu kama kumekuwa na upungufu wa aina fulani hata katika maamuzi ya Baraza la Mawaziri naweza nikasema ingawaje mimi sijawahi kuwa katika Baraza hilo lakini utekelezaji wa maamuzi ambayo yanafanyika pale limekuwa ni jambo ambalo linaachiwa Wizara peke yake kutazama ni vipi linaweza likafanya. Lakini nadhani kama kungekuwa kuna *mechanism* ambayo ingeweza ikafuatilia utekelezaji wa maamuzi ambayo yanachukuliwa katika ngazi hiyo lakini pia katika mambo ambayo Mheshimiwa Rais ameyataja humu ambayo mengi yanataka utekelezaji. Ipo haja ya kuwa na *mechanism* ambayo inaweza ikafuatilia utekelezaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani mahali ambapo inaweza ikawa *suited* labda ni katika ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa nini nasema katika Ofisi ya Waziri Mkuu? Kwa sababu mambo ambayo Rais ameyataja humu na utekelezaji wake unagusa kutoka katika *Central Government* mpaka katika *Local Government*. Nikimtazama Waziri Mkuu namuona yeye ndiye kiongozi wa shughuli za Serikali hapa ndani ya Bunge lakini pia nikitazama *Local Government* naona ziko chini yake. Kwa hiyo, nafikiri katika hili ni wazo tu ambalo nalitoa sina nia mbaya wala *hidden agenda* hapa isipokuwa nadhani iko haja ya kuwa na chombo ambacho nadhani kitafuatilia utekelezaji vinginevyo kama chombo hicho hakitakuwepo nachelea kusema kwamba kumekuwa na maamuzi mengi ambayo tumefanya, kumekuwa na *statements* nyingi ambazo zimetolewa, kumekuwa na maadili na mambo mengi mazuri lakini utekelezaji wake umekuwa ni tatizo kwa sababu kumekuwa hakuna ufuutiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nikiendelea katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais anasema kwamba kwa mfano ukurasa wa 8 na 9 anazungumzia kwamba na *infact anam-quote* Rais Mkapa au *kum-paraphrase* kusema kwamba pawe pana maadili yatakayotawala shughuli za kisiasa ambayo hayategemei hiari ya viongozi wa kisiasa walioko madarakani na kadhalika. Mimi nafikiri hili linataka ufuutiliaji, ni jambo zuri na ni wazo zuri lakini ni vipi linaweza likafanywa, linatakiwa ufuutiliaji.

Halafu ukurasa wa 9 anasema kwamba ingekuwa ni vema kujua mambo yanayohusu pesa katika masuala yote ya kampeni. Sasa hili suala la pesa katika suala la kampeni kwa kweli ni muhimu. Lakini kidogo ninachokijua mimi kwa mfano kama Marekani hili suala limekuwa katika Bunge la Marekani *for the last 20 years*. Maana yake wamejadili kuona ni njia gani za kutumia na waamue vipi na vyanzo vya pesa za kampeni na mpaka sasa hawajapata suluhu katika suala hili. Lakini hii haina maana kusema kwamba si suala muhimu ni suala muhimu na ninadhani ipo haja na sisi kulitizama kwa sababu zipo nchi *in fact* hata juzi Mmarekani mmoja ambaye aliweka *contribution* yake kwa Rais Bush imekuja kugunduliwa kwamba alikuwa ni mtu ambaye amekuwa na *scandals* nyingi sana kiasi cha dola 20,000 ikabidi zirudishwe taratibu. Lakini ikaonekana kwamba bado kufuatilia vianzilio vya wale ambao wanatoa *contributions* zao katika watu ambao wanagombea katika *Public Offices* ni kitu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wengi watakumbuka limekuwa ni tatizo katika baadhi ya nchi hata Colombia *drug traffic*, watu ambao wako katika biashara za madawa wamekuwa wanatoa pesa zao katika kampeni kiasi kwamba hiyo inaleta matatizo katika uendeshaji wa shughuli za Serikali. Kwa hiyo nadhani ni suala muhimu jinsi litakavyokuwa *tackled* hiyo ni habari nyingine lakini upo umuhimu wa kulifuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, nikakimbia kwa harakaharaka anapokuja Mheshimiwa Rais kuzungumza katika utawala bora. Katika utawala bora *of course* amezungumzia mgawanyo wa madaraka kwa mihimili mitatu. Amezungumzia juu ya utawala ambao ni *Executive*, amezungumzia juu ya Bunge ambayo ni sisi hapa na amezungumzia juu ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa hapa mimi nitasema kwa harakaharaka ni kwamba ukitizama Utawala *and that is the Executive* ama *the Presidency* ni upande ambao unakwenda kuchaguliwa, wanakwenda kwa watu, wanakwenda kutafuta *mandate* kwa watu, wanajieleza kwa nini wachaguliwe. Inapokuja katika Bunge pia sisi hivyo hivyo tunakwenda kwa watu tunajieleza kwa watu, tuna sera za Chama chetu, tunajaribu kuwa-*convince* watu kwa nini watuchague. Lakini inapokuja katika upande wa Mahakama, Mahakama siyo hivyo. Mahakama inachaguliwa na *Executive Branch*. Nafikiri na hili ni wazo tu katika utawala bora na katika matatizo ambayo yamekuwepo katika Mahakama ipo haja tutazame utaratibu kama nchi nyingine zinavyofanya kwa mfano kama Marekani suala la Mahakama linakuwa ni suala ambalo limeachiwa kati ya *Legislative* ambayo ni Bunge na *Executive*. *Of course* Wabunge hawawezi wakachagua ni nani watakuwa Majaji kazi ya kupendekeza inakuwa ni kazi ya Rais lakini kazi ya kuitisha inakuwa ni kazi ya Bunge. Sidhani kama hili ni suala ambalo ni *so complicated* kwa sababu kama tunaweza tukapitisha jina la Waziri Mkuu wa nchi ambaye Kikatiba sasa hivi ni *number three* na Rais ye ye anapendekeza jina linakuja katika Bunge na Bunge linatazama likiona kwamba ni sawa anapita. Sasa nafikiri iko haja hata ya upande wa Mahakama *honestly* hili ni wazo sina *agenda* ambayo unaweza ukasema ni *hidden agenda* lakini nafikiri linaweza likatazamwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo linahusu ulinzi na usalama, ukurasa wa 60 na 61. Mimi nataka kukumbusha kitu kimoja ni kwamba Polisi sasa hivi wamekuwa kwa kweli wanajaribu kujitetea na kumekuwa na mambo mengi katika magazeti lakini ukweli unabaki palepale na wenyewe ni kwamba *image* ya Polisi katika macho ya watu ni mbaya na unapozungumzia matatizo kwamba Polisi wana matatizo kweli tunayajua lakini siyo wao peke yao, kuna Walimu wana matatizo, Manesi wana matatizo, kuna Askari Magereza na matatizo yako *everywhere* katika sekta mbalimbali. Kwa hiyo, Polisi siyo wao peke yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa mimi nadhani kumekuwa mfano kama mwaka jana kulikuwa na Tume ya Jiji Kisanga ambayo ilitoa *report* yake na *report* *ili-focus* katika Polisi na ilikwenda katika Wilaya karibu 34 na wakaja na *findings* na *recommendations* zao. Mambo mengi ukiyatazama mle inaonyesha kabisa udhaifu ambao umekuwepo katika *Department* ya Polisi. Kwa hiyo, ipo haja ya kutizama na ku-

*take action* lakini taabu ni kwamba huwa tunaunda Tume zinatoa ripoti zao lakini machache yamekuwa yanafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba kwa mfano kama pale Bukoba ninapotoka kwa kweli Polisi ya pale mimi mwenyewe wakati wa kampeni ilikuwa wakati wote nikizungumza na *Regional Police Commander* nikimweleza matatizo ambayo tulikuwa nayo pamoja na *RCO* ambaye ni mtu mzuri kabisa lakini wengi waliobaki akina *OCD* na kadhalika walikuwa kwa kweli nasikitika na hata kama watakuwa wanania katika vyombo vya habari, ninasema mambo yao hayakuwa mazuri hata kidogo. Watu wamebambikwa kesi za uongo na kweli watu wamewekwa *detention* za uongo na kweli. Kwa kweli ni matatizo ambayo yapo na ninadhani hayawezi yakakimbia isipokuwa namuomba Mheshimiwa Waziri Mwapachu haya mambo wajaribu kuyatazama.

Sasa nikienda harakaharaka ...

**MBUNGE FULANI:** Umemaliza!

**MHE. BALOZI HAMIS S. KAGASHEKI:** Nimemaliza eeh!

**MBUNGE FULANI:** Kengele haijalia.

**MHE. BALOZI HAMIS S. KAGASHEKI:** Kengele haijalia lakini mbona mnaniamulia kama nimemaliza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kengele bado haijalia utapoteza muda wako, usisikilize mtu mwingine.

**MHE. BALOZI HAMIS S. KAGASHEKI:** Labda nazungumza vibaya.

Nikiendelea upande wa *Science and Technology*, maana nakwenda haraka bila mpangilio, kwa kweli nadhani Mheshimiwa Rais amezungumza mengi lakini ni eneo ambalo mimi nadhani Serikali lazima ichukue *a deliberate decision* ya kusema kwamba wana *strengthen science and technology...*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mdogo, naomba nisichukue muda mwingi sana kuwapongeza viongozi waliopata nafasi lakini nizungumze tu kwa kifupi kwamba kuongoza ni kuonyesha njia na iwapo wenzako watakuamini wakakuchagua kwamba uwaongoze ina maana wameona kwamba una uwezo. Kwa hiyo,

naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais, niwapongeze na wengine wote ambao wamepata nafasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nirudi kwa wananchi wangu wa Jimbo la Same Mashariki. Kwanza, nianze kwa Wajumbe wa Jimbo la Same Mashariki kwa kuniona kwamba nina uwezo wakanipa kura nikaongoza na wananchi wakanichagua kwa kura ambazo zilitosha, zilikuwa nydingi na leo kiti nilichokikalia siyo changu ni cha Jimbo la Same Mashariki. Nawashukuru sana wananchi wa Same Mashariki kwa kiniamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niangalie hotuba ya Mheshimiwa Rais tofauti kidogo. Mimi naomba Wabunge wa Majimbo tuone kwamba Mheshimiwa Rais ametusaidia sisi zaidi ambao tuna dhamana ya wananchi kwa sababu mwelekeo wake anataka maisha bora kwa wananchi na sisi Wabunge ambao tumechaguliwa na wananchi kazi yetu kubwa ni kuhamasisha maendeleo ya wananchi, kupigania haki za wananchi. Kwa hiyo, kwa mwendo anaokwenda Mheshimiwa Rais anatusaidia sana sisi ambao mwaka 2010 tutakuwa tunaulizwa maswali mengi na tutasutwa lakini katika mwendo huu ina maana atatupunguzia sana kusutwa na kuulizwa maswali mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie upande wa kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo na tumekuwa tunahubiri kilimo katika Bunge hili tangu mimi nimeingia Bunge hili mwaka 2000 lakini hatujasonga hata hatua moja ya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naona kuna kitu fulani ambacho bado tunakosea. Kwanza, mfano mimi katika Jimbo langu la Same Mashariki nina Kata 10 ambazo ni za Milimani, nina Kata 4 ambazo ni za Tambarare. Wananchi wa milimani wanalima tangawizi, iliki, ndizi na kadhalika na wanalima kwa bidii kwelikweli. Wananchi wa tambarare wanalima mpunga, mpunga wa Same Mashariki, sehemu za Tambarare unakaribiakaribia mchele wa Mbeya, una harufu nzuri sana lakini tatizo kubwa ni kwamba barabara kwenye Jimbo langu hakuna. Kule kuna kitu kinaitwa njia na huwezi kuitisha malori makubwa kwenye njia hasa milimani. Kwa hiyo, wananchi wa Same Mashariki wa Milimani hata wakijitahidi kulima kiasi gani mazao hayafiki kwenye masoko makubwa. Kwa hiyo, wanakuwa hawapati kipato kizuri, mazao yanaharibika kama ni mboga, nyanya, vitunguu vinaoza kwa hiyo kilimo hakiwanufaishi wananchi wa Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee na Wizara ya Miundombinu kuitia Serikali. Mheshimiwa Rais alipofika Jimboni kwangu aliwaahidi wananchi tena kwa nguvu zake zote kwamba atakapoingia madarakani jambo la kwanza ataboresha barabara za Milimani Same Mashariki na tambarare ili mazao ya wananchi yafike kwenye masoko makubwa. Alipokuwa anatuhutubia hapa Dodoma alitilia mkazo kutimiza ahadi akiogopa kusutwa mwaka 2010. Sasa ninaomba Wizara ya Miundombinu, Rais alipoahidi inabidi Wizara hii itilie mkazo wa kutekeleza ahadi zake. Aliahidi na mimi nitawakumbusha kila siku hapa Bungeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafurahia sana Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya ya Serikali ya Awamu ya nne. Sasa na sisi Wabunge ambao tuna wananchi ambao

wanatudai, Wabunge wa Majimbo na sisi tunakuja na kasi hiyohiyo na ari hiyohiyo ya kutaka maendeleo ya wananchi tukutane katikati na Serikali. Serikali inapokuja na Ari Mpya na Nguvu Mpya na Kasi Mpya tunafarijika na sisi tunakuja hivyohivyo tukifika katikati tuchukue kutoka Serikalini tupelekee wananchi. Kwa hiyo tunaomba tuwaambie kwamba tutawaungeni mkono na hiyo ari mpya mliyokuja nayo ili maisha bora yapatikane kwa wananchi wote kwa sababu inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatozo limejitokeza. Ni kweli tumepata chakula cha njaa. Chakula cha njaa kimefika Jimboni Kwangu, Jimbo la Same Mashariki, Makao Makuu ya Jimbo. Lakini bado ninaomba Serikali ifanye usambazaji mzuri kwa sababu chakula kile hakikufika kwenye Kata, Makao Makuu ya Jimbo na Kata zangu zilizoko milimani ni mbali sana. Sasa ukimwambia mtu ambaye ana njaa kutoka Mtii, Bombo, Kirangare, Vunta umwombie aende Ndungu na ina maana kwa sababu hakuna usafiri atembee kwa saa 5 kwenda kufuata mahindi kisha abebe hayo mahindi kichwani, naomba Serikali itusaidie kufikisha chakula cha njaa kwenye kata kule ambako kuna matatizo ya njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, japo namalizia lakini naomba nikupongeze sana wewe kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na Mheshimiwa Samuel John Sitta kuwa Spika wa Bunge letu. Naomba nimhakikishie kabisa kwamba Mama Anne Makinda tunamfahamu ana uwezo mkubwa na ana uwezo wa kuchukua nafasi ya Uspika mwaka 2010 ikiwa Spika aliyepo hatagombea. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza kuzungumza rasmi humu ndani, napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Newala ambao walinchagua kwa kura nyingi na kwa kishindo kuwa Mbunge wao kipindi cha miaka mitano ijayo. Nawashukuru sana wapiga kura wangu hasa wanawake, debe nililopigwa na akinamama lazima niseme hapa ili waliko wasikie. Pia vijana na wazazi wenzangu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu ya muda, nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa katuongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao tumepewa dhamana ya kuwawakilisha wananchi katika kipindi cha miaka mitano ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka nigosie suala la umoja wa Kitaifa. Nafikiri watu wengi wamechangia lakini mimi nina mambo mawili kuhusu hilo na nitayasema kwa kifupi. Katika kila nchi utakayokwenda kitu kinachojenga *National Unity*, kinachowafanya watu wajisikie kuwa Taifa moja, jambo mojawapo ni

sherehe za Kitaifa (*National Day*). Katika nchi yetu tume-water down *National day*. Sisi tulipokuwa vijana, wakati tunasoma mara baada ya uhuru, ukisikia tarehe 9 Desemba, Mkuu wa Mkoa anakagua gwaride, DC anakagua gwaride, nchi nzima kunakuwa na vuguvugu kwamba leo ni siku ambayo Watanzania wamejitawala. Nikuuilizeni Wabunge wenzangu sijui mnakotoka wenzangu, *National Day* siku hizi unaambiwa sherehe imefanyika Kimkoa katika Kijiji fulani. Mimi naomba Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo masuala ya sherehe za Kitaifa yako huko, ilitazame suala hili upya. *National Day* iwe ni *National Day*. Tunapokuwa tunapumzika tuwe tuna mambo ambayo nchi nzima tumefanya, turudi tulikotoka mara baada ya uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linalofanya watu wajisikie kuwa wamoja ni shughuli za michezo kama Taifa *Cup* ya *Netball*, ya wavulana imerudi mwaka jana. Mimi naomba sana haya mashindano ya Kitaifa yanayokusanya vijana kutoka Mikoa mbalimbali tuyafufue. Nashukuru watu wa mpira wameanza mwaka jana na nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza vijana wangu wa Mtwara waliingia fainali kombe la Taifa, Mbeya wakaponea chupuchupu lakini tunafanya mazoezi tutaonana mwakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, nizungumzie juu ya tatizo la maji katika Wilaya yangu ya Newala. Wote wasomi humu ndani, Newala na Tandahimba sisi tunaitwa Makonde *Plateau*, *What is a plateau? A raised flat piece of land*, ardhi iliyonyanyuka ambayo juu ipo *flat*, ndivyo ilivyo Newala na Tandahimba. Kwa hiyo, wenzangu katika Mikoa mingine mnapozungumza habari za kuchimba maji visima vifupi Newala na Tandahimba hiyo *concept* haipo kwa sababu ili uchimbe kwenye *plateau* uje ukutane na maji sijui uende kilomita ngapi chini. Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu inasema miaka mitano ijayo malengo, upatikanaji wa maji tufike asilimia sitini na tano. Nimesoma katika baadhi ya Mikoa, Vijijini wameshafika asilimia hamsini na tatu. Upatikanaji wa maji Newala na Tandahimba ni asilimia ishirini na mbili. Kwa hiyo mnawea kuona tuko nyuma kiasi gani juu ya upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Rais alipokuja alisema nichagueni mimi niwe Rais, mchagueni Mkuchika awe Mbunge wenu mimi na ye ye tutashirikiana kupunguza tatizo la maji Newala. Sasa tumepata, Mheshimiwa Rais kapata, Mkuchika nimepata, watu wa Newala wanasubiri kusikiliza utekelezaji kama tulivyowaahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Newala zamani tulipogundua tatizo la maji, Newala *District Council*, katika mwaka 1953 ilianzisha Kampuni inayoitwa Makonde *Water Corporation*. Ndani kulikuwa na *element* ya uchangiaji, maji yakawa yanatoka ndani ya Wilaya kiwango cha kuridhisha, baadaye Serikali ikasema hakuna kuchangia maji. Tulivyoacha kuchangia maji, maji hayapatikani. *UNICEF* walifanya *research*, tufanyeje watu wa Newala ili muweze kupata maji ya kutosha. 97% ya watu wakasema ni afadhali tuchangie maji yawe yanapatikana kila siku kuliko kutwambia maji bure lakini hayapatikani.

Naomba sana Wizara ya Maji iimarishe Bodi ya Maji ya Makondeko, mtubakishe kama tulivyo Newala na Tandahimba. Maji yale ya Mitema yanafika Mtwara Vijijini,

tunaomba Bodi ibaki moja *intact*. Yalikuwepo mawazo Tandahimba pawe na Bodi, Newala Bodi na Mtwara Vijijini Bodi ya Maji, lakini vyanzo vyote vya maji viro Wilaya moja. Mimi nafikiri mtuache kama tulivyokuwa enzi za Makonde *Water Corporation*, tukae mahali pamoja Newala, Tandahimba na Mtwara Vijijini, tuzungumze uzalishaji wa maji, tuzungumze habari ya namna ya kugawana maji. Nadhani tukifanya hivyo tutakwenda vizuri. Mitambo ya Mkunya imechoka, inahitaji ukarabati, watafiti walikuja....

### **WABUNGE FULANI:** Enhee?

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mitambo ya maji tunayokunywa Newala inatoka sehemu inaitwa Mkunya. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nimeeleweka. Hayo ni majina ya Mtwara. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo la maji, sasa nizungumzie habari ya kilimo kwani muda umekuwa mfupi. Tuna tatizo la korosho, msimu ukifika wanunuza wanatubabaisha, tunaomba mtusaidie kuimarisha ushirika. Juzi nilizungumzia soko la muhogo. Narudia tena, nilizungumza katika semina, leo nasema hapa ndani, tuna mihogo Mtwara ambayo haina soko, tusaidieni watu wa Wizara. Siku hizi mihogo inasindikwa na unaweza ukai-*pack*, unga wa muhogo Dar es Salaam ni almasi. Tunaomba tusaidiwe ili tuwanusuru wenzetu amba wana matatizo ya njaa. Pia Newala tunalima soya lakini haina wanunuza. Mbunge mmoja Bunge lililopita aliuliza humu ndani, soya inayotumika nchi hii inapatikanaje. Akaambiwa *ninety percent* inaagizwa kutoka nje, inayozalishwa humu ndani *is only ten percent*. Newala tunalima soya lakini wanunuza hawaii kununua, kwa hiyo tunaomba tusaidiwe katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nizungumzie kuhusu elimu. Mimi kama Mwalimu nitafanya makosa kutozungumzia elimu. Nataka niipongeze Serikali kwa mpango ule wa MMEM, tumeufanya vizuri na nataka niwapongeze wananchi wa Newala kwa sababu Wilaya iliyokuwa bora katika utekelezaji wa MMEM ilikuwa Newala ndio maana sherehe za Kitaifa zikafanyika Newala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikumbushe shida ya Walimu katika Mikoa yetu ambayo ipo pembezoni. Lakini naomba sana Wizara ya Elimu, lipo tatizo tunapowaajiri Walimu wa shule za msingi. Kibali kinatoka Utumishi, wanaleta Halmashauri, Walimu wanaajiriwa, wakishaajiriwa *you can imagine first appointment* Mwalimu anafundisha miezi saba hajapata mshahara, *why should it happen?* Kibali kimetoka, Halmashauri *ime-respond* kwamba tumeshaajiri, wanakaaje miezi saba hajapata mshahara? Mimi naomba hili jambo litazamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumza habari ya MMES na kwenye semina tulisema, tunaomba fedha za MMES ziende *straight* kwenye *site* inapoengwa shule, habari ya kupeleka fedha shule sijui Mlezi iliyopo kilomita mia moja

na ishirini, mwenyewe Mkuu wa Shule hiyo Mlezi hata gari la shule hana. Naomba fedha ziende *straight* pale kwenye *site* wanapojenga shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda umekwisha, naomba kusositiza, Serikali ilikwishaahidi kutoa ruzuku katika shule za *private*. Sisi Newala kule tunayo shule nzuri kabisa ya Kitangali, *owned by Newala Development Foundation*. Tuliahidiwa shilingi elfu kumi kila kila mwanafunzi, bajeti ya mwaka juzi hazikutoka, bajeti ya mwaka jana hazikutoka, tunaomba bajeti inayokuja fedha hizo ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimalizie kuhusu uhaba wa watumishi katika Mikoa ya pembezoni. Naomba sana Waheshimiwa Mawaziri maana hili si la Wizara moja tu. Kuna Mikoa ina watumishi mpaka hawana nafasi, wanachangia ofisi lakini vile vile kuna Mikoa ambayo hatuna watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe umefika. Baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais.

Awali ya yote, naomba nianze kwa kutoa pongezi kwa viongozi wote wa Kitaifa kuanzia Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar na Waheshimiwa Mawaziri kwa kuchaguliwa na baadaye kwa wengine kuteuliwa kushika nafasi walizonazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wa kimbunga ambao kwa kweli hata Wapinzani wamekubali kwamba kweli CCM ni nambari moja. Katika ushindi huo huo, naomba nichukue nafasi hii nitoe shukrani za dhati kabisa kwa wananchi wa Jimbo la Msalala ambao walionyesha imani kubwa kabisa kwangu kuanzia kwenye hatua za awali za kura za maoni kama wanachama wa Chama cha Mapinduzi, lakini baadaye kwa ujumla wao kama wananchi wa Jimbo la Msalala kunichagua kwa kura nyingi kabisa kuwa Mbunge wao wa Jimbo la Msalala. Nawashukuru sana na kama nilivyokuwa nikiwaahidi wakati wa kampeni nitajitahidi kuwawakilisha kwa uwezo wangu wote na bidii kabisa kuhakikisha kwamba kilio chao kinasikika hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwanza naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Hotuba hii ni hotuba ambayo imeandaliwa kwa ufanisi mkubwa kabisa ina *coverage* kubwa sana, kadhalika imewasilishwa kwa umahiri kabisa. Kwa kweli nimefurahi sana na naiunga mkono kwa asilimia zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzungumzia hotuba ile, ningependa nigosie suala la njaa. Kwanza kwa sababu kwetu sisi watu wa Shinyanga suala la njaa kwa kweli lina sura tofauti kabisa pengine na maeneo mengine. Hili suala limezungumzwa sana na

wachangiaji wengi, lakini mimi nilikuwa naomba sana Wizara inayohusika hasa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kitengo cha Maafa), kishughulikie kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka jana nimekuwa nikiwasiliana na *DC* wangu chakula hakijafika. Sasa tujiulize Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea Shinyanga tarehe 4 –5/02/2006, mpaka sasa hivi ni zaidi ya siku saba zimepita na wananchi wa Kishapu na sehemu zingine walimtaarifu kabisa kwamba wanakula mashudu wakati huo, maana yake ni kwamba walikuwa wameanza kula vitu ambavyo haviliwi na mtu anakula kitu ambacho hakiliwi huwa ni kiashiria kuwa yuko kwenye hatua za mwisho kabisa za uhai wake. Sasa kama walikuwa wanakula mashudu tarehe 5/02/2006 mpaka sasa hivi sijui kama hayo mashudu bado yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapigiwa simu watu wanalia, leo hii mchana nimepigiwa simu na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya anasema watu wamefurika nyumbani kwake na amelazimika kuwachotea sehemu ya akiba yake ya chakula waende kujipatia chakula. *DC* naongea naye anasema hajapata maelekezo yoyote kutoka kwa *RAS*. Nimeongea na *RAS* jana anasema hajapata maelekezo yoyote kutoka Wizarani kwamba ni kiasi gani cha chakula kinatakiwa kiende Kahama na pesa za kupelekea chakula hicho. Sasa naomba pamoja na kwamba huku Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rais tunaonekana na tunajitahidi kwa kweli kama Serikali inabidi kuwa na *speed* kubwa ya kukabiliana na tatizo hili, lakini inaonekana katika *system* bado kuna baadhi ya wenzetu watendaji ambao hawajawa tayari kuendana na *speed* ya sasa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tujitahidi kabisa katika siku chache sana chakula kifike maeneo hayo, hali ni mbaya sana. Ninapigiwa simu na Walimu wa shule za msingi wanasema watoto wanaanguka shulen, wakiulizwa wanasema kwamba hawajala kwa siku tatu. Mwalimu mmoja jana asubuhi kanipigia simu anasema siku ya Ijumaa kuna watoto watatu alikwenda kuwanywesha uji nyumbani kwake. Kwa hiyo, hali ni mbaya sana. Naomba sana suala hilo litazamwe na Serikali kwa mtazamo huo kwamba tuko kwenye *critical stage* ambayo kwa kweli hatuna fursa hata siku nne, tano kuanza kujandaa, naomba hatua za dharura zichukuliwe. Naamini kwamba kuna mgawo, nimeshapata hata nakala, tani elfu moja na mia moja na ishirini na moja tutapelekewa Wilaya ya Kahama lakini mpaka sasa hivi hazijafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia suala la chakula, naomba nizungumzie suala la madini na Mikataba inayohusu madini. Suala hili limekuwa likizungumzwa mara kwa mara na Waheshimiwa Wabunge na hata wananchi wanazungumza kuhusu jambo hilo. Manung'unico yapo na wananchi wa Jimbo la Msalala wamenitura nije niseme hapa kwamba, kwanza wanaona kabisa hali ilivyo ya utekelezaji wa uchimbaji, inaonyesha sura ya kutonufaika vizuri. Kwa bahati mbaya sana hata wakati wa kampeni sisi wagombea wa CCM tulipata shida sana kwa sababu hata wenzetu wa Upinzani walikuwa wanafika, hakuna mgombea wa Upinzani wa Urais ambaye alikuwa *serious* anataka kuwa Rais ambaye hakufika Kakola ambacho ni Kimji kilichopo kwenye mgodi wa Bulyanghulu. Mbewe amefika, Mtikila amefika na wote hawa wakifika wanakuja kuwaambia watu kwamba, ninyi Wasukuma mlishaonekana

*nduhutabu, nduhutabhu* maana yake *no problem* kwa Kiingereza yaani hakuna shida kwa Kiswahili. Nasema wenzenu kule Wamasai, *National Parks* zao wanapewa asilimia saba ya mapato yanayopatikana kutokana na utalii, lakini ninyi hampati kitu. Sasa sisi mkituweka madarakani, naomba tuwaambie kuna *percent* fulani ambayo inapaswa iletwe kama wanavyopata wenzetu wa sekta nyingine lakini haifanywi hivyo na sisi tutahakikisha hayo. Wananchi wanaona kabisa kwamba sisi hatuwatendei haki na wote wanakuwa *against CCM*. Kwa hiyo, naomba tujaribu kuangalia Mikataba hii iwe ya wazi ili wananchi wajue kama wanatakiwa kunufaika kwa kiasi fulani ieleweweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna mambo ya uharibifu wa mazingira yanayotokana na uchimbaji wa madini. Kwa mfano, mgodi wa Bulyanghulu ni mgodi ambaao unachimbwa chini kwa chini. Lile eneo la umiliki kwa sasa hivi wanavyovinjari kule chini ya ardhi wamekwenda zaidi ya kilomita saba. Sasa unakuta kwamba zile kilomita saba wanakwenda chini kwa chini wanafika mpaka kwenye maeneo ambayo hawayamiliki kwa mujibu wa kipimo kilichopo huku juu lakini pia hilo shimo linalotokea pale ni kwamba ile ardhi inabakia tete, kukitokea tetemeko la ardhi kidogo tu ina-collapse kwa sababu kule chini kuna shimo la kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna hali ya uharibifu wa barabara. Sasa yote haya tunavyoona sisi wananchi tunaona kabisa kwamba hatufaidiki na shughuli hizi zinazofanyika kwa kiasi kinachotakiwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali, kilio chetu mkisikie, pitieni upya Mikataba hii na sisi wananchi mtushirikishe. Sisi tunaotoka kwenye maeneo ya migodi tunatakiwa na sisi kama wenzetu wanavyofaidika na simba wao kadhalika na sisi angalau tunufaike na vumbi letu la dhahabu. Watu wanunung'unika sana kuona vumbi linasombwa linapelekwa nje ya nchi likisababisha uharibifu wa barabara kwenye maeneo yanakopita maroli yale, lakini hakuna ukarabati wa barabara unaofanyika, hakuna shughuli nyingine zozote za maendeleo ya jamii ambazo zinafanyika, wanajaribu kidogo kidogo lakini hatujui kama hicho tunachopata ndio wanachotakiwa kutoa. Kwa hiyo naomba sana Serikali mtusaidie kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, ningependa kuchangia kuhusu suala la mapato ya Serikali. Kwa mujibu wa hali ya sasa na Ilani yetu ya CCM kuna mambo mengi sana tunayopaswa kuyatekeleza. Naomba Wizara ya Fedha ijipange kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais na ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makofî*)

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nami pia ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu, naomba nianze kwa ruhusa yako kutoa shukrani. Shukrani zangu za mwanzo na za dhafi kabisa ni kwa Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kuwepo hadi siku ya leo hasa nikikumbuka hapo mwishoni mwa mwaka 2004 nilihuksika katika ajali mbaya sana, wenzangu watatu walipoteza maisha.

**WABUNGE FULANI:** Pole.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Ahsanteni.

Shukrani zangu za pili, ni kwa wajumbe wa ule Mkutano Mkuu katika Wilaya yangu ya Hai kunitfea katika kura za maoni na hatimaye Halmashauri Kuu kunipitisha. Halikadhalika, niwashukuru sana wananchi wa Hai kwa ujumla wao kwa ujasiri mkubwa kabisa na wa hali ya juu walioonyesha siku ya tarehe 14/12/2005 kwa kuweza kukatungua kale kahelikopta kalikokuwa kanatusumbua sumbu. Nawapongeza sana kwa dhati kabisa kwa huo ujasiri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu za tatu, ni kuwashukuru wananchi wa Tanzania kwa ujumla wao kwa kuweza kututeua Wabunge wengi wa CCM pia na hao wachache walioweza kufika hapa na kuendesa ule uchaguzi katika hali ya amani kabisa, nchi ilikuwa imetulia vizuri mno. Nawapongeza sana Watanzania wote kwa ujumla. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa ushindi wake ambao na sisi tulijumuika pamoja. Nampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa kuteua Baraza la Mawaziri na kwa kumteua Mheshimiwa Edward Lowassa, nasi tukamthibitisha. Niwapongeze pia wote walioteuliwa katika nyadhifa mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge wenzangu nimeshawapongeza kwa kuwashukuru wale wananchi waliotuchagua mpaka tupo mahali hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa katika Jimbo lake na wewe Naibu Spika kwa kuchaguliwa katika Jimbo lako, lakini pia niwapongezeni kwa sisi kuwachagua kama viongozi wetu wakuu ili mtuongoze hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais imesheheni na imeja mambo yote ambayo Watanzania wote tungeyatarajia. Sidhani kama tunayo mengi zaidi ya kuongezea pale, la zaidi ni kuipongeza na kuiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba tu nichangie katika maeneo machache ambayo ningejikita zaidi katika Jimbo langu la Hai. Hai ni Wilaya mojawapo katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro. Nikianza katika upande wa elimu, Kilimanjaro imekuwa ikitsemwasemwa kwamba labda imeendelea kielimu hata na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge nimewasikia wakisema hivyo, lakini ningeomba tukumbuke kwamba Kilimanjaro ni eneo dogo lakini wakazi ni wengi. Kwa hiyo tunao upungufu mkubwa wa shule, tusiwe na ile dhana kwamba Kilimanjaro bado ina shule nyingi mno, sisi tuna upungufu mkubwa kabisa hususan katika Jimbo langu la Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea katika upande wa elimu ningeomba basi kwa kushirikiana na Serikali tuweze kuboresha elimu kuanzia msingi hadi vyuo vikuu kwa Taifa zima tukielewa kwamba elimu ndio ufunguo wa maisha na ndiyo tutaweza kuyafikia yale maendeleo tunayoyatarajia kwa ujumla. Ningeomba pia Wizara inayohusika na Elimu, ingerudisha elimu ya watu wazima kwa kiwango kikubwa sana. Sasa hivi natumaini sio katika Jimbo langu tu, ni kwa nchi yetu nzima ya Tanzania, elimu ya watu wazima ni muhimu sana na tunaposema elimu ya watu wazima sio wazee tu hata wale ambao wameshafikia umri wa miaka thelathini lakini hawakubahatika kupata elimu. Kwa hiyo, ningeomba turidishe elimu ya watu wazima. Natumaini Waheshimiwa

Wabunge wenzangu watakuwa mashahidi. Siku ya uchaguzi kulikuwa na tatizo kubwa la baadhi ya vituo kuchelewa sana lakini ukitafuta kiini unakuta ni kwa sababu ya watu kutokujua kusoma na kuandika. Kwa hiyo ningeomba sana turejeshe ile elimu ya watu wazima. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie upande wa kilimo. Tumekuwa tukiimba kwamba kilimo ndio uti wa mgongo, kwa hiyo ningeomba sasa tukivalie njuga zaidi. Tunazungumzia suala la njaa hapa, hata mimi kwangu kule eneo la tambarare njaa ipo na kwa jirani zangu Siha njaa ipo, kwa hiyo ningeomba sasa kilimo tukiangalie zaidi. Sasa hivi hili tatizo la njaa ni la muda, naomba sasa tuangalie jinsi gani tupanue hiki kilimo ili tuachane kabisa na hii biashara ya kusema kuna njaa. Mwenyezi Mungu katupa nchi nzuri, ina mabonde, milima, mito na maji kwa wingi kabisa, sasa ningeomba tukae, tujipange ili tuweze kutumia hivi tulivyonavyo. Wenzangu wameshachangia sana kuhusu hayo maziwa na mito jinsi ya kutumia. Ninachoomba ni kwamba, tujipange ili tuweze kuvitumia hivi tulivyojaliwa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano eneo langu la Wilaya ya Hai sehemu za tambarare, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea kule majuzi nami nikiwa pamoja naye pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wengine, eneo lile tukilitumia vizuri ni kwamba tutajitosheleza kwa chakula katika Wilaya nzima ya Hai na maeneo ya jirani hata Mikoa ya jirani tutaweza kuilisha kwani Mungu ametujaalia eneo zuri na maji yapo kwa wingi, ni kiasi cha kujipanga na kufanya utaratibu mzuri wa kuyatumia. Naomba pia tujipange vizuri katika kilimo ili tuweze kuachana na hii dhana ya kwamba tuna njaa. Kwa wengine inashangaza kidogo kusema kwamba Tanzania tuna njaa wakati kila kitu tunacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichangie kuhusu ufugaji kwani katika Wilaya yangu pia ufugaji upo kwa wingi kabisa. Inasikitisha tunaposema ng'ombe mzima sasa hivi anauzwa shilingi elfu kumi na tano mpaka elfu thelathini. Ningeomba tufanye elimu zaidi kwa wafugaji wetu. Tunapowashawishi kuuza mifugo, hivi tunawashawishi tu wauze au wapate faida. Tungejenga mazingira ambayo tunapowaambia wauze, wanaiza zile fedha wanazozipata wanazifanyia kitu cha maana na hapo ningeomba kwamba tuweke maeneo vizuri ili tuepukane na migogoro katika nchi yetu kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda unakwenda haraka, ningeomba pia nichangie katika upande wa mashamba yaliyobinafsishwa. Zamani kulikuwa na mashamba hususan katika Wilaya yangu ya Hai. Yale mashamba utaratibu uliofanyika ni kwamba yalikabidhiwa kwa Vyama vya Msingi. Kwa maoni yangu ni kwamba ningeomba Wizara inayohusika, natumaini ni ya Ushirika, yale mashamba yawe chini ya Serikali za Vijiji kwani kinachopatikana kutoka kwa wawekezaji kinapofika kwenye Vyama vya Msingi sana sana hakioneckani. Vyama vya Msingi havielezi wananchi kwa ujumla na wanachama wa Vyama vya Msingi sio wanakijiji wote ni wachache tu ambao wanawenza kuvizua kahawa vile Vyama vya Msingi. Kwa hiyo ningeomba hilo suala tushauriane na kushirikiana na Wizara husika tuweze kufanya kitu ambacho kitakuwa na tija kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo katika zao la kahawa, tutashirikiana na Wizara husika kabisa katika kukipanua na kuwa na kilimo cha kisasa zaidi kwenye zao letu la kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais iliyosheheni mambo yote ambayo tungetarajia kuyasema na tunayoyatarajia kama Watanzania. Ningombwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu tujitume na tujitahidi kwenda na spidi ambayo Serikali yetu inakwenda nayo ili yale matarajio ya wananchi yawezekufikiwa. Naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii ya Waziri Mkuu juu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo naiunga mkono moja kwa moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kwa kifupi kabisa nitumie nafasi hii kutoa pongezi na shukrani. Kwanzaa kabisa nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Dr. Shein kwa ushindi wa kihistoria. (*Makofî*)

Pili, nimpongeze Mheshimiwa Dr. Amani Abeid Karume kwa ushindi wa heshima kule Zanzibar. Kuvuma kwake kule Zanzibar kumetusaidia sana kuvuma pia kule Arusha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimpe hongera kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili kwa kura za heshima kabisa pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Edward Lowassa nimpe pongezi kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wetu. Hongera Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa hongereni kwa kuteuliwa. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge wenzangu poleni na hongereni kwa kufika hapa Bungeni. Naelewa halikuwa tanuru rahisi la kupita, lakini tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ametuwezesha sisi sote kufika hapa. (*Makofî*)

Nitumie pia nafasi hii kuwashukuru wananchi na wapiga kura wangu wa Arusha Mjini, Makao Makuu ya Afrika Mashariki kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao kwa kipindi kingine cha miaka 5. Yamesemwa mengi lakini tumehakikisha kwamba Arusha inaendelea kubaki kuwa ngome ya CCM. Ushindi huo nilioupata umeniwezesha mimi jana kuchaguliwa na Wabunge wenzangu wa CCM kuwa Mjumbe wa NEC kwa kura nyingi ambazo sikuzitegemea. Wote ninyi wananchi wa Arusha, Waheshimiwa Wabunge wa CCM nawashukuru tena sana kwa kunichagua na nawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa uwezo wote alionijalia Mwenyezi Mungu. (*Makofî*)

Mwisho, nawatakieni ninyi nyote kuanzia Mheshimiwa Rais, Makamu, Spika, Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote mpaka ninyi nyote hapa

Waheshimiwa Wabunge afya njema na baraka za Mwenyezi Mungu ili tuweze kuyamudu majukumu tulionayo mbele yetu kwa njia ambayo itawaridhisha walio tuleta hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye hoja tulionayo mbele yetu. Ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninukuu sehemu hiyo. "Hotuba ya Rais ilikuwa nzito inaonyesha umakini, umahiri na yeny upeo wa hali ya juu tena iliyowasilishwa kwa ustadi na ufundi wa kipekee kabisa". Mwishiwa kunukuu. Kwa mara ya kwanza kwenye historia ya nchi hii Rais alihutubia Bunge kutumia vyombo na nyenzo za kisasa *teleprompter*. Haijapata kutokeea !!!!

Mheshimiwa Naibu Spika, mategemeo na matumaini ya wananchi juu ya awamu hii ya nne ni makubwa tena makubwa sana, sijapata kuona katika historia ya nchi hii. Mategemeo na matumaini na imani ya wananchi kufikia kiwango hicho. Hii kwa upande mmoja ina hatari zake na kwa upande mwingine ni changamoto pekee na ya kihistoria. Wananchi walimtzama na kumsikiliza Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na ahadi alizotoa na chama anachokiwakilisha wakahamasika kuwa na mategemeo hayo na matumaini hayo. Sasa kazi yetu, kazi ya Serikali hii ni kuhakikisha kuwa hatuwaangushi wananchi hao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaelekeza nguvu zangu katika sehemu mbili ambazo tukianza kuzifanyia kazi nina kila imani kwamba tutaendelea kuwapa nguvu wananchi kwamba kweli Serikali hii imeanza kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Nianze na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo sasa hivi, watu zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wa nchi yetu wako kwenye sekta hii ya kilimo na wanalima zaidi ya hekta milioni 6. Nchi yetu hii ina hekta zisizopungua 84 milioni. Kati ya hizo zinazolimika ni 44 milioni ni hekta milioni 6 tu ndizo ambazo zinazolimwa sasa hivi na zinalimwa kwa kilimo cha kujikimu sio kilimo cha biashara. Ndiyo sababu tunakuwa na matatizo ya njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto yetu kubwa ni kugeuza kilimo hicho kutoka kwenye kilimo cha kujikimu na kuwa kilimo cha kibiashara. Maana kilimo ni biashara. Popote duniani nchi zilizoendelea zimegeuza kilimo chao kutoka kilimo cha kujikimu na kukifanya kuwa kilimo cha biashara. Hiyo ni moja. Sasa tufanye kugeuza sekta hii itoke kwenye kilimo cha kujikimu iingie kwenye kilimo cha biashara, ni kubadilisha nyenzo wanazozitumia wakulima wetu. Sasa hivi wanatumia nyenzo za jembe la mkono, hii haiwezi katuondoa kwenye kilimo cha kujikimu. Lazima tuwawezeshe hawa wakulima waweze kutumia nyenzo za kisasa na njia sahihi ya kuwawezesha ni kuja na utaratibu wa kuwawezesha wakulima wangu wa Terati waondokane na kilimo cha jembe la mkono wawe na matrekta ili waingie kwenye kilimo cha kisasa. Kwa hiyo, mategemeo yangu ni kwamba kwenye bajeti inayokuja utaratibu wa *leasing arrangement* utakuwa umekamilishwa ili wakulima waweze kupata nyenzo hizi kwa mikopo ya nafuu kwenye bajeti hii inayokuja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia eneo la sekta ya nyumba kwa sababu muda unakwenda kasi. Sekta ya nyumba ni sekta nyingine ambayo tukiweka mkazo inaweza kutupeleka upesi sana kutoka kwenye uchumi unaokua kwa asilimia 6.7 kama ilivyo hivi sasa kufikia asilimia 10, ambayo tunataka kuwa nayo ili tuwaondoe wananchi wetu kwenye umaskini huu uliokithiri. Sasa sekta ya kilimo tufanye nini?

Hivi sasa nyumba zinazojengwa katika Taifa letu hazizidi 2,000 au 3,000 kwa mwaka. Kuna uhaba (*demand*) ya nyumba zisizopungua 200,000 kwa mwaka. Kwa nini nyumba hizi hajijengwi? Hajijengwi kwa sababu watu wanatumia *cash* kujenga nyumba za kuishi. Hamna uchumi wowote duniani ambapo watu wanajenga nyumba za kuishi kwa kutumia *cash*. Sasa tuje na mfumo ule wa kutoa *mortgage finance facilities* wa kuwawezesha wananchi kuweza kupata mikopo ya miaka 20 mpaka 30 ya kuweza kujenga nyumba zao za kuishi na za biashara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Magufuli nguvu yako huko ulipo kwenye Wizara hiyo ya Ardhi wekeza sio katika kuwaondoa wale wateja wako (*tenants*) wako wa nyumba zako za *National Housing Corporation* kama wale wa kwangu kule Ngarenaro na *Cuban Quarters*. Wawezeshe hao *tenants* wa *Cuban Quarters* Ngarenaro na Sekei pamoja wawze kuzinunua hizo nyumba zao na kuwageuzea wao kuwa *property owners* waingie kwenye hii ngazi ya *middle class* ambayo tunataka iongezeke katika Taifa letu. Maana yake bila ya kuwa na *middle class* ambayo inaongezeka tutaendelea hivi tulivyo hatutaweza kujiionda hapa tulipo lazima *middle class* yetu ipanuke na njia ya kuipanua ni kuwawezesha hawa kuwa na hizi *properties*. Kwa hiyo tuharakishe hiyo ili hawa wananchi kuweza kuzipata hizo nyumba wawze kuwa na hizi *properties* wawe kwenye *middle class*.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umekwisha nashukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Lakini kabla sijasema chochote kuhusiana na uchangiaji napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa Makamu wa Rais Mheshimiwa Ali Mohamed Shein, kwa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Ngoyai Lowassa. (*Makofî*)

Katika pongezi hizo hizo ziendelee kwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri nawe Mheshimiwa Naibu Spika na bila kumsahau Mheshimiwa Spika mwenyewe, hongereni sana kwa kuchaguliwa na kupewa nyadhifa hizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nitoe pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Mikumi kwa kuwa na imani nami na baada ya mapigano makali na vyama vitano vya Upinzani nikaibuka na ushindi mnono. (*Makofî*)

Kama walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote tunajua kwamba ushindi wa CCM Zanzibar ulichochea asilimia kadhaa ya kuongeza ushindi Tanzania Bara. Kwa hali hiyo, sina budi kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Wana-CCM

na wananchi wa Zanzibar pamoja na Wapinzani wa Tanzania Bara ambao baada ya ushindi wa Zanzibar waligeuka wakapigia CCM. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, napenda kwanza kabisa kuwaahidi wananchi wa Jimbo la Mikumi kwamba nitakuwa Mbunge muendelevu ambaye nitajali maslahi na maendeleo ya wananchi kadri ya ilani ya CCM ilivyoelekeza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitasema kwa kifupi kwa sababu mambo ni mengi. Mimi yangu kwanza nianze na suala la mpasuko Zanzibar. Mimi ni mara yangu ya kwanza kuwa Bungeni na sina uzoefu wa masuala ya ndani kabisa kuhusu mpasuko. Lakini rai ninayoitoa kwa ndugu zetu Wabunge wanaotoka Zanzibar ambao ninaamini wao ni kioo na mfano kwa wananchi wote waliobaki Zanzibar ambao sio Wabunge, kufuatana na uzoefu mfupi niliouona nikiwa Bungeni hapa atakapotoa mchango Mbunge wa kutoka CCM moyo unaanza kudunda kujua Mbunge wa kutoka *CUF* atajibu nini kwa sababu jazba inatawala na maneno, kwa kweli maneno hayo hayasaidii kuwa mfano mzuri kwa wananchi wetu waliobaki Zanzibar kama sisi humu ndani tunaanza kusigana maneno kwa jazba. Kwa hiyo, naomba kutoa rai ndugu zangu Watanzania wenzangu sisi ndio kioo cha wananchi Zanzibar na kama tutaanza kulumbana lumbana katika kauli hatuwasaidii kujenga amani na hii inatishia Muungano wetu siku za mbele, naomba hili m jitahidi kutuliza jazba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine labda nizungumze baadhi ya masuala ambayo yanatukera katika Jimbo la Mikumi. Kwa upande wa Kata mbili, Kata ya Uleling'ombe na Vidunda tatizo kubwa sana ni barabara. Ukienda Uleling'ombe ambayo ni mwendo wa kilomita kama 15 kutoka tambarare katika kijiji kinaitwa Mlunga kwa mguu unachukua masaa 8 kwa gari utachukua saa moja lakini barabara hiyo haijawahi kuonekana na nafikiri hakuna ambaye amekwishapita barabara kama ile kwa sababu ni barabara isiyokuwa na changarawe. Ni barabara ambayo ina mawe makubwa. Katika kampeni nimevunja *spring* za *Nissan Patrol* mara tatu kila nilipovunja zimevunjika mara mbili. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Mashishanga alifanya ziara mwaka jana alikaribia kushuka kwenye gari arudi kwa mguu. Kwa kifupi tunaomba Wizara ya Miundombinu itupie macho katika Kata hizo. Wanalima mazao ya vitungu swaumu, hiliki na kama barabara ingekuwa nzuri kwa sababu ni milimani hata uwezekano wa kulima kahawa upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine katika Jimbo letu liko katika Kata ya Mikumi nalo ni suala la maji. Kama nilivyoongea kwenye semina suala la maji ambapo wote tunajua maji ni uhai linaleta kero sana kwa wananchi wa Mikumi. Wote mnajua Mikumi pana *National Game Reserve*, kuna wageni wengi, kuna magari yanayobeba mizigo kutoka Dar es Salaam kupeleka Zambia na katika Ilani ya Uchaguzi kutakuwa na barabara ya lami inayotoka Mikumi kupitia Kilosa hadi Dumila. Hii italeta *traffic* kubwa zaidi na wageni wengi zaidi pale Mikumi. Tunaomba suala hili Wizara ya Maji ilitazame kwa makini na tunakuja kuomba msaada kwa Kampuni ya Maji ambayo imekuwa inaleta matatizo makubwa pale na kuwafanya wananchi wasiwe na imani kuchangia. Mheshimiwa Waziri Mkuu wa sasa hivi, Mheshimiwa Edward Lowassa alifanya ziara

mwaka jana alikuta sokomoko la ajabu ambalo mpaka sasa halijapata ufumbuzi tutaomba msaada liweze kutatuliwa.

La mwisho kwa vile muda ni mchache nizungumzie suala la uharibifu wa mazingira. Kati ya Mikumi na Kilosa kuna Kata tatu pale zimekuwa ni uwanja wa magombano kati ya wafugaji na wakulima kwa sababu wafugaji wanapeleka kunywesha mifugo kwenye vyanzo vya maji. Sasa ili mradi kwa kweli tumeona kwamba uharibifu wa mazingira madhara yake ni makubwa kupita kiasi kwa maana ya nishati, maji yanatakiwa kwa ajili ya kuendesha mitambo ya umeme lakini pale pale uharibifu wa misitu na kuleta ukame yote inatokana na uharibifu wa mazingira. Imefika wakati nafikiri Serikali ichukue hatua za makusudi na za lazima kupiga marufuku wafugaji kutembeza mifugo katika maeneo ya vyanzo vya maji na pengine hata kuanzisha jeshi la kulinda vyanzo vya maji vyote nchini ili tujinusuru katika matatizo yanayoweza kujitokeza huko mbele. Hifadhi za wanyama kuna maaskari kwa sababu ya umuhimu wa suala hili ninaona inastahili nalo kufikiriwa ulinzi wa vyanzo vya maji na misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho la mashamba makubwa yaliyokuwa ya watu binafsi zamani ambayo yameachwa ovyo ovyo hasa ya mikonge. Wananchi walikuwa wanafanya kazi kwenye maeneo yale walikuwa wameajiriwa lakini sasa mashamba yale yamebaki *idle*. Wafanyakazi hawa wamekaa miaka mingi hawakuwa kipindi kile na mahali pa kwenda kulima sasa mashamba haya yakiwa *idle* inabidi yatumiwe ama sivyo hawana mahali pa kulima. Ilikuwa ni jambo zuri la kuwawezesha wananchi amba ni wengi wamezaliana pale wamekuwa na wajukuu wakapewa maeneo yale wayamiliki kusudi waweze kujiendeze kimaisha katika mkakati wa kupunguza umaskini. Najua ni suala la sheria lakini.....(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais alioitoa tarehe 30 Desemba, 2005.

Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi mkubwa alioupata. Aidha, naendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kwa kuteuliwa na vile vile kupitishwa kwa kura za kishindo na Waheshimiwa Wabunge.

Nampongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Mawaziri, Manaibu Waziri pamoja na Wabunge wote kwa nafasi tulizonazo za kuwakilisha wananchi wetu katika kipindi cha miaka 5. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii ya pekee kwanza kwa kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Musoma Mjini. Maana wamenipa heshima ya pekee na ndiyo maana leo nimekuwepo katika jengo hili la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama mwakilishi wao. Nami nasema nitawakilisha pasipo kutegeea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza niweze kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli hotuba hii naamini imemgusa kila mtu, kila mmoja wetu amekubaliana nayo kwamba hii ndiyo dira pekee itakayotuondoa katika dimbwi la umaskini kwa maana ya maisha bora kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Mheshimiwa Rais wetu si suala la kutoa hotuba tu naamini utekelezaji wake sisi wote tumeanza kuuona. Ameanza kwa *style* ambayo amejaribu kutuonyesha njia kwamba ni namna gani sisi sote tunapaswa kwenda. Tumeshuhudia yeye mwenyewe ameamka amekwenda mahospitalini kujionea hali halisi, amekwenda mwenyewe katika Wizara mbalimbali amejionea hali halisi na kuzungumza matarajio yake na amekwenda hata katika masoko yetu. Kwa hiyo hii ni njia ambayo ametuonyesha kwamba kumbe sasa si wakati wa kukaa maofisini isipokuwa ni wakati wa kufanya kazi za wananchi. Nampongeza sana. (*Makofi*)

Lakini hata Mheshimiwa Waziri Mkuu naye amefuata nyayo ni hizo hizo. Tuliona tatizo la umeme lilipoanza hakuchelewa kufika katika maeneo yetu mbalimbali ya vyanzo kwa maana katika mabwawa yetu. Tumepata tatizo la njaa amekimbia katika maeneo yale nyeti na kuangalia. Hali kadhalika na hata Spika wetu kwa kweli naamini kila mmoja wetu anakubali kwamba ni Spika wa *Standard and Speed*. Hiyo ni changamoto ambayo sisi wote tunapewa kwa maana ya Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya mpaka wale viongozi wa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nafasi ni ndogo ebu na mimi niweze kuchangia kidogo katika yale maeneo ambayo nimeyaona. La kwanza kwa kuwa sasa ni jukumu la kila mmoja wetu aweze kutekeleza wajibu wake mimi ningeomba kabisa pasipokutegea kwa moyo wa ujasiri pale tutakopofika katika kipindi chetu cha bajeti ebu tuweze kuangalia wale wenzetu ambaao kile wanachokipata kwa kweli hakiwatoshelezi. Leo unapozungumza masuala ya Waheshimiwa Madiwani kupata shilingi 30,000 kwa mwezi na wao ndio wako kule kwenye Kata zetu kwa maana katika Majimbo yetu wanatusaidia kusukuma maendeleo kwa kweli haiwapi moyo. Kwa hiyo muda utakapofika itabidi tuliangalie kwanza. Lakini chini yao tena kuna wasaidizi wengine kule Wenyeviti wetu wa Mitaa na Vitongoji. Sisi tunafahamu kila jambo linapojitokeza aidha la kuchangisha au lolote la maendeleo wale ndio wa kwanza kusukuma. Ebu na wao ni vizuri tukaanza kuwaangalia angalia namna wanavyoweza kuwa wanapata walau maji ya kunywa pamoja na vitendea kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niweze kuchangia katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Nashukuru kwa juhudhi ambazo zimechukuliwa na kwa kweli nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu maana hata mimi Jimbo langu halikuwa na chakula lakini juzi aliweza kuniambia kwamba ametupatia tani 600. Lakini bado nasema hata hizo tani 600 ni ndogo kwa sababu zifuatazo.

Kwanza, ni kweli kwamba chakula tumekuwa tukikipeleka zaidi katika yale maeneo ya wakulima na safari hii hawakupata chakula. Lakini naomba nimwambie tu

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba sisi tulioko mjini ndio tumeathirika zaidi kwa sababu mbili. Kwanza wale wote waliokosa baada ya kuwa chakula kule hawakuvuna, wote wamekimbia mijini maana wanatarajia kwamba kule mjini ndipo watapata kazi. Sasa wamefika mijini kazi hakuna chakula hakuna. Kwa hiyo kutokana na sababu hiyo sasa hivi tuna shida kubwa sana ya chakula kwa maana kwamba watu wetu hawana chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sababu ya pili kabla ya njaa chakula kilikuwa kinauzwa kati ya shilingi 80 mpaka shilingi 120 kwa kilo. Sasa leo kipato cha huyo mwananchi wa mijini kiko pale pale, lakini chakula kinauzwa kati ya shilingi 350 na 400. Sasa ebu angalia hapo kimepanda zaidi ya mara nne. Kwa hiyo kutokana na sababu hizo ndiyo maana tunasema hata mijini tujue kwamba hali ya huko si nzuri kabisa inahitaji msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwenye Wizara ya Kazi hasa kuhusiana na suala la ajira. Tunashukuru kwamba viwanda sasa vipo vyta kutosha katika miji yetu lakini tatizo linakuja moja kwamba hata wale wafanyakazi ambao wamepata ajira mfano kama mimi katika mji wangu wa Musoma wanalipwa shilingi 1,850 kwa siku akiondoa gharama ya usafiri kwa maana ya daladala kwenda na kurudi ni shilingi 400 na anabakiwa na shilingi 1,450. Sasa 1,450 akiondoa chakula cha mchana anakwenda nyumbani na shilingi 1,000 ana familia zaidi ya watu 5. Ambapo ukiangalia fedha hizo ni chini hata ya kima cha chini cha mshahara. Kwa hiyo hili nalo ni tatizo ambalo wale watu tunadhani kwamba vile viwanda vinatusaidia lakini haviwasaidii sana. Kwa hiyo ni jukumu la Waziri wa Kazi aweze kuangalia kwamba na hili atashughulika nalo vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya muda naomba basi niingie kidogo kwenye sekta ya maliasili kwa maana ya Wizara ya Maliasili. Sisi watu ambao tulioko Kanda ya Ziwa na hata wale Wabunge wenzangu naamini vile vile watakubaliana nami tunao wavuvi ambao wamekuwa wakiuzia viwanda samaki. Lakini leo wale wote tukifanya tathmini wale waliokuwa wanafanya biashara hizo leo wote wanafilisika kwa maana kila aliyekuwa na fedha aliyejiingiza kwenye biashara ile ameishia kuishiwa fedha. Lakini ukija kuangalia sababu ni nini viwanda vyote vya Kanda ya Ziwa karibu vyote ni vya mtu mmoja ni mtoto wa binamu kiwanda ni cha mjomba, kingine ni cha baba mdogo. Kwa hiyo, matokeo yake sasa wanapanga bei wanayotaka kununulia samaki. Ndiyo maana nadhani kumekuwa na lile tatizo la watu kupeleka samaki nchi jirani kama mimi katika Musoma maana tuko mpakani wanapeleka Kenya na wanapofanya hivyo wanashikwa kwa sababu ni makosa. Lakini unajua sababu pale upande wa Kenya samaki zinanunuliwa shilingi 1,950 lakini hapa kwetu shilingi 1,450 sasa ukiangalia tofauti ya shilingi 500 kwa maana kwamba bei wanayolipwa haikidhi na hailingani na gharama halisi ya uendeshaji wa biashara ya uvuvi. Kwa hiyo na hilo Waziri wa Maliasili nadhani anahitaji kuliangalia kwamba atashughulika nalo kwa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka nigusie Wizara ya Afya. Kwenye Wizara ya Afya mimi nakumbuka katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi wakati tunajinadi tumekuwa tukisema kwamba wazee watapata matibabu bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya muda naomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Rais wetu; na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza, na mimi pia nichukue nafasi hii kuungana na wenzangu kuwapongeza viongozi wetu walichukua uongozi na nyadhifa mbalimbali katika Serikali ya Awamu ya Nne.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Jakaya Mrisho Kikwete kwa kupata kura nyingi, nampongeza Rais wa Zanzibar, Makamu wa Rais, nampongeza Mhesimiwa Spika wa Bunge letu, nakupongeza wewe Naibu Spika, nampongeza Waziri Mkuu, nawapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri na pia nawapongeza Wabunge wenzangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii pia kuwapongeza na kuwashukuru kwa moyo wa dhati wanawake wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa wa Manyara walionipa kura nyingi sana na kuniwezesha kuingia Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kumpongeza na kumshukuru kwa moyo dhati Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuongeza idadi ya wanawake Bungeni kufikia asilimia 30, suala ambalo limetusukuma wengi wetu hata kugombea nafasi hizi na kuweza kungi Bungeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu bali pia kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Manyara na wanawake wa Tanzania kwa ujumla tumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwa kuwateua Mawaziri Wanawake wengi na kuwapa Wizara nyeti, ishara ambayo inaonyesha kwamba ana imani kubwa kwa wanawake na kwamba wanaweza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii, kwa sababu nimefanya kazi kwa miaka 14 Wilaya ya Monduli nikiwawezesha kiuchumi, niwashukuru sana wanawake wa Mondulu kwa sababu sifa niliyopata huko Manyara imetokana na sifa walionipa wanawake wa Monduli. Wamefanya kazi nzuri ya kurejesha mikopo waliyopewa na taasisi niliyokuwa naiongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo na shukrani, naomba sasa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Mimi ninaunga mkono kwa asilimia mia moja na baada ya hapo ninampongeza kwa moyo wa dhati kwa kuipa kipaumbele sera ya uwezeshaji wa wanawake kiuchumi. Kwa hakika hotuba ya Mheshimiwa Rais imekuwa dira yetu sisi wanawake na kuwa changamoto kwa wote tutakaotekelleza Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kwa sababu ya ufasaha na jinsi ambavyo imeweza kutuongoza hata sisi amba tuko wachanga katika siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Rais kuwa limetfurahisha sana wanawake kwa sababu hata wakati wa uchaguzi mabango mengi yameweza kuandikwa kwamba

tutawawezesha wanawake kiuchumi na hili nadhani kwa sisi wanawake tumeweza kufurahi na kuona kwamba uongozi huu wa awamu ya nne unatupa matarajio makubwa ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea katika kuchangia suala hili, kwa niaba ya wanawake wa Jimbo la Monduli, napenda pia tumpongeze sana na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Lowassa kwa sababu ninavyozungumza hapa katika Jimbo lake wanawake wengi wameweza kupata mikopo na kuwezesha kiuchumi na hadi Desemba mwaka 2005 wanawake wapatao wengi wameweza kupata mikopo na kwa mantiki hiyo basi nadhani Waziri Mkuu wetu si kwenye Jimbo lake tu atakuwa ni mfano wa kuigwa wa kuendeleza wanawake Tanzania. Kwa hakika nadhani katika kuwezesha wanawake kiuchumi, tuna mfano wa kuiga Wilaya ya Monduli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuendeleza wanawake kiuchumi nadhani zaidi sana ni kuwapa mikopo. Lakini ningependa kutoa maoni kwamba tunaomba Serikali iweze kufikiria kuboresha mazingira ya utowaji ama uvezeshaji wa wanawake kiuchumi. Kwa mfano, fedha unazotoa kama mkopo kwa mwanamke unatarajia arejeshe na kwa mantiki hiyo basi inambidi afanye biashara. Sasa kama mwanamke hata kuwa na nyezo ama mazingira ya kuboreshwa, kwa mfano maji, ama umeme, kwa sababu katika vijiji vyetu Tanzania vijiji vingi hatuna umeme, kazi hii haitaweza kufanywa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni mazingira magumu sana kuendesha biashara sehemu ambazo hakuna umeme. Akinamama wengi wanapenda biashara ya mama lishe kwa mfano. Kama hatoweza kuhifadhi vyakula vyake ama malighafi ambayo atatumia katika kufanya hiyo biashara itakuwa vigumu kufanikisha biashara yake. Suala la maji ni suala ambalo linaathiri sana wanawake wengi Tanzania hususani Majimbo yetu haya ya Mkoa wa Manyara na hata Arusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani sitakwenda kugombea Wilaya ya Monduli, wale wenzangu wasiwe na wasiwasi. Lakini natoa uzoeufu kwamba suala la maji akinamama wengi wanatumia muda mrefu sana kutafuta maji na hakika watakapopata mikopo watapoteza muda katika kutafuta maji na kushindwa kufanya biashara zao. Kwa hiyo, natoa wito hasa hasa kwenye kusisitiza kwa ajili ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya basi tuanze na kuboresha mazingira ili tuisiachwe nyuma hasa sisi wa Mkoa wa Manyara amba mazingira yetu kwa kweli yanakuwa na ugumu fulani katika kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito pia kwa wanawake Wabunge wenzangu amba tuko hapa. Nadhani Serikali yetu ina matarajio makubwa. Kila moja ametoka katika Mkoa wake. Ninajua kwamba kipaumbele ataupa Mkoa wake lakini najua kwamba tulioko hapa wengi wetu tuna uzoeufu mbalimbali na wanawake Watanzania wana matarajio makubwa kwetu sisi. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kuomba ushirikiano wa dhati tushirikiane uzoeufu ili tuweze kuwaendeleza wanawake Watanzania kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikifika hapo ninaomba kusema kwamba ninaunga mkono kwa mara ya pili hotuba ya Mheshimiwa Rais, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika asante. Kwa kuwa na mimi hii ni mara yangu ya kwanza kuongea ndani ya Bunge hili Tukufu, napenda niungane na wasemaji wote waliopita kwanza kabisa kushukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu.

Pili napenda nikupongeze wewe mwenyewe lakini awali ya yote ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana na hatimaye kukipa Chama cha Mapinduzi kuwa ni Chama Tawala ambacho kimeshinda kwa kishindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niwapongeze viongozi wengine wote ambao walipata nafasi ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wetu, Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu Mawaziri. Lakini pia na mimi naungana na wasemaji waliotangulia kumshukuru sana Rais wetu kwa kuwa ni mtekelezaji wa ahadi zake. Wakati anapita kwenye kampeni alitoa ahadi akasema kwamba atatoa nafasi nyingi kwa wanawake katika Serikali hii na ametimiza. Kwa kweli namshukuru sana na kumpongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaungana na wanawake wote waliopata nafasi hizi kubwa katika Wizara kubwa kwamba tutashirikiana nao kwa dhati kabisa ili tuweze kuonyesha nguvu zetu wanawake kwamba tunaweza kutenda.

Basi nikiingia katika kuchangia, hotuba ya Mheshimiwa Rais kwanza kabisa, naomba nianze na jambo ambalo limekuwa likizungumziwa sana, jambo la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekumbwa na janga la njaa. Janga la njaa ni jambo ambalo ni aibu sana katika Taifa letu. Suala hili lilitakiwa kuangaliwa mapema sana ilikuwa sio suala la kuanza kukimbizana sasa hivi. Lakini sasa kwa sababu yameshatokea, tusiendelee tena kukaa vikao kwa sababu kadri tunavyokaa vikao ndivyo watu wanavyozidi kufa. Ni kweli kabisa kuna sehemu zingine chakula hakijafika, sasa kama tutaendelea kutuma wataalam kwenda kufanya utafiti na kuchunguza tutakuwa tunazidi kupoteza muda na watu watakuwa wanazidi kufa. Hapa suala ni kunyanyuka na kupeleka chakula kwa hali yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba Serikali hii ichukulie jambo hili kama vile tunavyoweza kuchukulia maafa mengine kama ya mafuriko au ugonjwa wa kipindupindu ili kuweza kwenda kuokoa hawa watu. Itakuwa ni aibu sana kama ataokea mtu atakufa kwa sababu ya njaa na Rais wetu alishatangaza kwamba hakuna atakaye kufa na njaa. Kwa hiyo, ninaomba sana suala hili litiliwe mkazo, ni kunyanyuka na kupeleka chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu upande wa elimu. Ni kweli mikakati ni mizuri, tumeona kabisa kwamba kuna watoto waliofaulu lakini wamekosa nafasi za kuingia sekondari. Katika Mkoa wa Singida

wakati napita kwenye kampeni shule za sekondari za Kata zilikuwa zimeshajengwa zimefikikia kiwango cha kupewa hela kutoka MMES. Lakini zile pesa zinachelewa. Kwa hiyo ninaomba sana, kuna watoto zaidi ya 7,000 ambaو wanasubiri kuingia kidato cha kwanza zile pesa ziende haraka ili kuweza kumalizia zile shule watoto wale wapate kuingia waweze kuijiunga na masomo ya sekondari ili kupunguza wingu la watoto wasio kuwa na makazi au kazi maalum matokeo yake ndiyo tunakuja kupata vijana wengi wanaokimbilia mijini kwa kutokuwa na ajira. Kwa hiyo, ninaomba sana fedha za MMES zipelekwe katika shule za Sekondari za Kata ili zikamaliziwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni shule za sekondari za Tarafa. Shule hizi ni za kutwa. Watoto wengi wa kike na wakiume wanapanga kwenye nyumba za watu. Watoto wanaofanikiwa kumaliza kidato cha nne ni wavulana. Lakini watoto wa kike wamekuwa wakiishia njiani. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ifanye mpango shule hizi zipatiwe hosteli kwa ajili ya wasichana ili waweze kuwa salama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu afya. Mkoأ wa Singida ni Mkoأ mkubwa sana. Sehemu zingine hakuna usafiri, usafiri ni wa baiskeli au kwenda kwa miguu. Hospitali zimekuwa aidha katika Tarafa kwa hiyo unakuta mama mjamzito au watoto wanapopelekwa katika hospitali zile wataalam wanakuwa ni wachache kutokana na hali ile mtoto au mama anapotaka kujifungua anatakiwa aende katika hospitali ambayo anaweza akapata Daktari Bingwa wa tatizo alilonalo lakini mama yule hufia njiani kutokana na kwamba hakuna usafiri wa kuweza kumfikisha haraka mahali ambapo anatakiwa apate huduma. Ninaomba Serikali hii ili kuweza kufanya kila Mtanzania akajisikia anapata huduma bora kutoka kwenye Serikali yake angalau kuwe na gari moja kila Tarafa sio lazima iwe ni *ambulance*, hata gari za kawaida kwa ajili ya kubeba wagonjwa kuapeleka mahali ambapo watapata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye ajira ya vijana, vijana wengi wanaotizamwa sasa hivi ni wa mijini kwamba ndiyo hawana ajira. Lakini ujue vijana hao waliopo mijini wamerundikana kutoka vijiji. Wamekimbilia vijiji kwa sababu ya hali ngumu za maisha. Kwa hiyo, kuna kila sababu Serikali ichukue jukumu la kuwawezesha vijana waweze kutulia vijiji, wawatengenezee mazingira mazuri wabakie kule kule wanakimbilia mijini kwa sababu hakuna umeme wahasikii redio, hakuna TV hawawezeshwi kwa kitu chochote. Kwa hiyo, Serikali iwawezeshe vijana waweze kubakia vijiji. Hata michezo, michezo inaangaliwa sana mijini lakini vijiji kuna vijana wenye vipaji kabisa. Waimbaji, waigizaji wacheza mpira, basi Serikali irudi kule ikawaangalie wale vijana iwawezeshe waweze kutulia kule kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakwenda kwenye mazingira. Katika upandaji miti, kuna miti inayoharibu vyanzo vya maji. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali ichukue jukumu inapohimiza upandaji wa miti basi itume wataalam ikafanye utafiti kwamba ni miti gani hapa inafaa na miti gani hapa haifai ili tusiweze kuharibu vyanzo vya maji na katikati ya miji kwenye vijiji basi watu wahimizwe kupanda miti ya matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunifanya kuwa kitinda mimba katika kuchangia hoja hii.

Napenda kuchukua nafasi hii, awali kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ushindi wa kishindo alioupata katika uchaguzi mkuu uliopita. Vile vile niwapongeze wana CCM wa Mkoa wa Singida na wananchi kwa ujumla jinsi walivyomuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kupata nafasi ya pili katika wingi wa kura. Vile vile hata wakati Mheshimiwa Rais anatafuta wadhamini Mkoa wa Singida ulishika nafasi ya kwanza. Kwa hiyo inaonyesha ni jinsi gani Mkoa wa Singida ambavyo ulikuwa na imani na Mheshimiwa Rais.

Naomba nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kura za kishindo alizopata katika uchaguzi wa Spika wa Bunge let. Nikupongeze pia wewe kipekee Mheshimiwa Naibu Spika kama mwanamke mwenzangu kwa nafasi nzito uliyopata ambayo imeweka historia kwa wanawake. Mungu akutangulie, akubariki sana ili uweze kuitumia nafasi hiyo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote na Manaibu Waziri, Wakuu wa Mikoa pamoja na wajumbe wa NEC kwa ushindi walioupata na kwa wale waliopata uteuzi wa Rais, Mungu awatangulie katika nafasi zao ili waweze kuzitumikia vyema kwa lengo la kuleta maendeleo kwa Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia Wabunge wenzangu kwa heshima waliyoipata ya kuingia hapa Bungeni inaonyesha ni jinsi gani wananchi wao walivyokuwa na imani na wao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kwa wanawake wa Mkoa wa Singida na wananchi kwa ujumla kwa heshima walionipa kwa kunipa kura za kishindo ambazo zinanipa deni la kwa jinsi gani niwatumikie ili niweze kulipa kura zao walizonipa za ushindi wa kishindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, sasa naomba niingie katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nikianza na suala zima la chakula. Naipongeza sana Serikali kuwa imeona umuhimu wa kuwapelekea chakula wananchi waliokumbwa na njaa kwa haraka, lakini ugawaji wa chakula hauendi vizuri. Ninaomba Serikali itilie maanani, imulike kuona wananchi wanagawiwa chakula kwa jinsi Serikali ilivyokuwa imetarajia. Kwa sababu kaya zinagawiwa kilo 14 kwa mwezi hivi kilo 14 kwa kaya yenye watu 10 zitatosha? Ninaomba Serikali ilitazame upya suala hili, yenewe imegawa mgao mzuri lakini Watendaji hawatekelezi ipasavyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ugawaji wa chakula kwenye miji yetu inasahaaulika. Kwa mfano Mji wa Singida una vijiji 19 ambavyo vina wakazi wanaoishi kwa kutegemea kilimo nao wamekumbwa na hili janga la njaa. Ninaomba miji yetu isisahaaulike kupewa chakula ipate mgao sawa kama vijiji vingine vinavyogawiwa ama

Majimbo mengine ambayo yako vijijini kwani wote hawa ni Watanzania wetu na wote wamekumbwa na janga la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kuongelea suala la usalama wa raia. Kwa kweli ujambazi umekithiri katika nchi yetu tunatakiwa sasa tujipange upya. Naomba Jeshi la Polisi lijipange ni wakati muafaka sasa wa kufichua majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitaka kufanikiwa, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wawe wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge ndio wanaoishi na Watanzania, ndio wanaoishi na wananchi, ndio wepesi wa kupewa taarifa na mwananchi wa kawaida. Ni kazi kubwa kumkuta *RPC*, kumkuta Mkuu wa Mkoa, kumkuta *DC* na kumpa taarifa ya jambazi lakini ni rahisi kwa mwananchi kumpelekeea taarifa Mbunge wake. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge wakiwa wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama tutatoa hali halisi ya majambazi wetu wako wapi na wanafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wetu wanaenda Dar es Salaam kibiashara na kufanya shughuli mbalimbali na Wizara zetu nyingi ziko Dar es Salaam. Sasa ujambazi ulikithiri uko Dar es Salaam, ninaomba Dar es Salaam igawanywe, Dar es Salaam ina wakazi wengi sana watu hawa wengi wameshamzidi Tibaigana nina hakika kasharusha buti yake vya kutosha kashagonga mwamba. (*Makofi*)

Dar es Salaam kidola igawanywe tupate ma-*RPC* wawili, watatu ikiwezekana hata kila Manispaa iwe Mkoa. Nina hakika tukifanya hivyo tutaweza kulidhibiti Jiji letu la Dar es Salaam katika suala zima la ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ulinzi kwa kweli bado linahitaji hekima na busara, tujifunze mbinu mpya za kuangalia ulinzi wa nchi. Nataka nitoe mfano mmoja tu. Singida ilikuwa na ujambazi ulikithiri miaka ya nyuma, tukaletewa *RPC* mmoja Bachubira. Huyu bwana aliweza na sasa hivi ingawa anaumwaumwa lakini yupo hai, yuko Makao Makuu ya Polisi, nendeni mkamuulize mbinu alizotumia yule bwana. Alikuwa anavaa mpaka kaputi, anavaa nguo za ajabu ajabu anaingia maeneo ambayo ni magumu lakini aliweza kuwakamati majambazi yeze mwenyewe bila kutegemea hata Maaskari wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tujaribu kutumia mbinu mpya kabisa ili tuweze kumaliza suala hili la ujambazi. Hawa wawekezaji wetu tunawapa mabenki wanatafuta riziki zao na sisi wanatuhudumia lakini kwa nini majambazi yatuzidi? Wanatuwekea walini wenyewe rungu kwa sababu wanaoweka pesa pale ni Watanzania. Ninaiomba Serikali iwawekee sheria ngumu hawa wawekezaji wetu waweze kuweka walini wenyewe silaha ili Watanzania wetu waweze kuwa na amani katika uwekaji wa pesa na katika uchukuaaji wao wa pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niambie sasa hivi madawa ya kulevyia yalivyokithiri, yanaingiaje? Watumiaji hatuwajui, waingizaji hatuwajui, tunawafahamu vizuri sana na

kwa nini tuwafiche. Ni wakati muafaka sasa kufichua vitu kama hivyo vinaleta aibu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba niongelee suala la umaskini. Umaskini nashukuru sana Mheshimiwa Rais amesema sasa ni wakati muafaka kwa Watanzania kuondokana na umaskini hasa akina mama. Je, tumewawezesha? Sasa hivi sio wakati wa kuwakopessa shilingi 50,000 au 100,000 ni wakati wa kuwapa mikopo mikubwa, wanahitaji miradi mikubwa sasa huwezi kulima hekari 10 au hekari 50 kwa kupata mkopo wa 100,000. Naomba tuwawezeshe akina mama.

Tunashukuru kwamba sasa kuna mfuko uliowekwa kwa ajili ya kukopesha watu wanaohitaji kujiendeleza lakini unafahamika? Serikali itoe elimu kwa wananchi wetu hasa akina mama wajue watapata wapi, ni taratibu zipi ili waweze kuondokana na umaskini uliokithiri na wale kina mama wanaofanya miradi mbalimbali wawezeshwe mahali pa kupeleka biashara zao, bidhaa zao zinakosa soko kwa sababu hawajui wapeleke wapi? Nina hakika tukiwafuatilia akina mama hawa tuwasaidie tutakuwa tumewakomboa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala zima la ajira kwa vijana. Naipongeza Serikali imetoa kipaumbele kwa ajira ya vijana. Hivi vijana wenyewe wanajulikana mahali walipo, takwimu zipo zenye kuonyesha idadi, tumewaandaaje? Sasa hivi ni wakati muafaka wa kuwaandaa vijana na kujua mahali walipo na idadi yao na tuwaanzishie namna ya kuwfanya waweze kuyamudu maisha. Kama ni kujiunga na Jeshi, tupunguze taratibu zingine ambazo Hazina msingi mnaweka miaka 24 mwisho, huyu wa 29 mnampelika wapi? Vijana wetu wanakwenda mpaka miaka 35 hivyo tuhakikishe vijana hawa tumewaandalia mazingira ya kuweza kujajiri. Amesema Mheshimiwa Rais kwamba vyuo vya *VETA* vitakuwepo mpaka Wilayani sasa jeshi la mwamvuli kazi kwenu. Hakikisheni *VETA* sasa zinaenda Wilayani zihame Mikoani ili vijana hawa waweze kupata elimu ambazo zitawafanya wajajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda niongelee suala zima la kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji. Tungekuwa tumeanzisha kilimo hiki cha umwagiliaji mapema hata janga la njaa lisingetukuta. Tuna mabonde mazuri kabisa ....

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema, huyu ndio msemajii wetu wa mwisho na baada ya kuwasiliana na mtoa hoja amesema tumezungumza kwa muda wa siku nne tena kwa dakika kumi kumi kwa hiyo tumezungumza wengi sana. Kwa hiyo tuahirishe kikao sasa kusudi tuwaachie upande wa mtoa hoja na wasaidizi wake wajipange vizuri.

Kesho asubuhi baada ya maswali wataanza kuchangia, kwanza Mawaziri wengine wote watakuwa wanachangia mtoa hoja ni mmoja tu Waziri Mkuu. Hawa wachangiaji wa kesho watarudi kwenye kanuni yetu ile ya dakika 15, halafu Mtoa hoja yeoyote ni dakika 60 kwa hiyo watajipanga wanavyoona inafaa.

Baada ya kusema hayo, nasitisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.59 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne  
Tarehe 14 Februari, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*